ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 4 Julai, 2012

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida na leo tumetembelewa na Wageni ambao ni Makundi Mawili. Kundi la Kwanza ni wageni wetu ambao ni wanafunzi wa Skuli ya Maungani Jimbo la Dimani ambao ni jumla ya wanafunzi hamsini na walimu wao watatu.

Kundi la Pili ni wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, hao ni wageni wa Mwenyekiti wetu Mhe. Mgeni Hassan Juma na wanatoka kitengo cha *Political Science* wanasomea *International Relation*.

Na Mhe. Mgeni yupo tayari na wageni wake wako pale ambao wamekuja kumshuhudia yeye na wenzake wakifanya kazi katika Baraza hili. Wageni wetu nakushukuru sana na karibuni sana na Waheshimiwa Wajumbe Ahsante sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 47

Uharibifu wa Mazingira

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekuwa ikitoa matamko na kauli mbali mbali kuhusiana na uharibifu wa mazingira kwenye maeneo ya ardhi, fukwe na bahari za Zanzibar.

(a) Je, tokea mwezi Novemba 2010 hadi sasa, kuna kesi ngapi zilizoripotiwa au kufanyiwa utafiti na kugundulika kuwa zinahusu uharibifu wa mazingira.

(b) Hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wahusika wa uharibifu wa mazingira ulioripotiwa au kugundulika katika kipindi hicho.

(c) Ni wahusika wangapi waliochukuliwa hatua za kisheria, wangapi waliotiwa hatiani na wangapi waliopewa adhabu kutokana na makosa ya uharibifu wa mazingira katika kipindi hicho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi napenda kutoa maelezo yafuatayo:-
Kama tunavyofahamu kuwa suala la mazingira ni mtambuka, ingawa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imepewa jukumu la kusimamia, lakini kuna taasisi mahususi ambazo zimepewa jukumu la kusimamia sehemu mahususi za mazingira. Kwa mfano:-

- Wizara ya Kilimo na Maliasili imepewa jukumu la kudhibiti uharibifu wa misitu na maliasili zisizorejesheka.

- Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepewa jukumu la kudhibiti uharibifu wa mazingira ya bahari kama ule unaotokana na matumizi ya njia za uvuvi zinazoharibu mazingira.

- Afisi ya Rais Tawala za Mikoa kupitia Manispaa, Mabaraza Miji na Halmashauri za Wilaya imepewa jukumu la kudhibiti uchafuzi wa mazingira hasa unatokana na taka na maji machafu katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Pale ambapo Sheria za Taasisi husika itakuwa haijaeleza au inakasoro kwa jambo fulani basi Sheria ya Mazingira inaweza kuchukua nafasi kwa suala hilo.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo kila taasisi ina utaratibu wa namna ya kuweka kumbukumbu za mambo yake ambayo hata hivyo tumekuwa tukishirikiana kwa kiasi fulani ili kujua nani anafanya nini na kuepuka jukumu moja kufanywa na taasisi mbili kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira inaweza kueleza mazingira ya aina yoyote yakiwemo ya uvuvi, misitu, maliasili zisizorejesheka, au uchafuzi wa taka na mengineyo. Mengi ambayo husimamiwa na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kama vile mabadiliko ya tabia nchi.

Aidha Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imekuwa na tabia ya kuwasiliana na taasisi husika ili ziweze kufatilia masuala ya mazingira ambayo ama yatawasilishwa na wananchi kuwa ni kero au itaona ni tatizo la kimazingira linalolihusu taasisi mahususi. Hii ndio sababu Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imekuwa ikitoa matamko na kauli mbali mbali kuhusiana na haribifu wa mazingira kwenye maeneo ya ardhi, fukwe na bahari ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya kina sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo na ambazo tumeweza kuzikusanya kutoka taasisi mbali mbali tunazoshirikiana nazo katika suala hili la usimamizi wa mazingira, zinaonesha kwamba tokea mwenzi wa Novemba 2010 hadi Mei 2012, jumla ya kesi 222 ziliripotiwa kuhusika na uharibifu na uchafuzi wa Mazingira.

(b) Kulingana na ukubwa wa tatizo la uharibifu wa mazingira hatua mbali mbali zimechukuliwa dhidi wa wahusika wa uharibifu wa uchafuzi wa mazingira ulioripotiwa katika kipindi hicho. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuonywa na kusamehewa, kutaifishwa kwa vifaa vilivyokamatwa kwa vile wahusika wamekimbia hasa kwenye uchukuaji wa mchanga kwa gari za punda au ng'ombe na mitego ya uvuvi. Wahusika hutakiwa kuondoa majengo waliyojenga na kuharibu mazingira, kukamatwa na mifuko wa plastiki. Lakini pia wengine walifikishwa kwenye vyombo vya sheria ikiwemo Polisi na Mahakama.

(c) Jumla ya wahusika 204 wamelichukuliwa hatua za kisheria ambapo wahusika wote 204 walitiwa hatiani na wote walipewa adhabu kutokana na makosa ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika kipindi hicho.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu ya kina na ya ufasaha.
Naomba kumuuliza swali lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, kwa sababu katika majibu yake amekiri kwamba kumekuwa na Idara zilizokuwepo katika wizara tofauti zinazosimamia masuala ya uharibu na uchafuzi wa mazingira. Lakini bado jukumu kubwa la kusimamia hili limekabidhiwa ofisi hii kuwa ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

(a) Ni hatua gani zilizofanywa ili Ofisi hii kuona kwamba ndio iliyokuwa msimamizi mkuu na inazisimamia Ofisi nyengine zote katika serikali katika suala hizi zima la uharibu wa mazingira

(b) Katika kesi mbali mbali alizozitaja nilikuwa nataka kujua kwamba moja katika maeneo ambayo yameripotiwa sana ni suala zima la uharibifu wa mazingira kwa ujenzi katika fukwe hasa unaofanywa na wawekezaji wa ujenzi wa mahoteli ya kitalii. Wizara imegundua kuna hoteli ngapi ambazo zimekiuka sheria za mazingira. Na ngapi zimechukuliwa hatua kwa kutakiwa kubomoa yale maeneo waliyojenga katika maeneo ya fukwe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika,

(a) Kwa kuona muhimu kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira ndio yenye jukumu kubwa katika kuzimamia na kutoa miongozo ya kisera juu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mhe. Spika, utakumbuka kwamba Wakati nawasilisha bajeti yangu hivi juzi nilieleza kwamba Sera ya Mazingira ambayo ndiyo inatuongoza juu ya usimamizi mzima wa rasilimali na uchafuzi wa mazingira ni ya muda mrefu sasa tokea mwaka 1992. Tumeigundua kwamba ina mapungufu na tumeshaifanyia marekebisho ili iweze kutuelekeza vizuri katika maeneo ya usimamizi. Hivi sasa karibu itapelekwa katika

Kamati ya Makatibu Wakuu kabla Wajumbe wako hawajapata nafasi ya kuiyona. Ili baadaye itupe fursa ya kuirekebisha Sheria nzima ya Mazingira ambayo kwa sasa ina mapungufu ambayo inainyima Idara ya Mazingira kuweza kusimamia vyema majukumu yake.

(b) Mhe. Spika, suala la takwimu nimkumbushe tu Mhe. Mwakilishi kwamba katika kitabu change cha bajeti taarifa hii imo kwa ukamilifu ni vizuri akarejea kitabu hicho, nina hakika kitabu hicho anacho wakati nawasilisha bajeti. Kuna takwimu zote ambazo tumezieleza katika hicho kitabu na hatua ambazo zimechukuliwa.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Naomba kama kanuni zetu zinavyojielekeza kwamba Waziri atujibu swali. Mheshimiwa kitabu tunacho, lakini kilichokuwemo katika kitabu ni orodha ya hoteli zilizokaguliwa na hata katika mchango wangu katika Ofisi hii nilisema kwamba kitabu kile katika takwimu zile hazijielezi ni hoteli ngapi zimegundulikana zimekiuka sheria na ngapi zimechukuliwa hatua zipi. Kuna orodha tu ya mahoteli ambazo zimekaguliwa kwa mwaka mzima. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri ajibu swali langu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimletee taarifa hiyo kwa kuwa ni ya takwimu na orodha ni mkubwa mno ili uwe sahihi naomba nimletee kwa maandishi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali mojia la nyongeza.
Pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri na nakushukuru sana kwa majibu yako, lakini utakubaliana nami kuwa hivi sasa Zanzibar imekabiliwa na mmong'onyoko wa ardhi ambayo maji hupanda juu na ardhi kumong'onyoka kutokana na mabadiliko haya ya tabia ya nchi.

Je, Mhe. Wiziri una wito gani kwa wananchi ili Zanzibar kwa ujumla ili kujikinga na mabadiliko haya ya nchi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ni kweli kwamba Zanzibar inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa Mazingira hasa katika sehemu za fukwe. Wito ambao naweza kuutoa kwamba pamoja na kukabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi ambayo mengine yapo nje ya uwezo wetu kama wanadamu ni mambo ambayo yanatokea kwa sababu kuna mabadiliko ya tabia nchi. Lakini yamo ambayo sisi wenyewe kama wanadamu tunayachangia kwa mikono yetu kwa shughuli ambazo tunazifanya.

Naomba kuwasihi sana wananchi wa Zanzibar waacheni na tabia ya kukata miti ovyo hasa katika sehemu za fukwe. Miti ya aina ya mikoko na mengine ili kuzuia mmong'onyoko wa ardhi. Vile vile kwa wawekezaji na wananchi kwa jumla kuacha kujenga katika maeneo ya fukwe ili kuzuia mmong'onyoko huo. Pia kufanya jitihada za makusudi kuweza kupanda miti kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Nam. 96

Mfumko wa Bei na Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kazi yake kubwa ni kusimamia mwenendo wa ukuaji wa uchumi na kutoa taaluma ya njia bora ya kupunguza mfumko wa bei na mikakati ya kukuza uchumi wa nchi ya Tanzania ikiwemo Zanzibar.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inanufaika vipi na BoT katika mikakati yake ya kupunguza mfumko wa bei ambao hadi Januari umeripotiwa kufikia asilimia 17% na kuathiri wananchi wakiwemo wanyonge.

(b) Serikali ya Zanzibar ina mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wake (MKUZA). Je, serikali imenufaika vipi na BoT katika utekelezaji wa mpango huo.

(c) Kwa kuwa SMZ inaaminika kuwa na hisa ya asilimia 11% ya kuanzishwa kwa (BoT) Je, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Zanzibar imepata gawio la kiasi gani cha faida kupitia Benki hiyo.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Alijibu:-

Mhe. Spika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 96 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo.
Mhe. Spika, mfumko wa bei kwa hapa Zanzibar unasababishwa na mambo yafuatayo.

1) Uagiziaji mkubwa wa bidhaa za chakula hasa mchele, sukari na unga wa ngano kutoka nje ya nchi.

2) Kuendelea kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

3) Kiwango kidogo cha usafirishaji nje wa bidhaa mbali mbali.

4) Tatizo la kukatika kwa umeme kusikotarajiwa amapo kunapelekea kupungua kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa na huduma.

5) Kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya msingi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Mapinduzi katika mikakati yake ya kupunguza mfumko wa bei inapata manufaa kutoka Benki Kuu ya Tanzania katika maeneo yafuatayo.

   i) Kudhibiti mzunguko wa fedha ili mahitaji ya fedha yalingane na mahitaji ya bidhaa na huduma zinazotolewa Zanzibar.

   ii) Kudhibiti thamani ya shilingi ya Tanzania ili iwe na nguvu zaidi.

   iii) Kutunza fedha za kigeni za kutosha kwa lengo la kuisaidia serikali wakati inapohitajia badala ya kuzinunua kutoka nje ya Benki Kuu.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inao mpango wake wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wake. Hata hivyo katika kufanikisha mpango huo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imenufaika kutoka Benki Kuu ya Tanzania katika mambo yafuatayo:-

(c) Benki kuu ya Tanzania imeshiriki kikamilifu katika utayarishaji wa MKUZA pamoja na uchambuzi wa ukuaji wa uchumi na mwenendo mzima wa mfumko wa bei. Benki kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na serikali imeanzisha Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiri Amali Wadogo Wadogo pamoja na wale wanaosafirisha bidhaa nje. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/201, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea gawio la faida la shilingi bilioni 7.8 kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri, marefu na ya kisiasa ya Mhe. Waziri; Je, BoT imetoa mchango gani wa kifedha angalau kusaidia kupunguza mfumko wa bei badala ya ushauri na utekelezaji wa mpango wa kukuza uchumi.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, BoT haijatoa msaada wa fedha zozote kwa sababu sio taasisi ya kutoa fedha kwa serikali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Wakati uchumi wa nchi unapokuwa kwa asilimia 6.8, na mripuko wa bei unapokuwa kwa asilimia 17 kwa manufaa gani kwa wananchi katika hali hii ya mkanganyiko.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi ni kitu tofauti sana na mfumko wa bei, ukuaji wa uchumi unasababishwa na bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani na mfumko wa bei unaotokana na kupanda kwa bei za bidhaa ambazo zinazouzwa ndani.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Swali langu halikutaka kujua tofauti ya mambo mawili haya. Nilitaja takwimu kama ukuaji wa uchumi nilisema asilimia 6.8 wakati mfumko wa bei ni asilimia 17. Je, kwa wananchi kuna manufaa gani.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza ajieleze manufaa kwa wananchi ukuaji wa uchumi manufaa kwa wananchi mfumko wa bei, kipi ambacho anakusudia yeye.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mheshimiwa ufafanuzi ni kwamba mfumko wa bei ni mkubwa kuliko ukuaji wa uchumi. Je, hapo wananchi wananufaika au wanakula hasara katika nchi. Kwa kikawaida mfumko wa bei unatarajiwa uwe chini ya ile asilimia ya ukuaji wa uchumi ndio wanavyonufaika wananchi. Kwa hapa Zanzibar mambo yanakuwa vipi?

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nasoma bajeti ya taifa nilitoa takwimu ambazo zimeonesha kwa kina karibu duniani kote ukuaji wa uchumi umekuwa mdogo kuliko mfumko wa bei. Nilizieleza kwa kina sababu zilizopelekea mfumko wa bei kuwa mkubwa. Mfumko wa bei unapokuwa mkubwa kuna muathiri sana mwananchi wa kawaida.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa BoT ni Benki ya Muungano na kwa kuwa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali amesema Zanzibar tumepata milioni 5 na kitu kutokana na gawio la fedha hizo. Napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa Zanzibar ugavi wetu maalumu tunaopata kutoka Tanzania ni 4.5. Namuuliza Mhe. Waziri je, kigezo hicho cha fedha tulizopewa kimezingatia kigezo hicho. Na je, ni faida ya kiasi gani ilipatikana mpaka tukapata milioni 7.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako naomba kujibu swali la kaka angú Mhe. Subeit kama ifuatavyo.

Nimesema kwamba gawiwo la faida tulilolipata ni bilioni 7.8 na hiyo tumeipata kwa kuzingatia asilimia 4.5 ukitaka kujua faida yote iliyopatikana basi hii tuliyopata sisi asilimia 4.5 basi faida itakuwa ni asilimia 100. Ukifanya hesabu unaweza ukajua, lakini kama unahitajia mimi kupatie nitakupatia baadaye.

Nam. 153

Suala la Mfumko wa Bei

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kunipa nafasi hii na kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali lililotangulia ambalo linafanana sana na langu. Kwa sababu hiyo Mhe. Spika, naomba kifungu (b) cha swali langu asikijibu kwa sababu tayari ameshalijibu katika swali la Mhe. Jaku la Nam. 96 badala yake anijibu swali langu kifungu (a) na (c) Naomba swali langu sasa lijibiwe.
Aliuliza:-
Katika mwezi wa Mei, 2012 ripoti za Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) zilieleza kwamba kiwango cha mfumko wa bei kwa upande wa Tanzania Bara kilifikia asilimia 19.

(a) Kwa upande wa Zanzibar, kiwango cha mfumko wa bei kimefikia asilimia ngapi na kiwango kama hicho huwa kinapimwa kutoka msingi (*base*) wa muda gani.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea mfumko wa bei kupanda kwa kasi kubwa hapa Zanzibar katika miaka ya karibuni.

(c) Je, Zanzibar kukosa uwezo na udhibiti wa kupanga sera zake za fedha na uchumi hasa katika maeneo ya sarafu na kodi *(fiscal and monetary policies)* na badala yake mamlaka hayo kuwa kwenye taasisi za Muungano kama vile BoT na TRA kunadhoofisha kwa kiwango gani jitihada za kudhibiti mfumko wa bei ndani ya Zanzibar.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mjimkongwe kwa kutanabahi kwamba swali lake la (b) nimeshalijibu na kuniruhusu nimjibu (a) na (c). Nadhani sisi wengine tutaiga mfano wako, kama swali limeshajibiwa basi tusilirudie.
Mhe. Spika kwa heshima kubwa naomba kujibu swali Nam. 153 lake lenye kifungu (a) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar katika mwezi wa Mei 2012 Mfumko wa bei umefikia asilimia 11.6 na mwezi Juni umefikia asilimia 9.9. Kasi ya mfumko wa bei inapimwa kwa kila mwezi na kila mwaka kwa kutumia bei za bidhaa mbali mbali zinazotumiwa mara kwa mara na wananchi wetu.

(c) Mhe. Spika, duniani kote sera za fedha zinadhibitiwa na Benki Kuu ya Nchi yaani *(Central Bank)* na sio serikali. Serikali nayo inadhibiti sera za kodi. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia tunadhibiti sera za kodi isipokuwa kodi ya ushuru wa forodha, kodi ya mapato yanayotokana na Makampuni na ushuru wa bidhaa.

Hata hivyo jitihada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kudhibiti mfumko wa bei ndani ya Zanzibar zinatia moyo zaidi ukilinganisha na zile za wenzetu Tanzania Bara. Mfumko wa Bei Zanzibar mnamo mwezi Mei ulifikia asilimia 11.6, ukilinganisha na ule wa Tanzania Bara asilimia 19.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, na namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa majibu mazuri ya kitaalamu yaliyokuwa yamejielekeza katika maswali yaliyoulizwa.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika jibu lake lililotangulia kabla yangu Mhe. Waziri alisema moja ya manufaa tunayoyapata kutoka BoT kwa kuwa ndio dhamana wa suala la Sera za Fedha kwa pande zote mbili au nchi zote mbili zinazounda muungano. Pamoja na kutoa mikopo kwa njia ya SMEs *(Small and Medium Enterprises)*.

Swali langu kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kwa upande wa Zanzibar kwamba huduma hii haikuwafika pamoja na kuorodheshwa mabenki mengi ambayo yana matawi mengi hapa Zanzibar lakini Wazanzibari hawakupata manufaa haya. Anaweza kunieleza ni kwa nini Wazanzibari hawanufaiki katika huduma hii ambayo Zanzibar inahisa ya asilimia 11.02, mbali ya kuwa ni m-bia kupitia Muungano.

(b) Mhe. Spika, katika majibu yake vile vile ameeleza kwamba BoT inadhibiti Sera za Fedha lakini Sera za Kodi zinadhibitiwa na serikali. Akasema kuwa Zanzibar tunadhibiti kodi zote ukiondoa kodi ya mapato, kodi inayolipwa na mashirika na Ushuru wa Forodha.
Swali langu ni kwamba kwa Zanzibar kukosa udhibiti wa kodi hizo za aina tatu, kunadhoofisha kiasi gani uwezo wake kama Waziri wa Nchi, anayeshughulikia Fedha kwa upande wa Zanzibar kudhibiti uchumi wetu. Anawambia nini wananchi wa Zanzibar juu ya haja ya kuyarejesha mamlaka haya kwa Zanzibar ili kuweza kuudhibiti vizuri uchumi wetu.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika,

(a) Nakubaliana na naye kwamba wananchi wa Zanzibar hawajafaidika na fedha zilizopo katika Mfuko wa SMEs. Hili kwa upande wetu tumeliona, tunajaribu kushea na wenzetu wa BoT, kutokana na taratibu za kupata mkopo ni ngumu. Wenzetu sasa wanafanyia marekebisho taratibu hizo ili basi ziwe nyepesi na wananchi wetu waweze kufaidika na Mfuko huo wa SMEs. Hilo nakubaliana nalo kabisa. Hata juzi nilikuwa na watu wangu wa BoT, tumeliona hilo na wakaniahidi kwamba katika kipindi kifupi watakuwa wamesharekebisha hizo taratibu, ili kila mmoja aweze kunufaika na hizo fedha zilizokuwemo katika mfuko huu. Hilo nakubaliana naye kabisa.

(b) Nataka niseme kwa kiasi fulani ukikosa udhibiti wa baadhi ya sera za kodi. Kwa kiasi fulani nakubaliana naye Mhe. Jussa kwamba kunadhoofisha hali yetu ya kuinua uchumi wetu. Hata hivyo katika baadhi ya maeneo kwa mfano kodi ya forodha hasa kwa kuzingatia kwamba eneo la chakula nalo vile vile tunapata unafuu kidogo wa kuweza kupunguza kodi za chakula na kodi za bidhaa nyenginezo kwa ajili ya watu wetu.

Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba kiasi fulani ukikosa udhibiti huo unadhoofisha hali yetu ya uchumi. Hili tunalizungumza ili hatimae liweze kuwa na manufaa kwa Zanzibar na kwa Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, mfumko wa bei kwenye nchi nyingi ulisababishwa pamoja na Mtikisiko wa Kiuchumi na katika kuliona hilo *BOT* walitoa fedha maalum, ambazo waliziita *Stimulus Package* kwa zile taasisi ambazo zimekumbwa na mtikisiko wa kiuchumi. Je, kwa Zanzibar SMZ ilipata kiasi gani kwenye hiyo *Stimulus Package*?

(b) Mhe. Spika, hapo zamani SMZ ilipokuwa inaomba fedha *BOT*, yaani fedha za ndani ilikuwa huzipata kwa kununua kwa *dollar*. Je, hadi hivi sasa fedha ya ndani shilingi ya Tanzania SMZ inapoiomba bado huinunua kwa *dollar*.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, wakati ulipotokea Mtikisio wa Uchumi mwaka 2007/2008 SMZ haikupata kitu kutoka *BOT*. (*Makofi*)

Hivi sasa nataka nimueleze ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, kwamba SMZ tunazo fedha za kutosha *local* na pia tunazo fedha za kutosha *foreign*. Kwa hivyo, sisi hatuhitaji kununua kutoka *BOT*, yaani hatuhitaji kununua shilingi wala *local*. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunashukuru Mhe. Waziri na tunaendelea.

Nam. 98

Ukarabati wa Uwanja wa Ndege Pemba

Mhe. Salma Mussa Bilali (Kny: Mhe. Shadya Moh'd Suleiman) – Aliuliza:-

Zanzibar inategemea mapato yake kwa njia nyingi, moja wapo ni njia ya utalii, na ili kupata fedha hizo kwa njia hiyo ni lazima kuwepo kwa miundombinu ya barabara, umeme, maji na viwanja vya ndege vya kisasa.

(a) Je, Mhe. Waziri unatueleza nini kuhusu uwanja wetu wa ndege wa Pemba.

(b) Ni lini serikali itapanua uwanja huo ili kuweza kukua kwa biashara kisiwani Pemba na wananchi waweze kupata ajira kwa kuinua maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Uwanja wa Ndege wa Pemba ni miongoni mwa viwanja vya ndege vya Kiwango cha Kikanda (*Feeder Airport*), na hivyo hautoi huduma za kimataifa. Kwa kweli matumizi makubwa ni kuhudumia kwa ndege za kikanda.

Hata hivyo, kwa muda mrefu tumekuwa na tatizo la kushindwa kutoa huduma za uwanja wa ndege kwa wakati wa usiku kutokana na tatizo la kukosekana kwa taa kiwanjani hapo.

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika kukabiliana na tatizo hilo kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeweza kufanya mazungumzo na kampuni mbili za Afrika ya Kusini, yaani Kampuni ya *Setgat* na *ADB* na kufanya uchambuzi yakinifu na tathmini, na hivyo kutupa tathmini hiyo. Katika kufanikisha suala hili Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika bajeti yake ya 2012/2013 imetenga fedha kwa ajili ya kuanza zoezi hilo la uwekaji wa taa uwanjani hapo, ili kutoa huduma kwa masaa 24.

Katika hatua ya pili ni kuona kwamba tunafanya uchambuzi yakinifu na baadaye kuwasiliana na wenzetu wa *ADB* kwa ajili ya kupata fedha za kuweza kufanikisha utanuzi wa uwanja huo. Mhe. Spika, katika utanuzi huo tunakusudia kufanya utanuzi katika majengo, uwanja wenyewe pamoja na huduma nyengine.

Hata hivyo, katika uanzaji wa jambo hilo pia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imetenga fedha kwa ajili ya kufanya *study* ya kufanikisha mradi huo. Hivyo, uwanja huo lini utajengwa ni pale taratibu hizo tulizozieleza zitakapokamilika.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kweli uwanja wa ndege wa Pemba hivi sasa una matatizo mengi, hata taa uwanja huo hauna endapo itatokezea dharura ya kutua ndege usiku au jambo lolote. Je, Mhe. Waziri ni lini hasa atachukua juhudi za makusudi, ili kuweza kuuwekea taa uwanja ule uweze kunusuru wakati inapotokea dharura. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu mama tumeeleza kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tumefanya mawasiliano na mazungumzo na kampuni mbili.

Kampuni zenyewe ni *Safeget* na *ADB* zote za South Africa, na wao wanatuletea uchambuzi wao na tathmini, na sisi kama wizara tumeweza kutenga fedha katika bajeti ijayo ya 2012/2013 tayari zoezi la uwekaji wa taa litaanza katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi afanye subira na bajeti haiko mbali watupitishie na twende tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, moja kati ya tatizo linalokikabili kiwanja chetu cha ndege kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni ukosefu wa taa kitu ambacho kimepelekea uwanja wetu kutofanya kazi wakati wa usiku, kitu kilichosababisha matatizo makubwa.

Nakumbuka kwamba katika kipindi cha miaka 7 sasa, serikali miaka yote ya bajeti inawasilisha katika Baraza hili, kwamba kuna *program* ya utengezaji, na kipindi cha nyuma walikuwa wakisema hasa uwekaji wa taa. Lakini sasa inaonekana wanaanza kuona haya na kusema uimarishaji wa huduma. Kwa hivyo, mara hii wametenga shilingi milioni 900/= katika bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba anieleze Mhe. Waziri kuna sababu gani kupelekea Baraza kuidhinisha fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa shughuli hiyo na wizara ikashindwa kutekeleza kama vile ambavyo imeahidi? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, inawezekana ikawa Baraza limeidhinisha fedha na katika matumizi wizara ikakutwa na matatizo. Lakini sisi kwa upande wetu kuhusiana na suala hili tulichokisema pengine changamoto kubwa ilikuwa ni kufanya uchambuzi na kujua tatizo halisi pamoja na gharama zake.

Katika kuliondosha tatizo hili wizara yetu katika kipindi hichi chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tumeweza kufanya huo uchambuzi kwa maana ya *study* na kujua gharama halisi inayohitajika, ndio maana tukaahidi kwamba katika bajeti inayokuja sisi tutakachoweza kufanya tutaanza huo utaratibu wa kuweka taa uwanjani hapo.

Kwa hivyo, kama kulikuwa na fedha ambazo zinapitishwa na kushindwa kutumika kwa hilo, pengine kulikuwa na changamoto nyengine za kiwizara katika shughuli za kiutendaji.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuingia katika mchakato wa kupanga mambo yetu.

(a) Mhe. Spika, kwa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri kama alivyoeleza swali mama. Je, Mhe. Spika, katika fedha hizo zilizotengwa kwa Uwanja wa Ndege wa Pemba atakubaliana na mimi kwamba, kwa kweli Uwanja wa Ndege wa Pemba hauna uzio na wakati mwengine mbwa wanapita katika uwanja ule na kuhatarisha maisha ya watu? *(Makofi)*

(b) Ni vyema uwanja ule ukaangaliwa vizuri, kwa sababu juzi nimetoka Pemba Mhe. Spika, kwa kweli lile jengo lenyewe ni shaghala baghala. Je, atakubaliana na mimi katika fedha hizo za upande wa Pemba jengo lile liangaliwe vizuri? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Uwanja wetu wa Ndege wa Pemba hasa upande wa magharibi na kaskazini unakosekana uzio.

Kwa kweli uzio ulikuwepo ambao ni wa muda mrefu na hivi sasa umechakaa kwa maana ya kwamba nguzo zimeoza na kuanguka. Miongoni mwa jitihada zetu kwa kupitia Mamlaka kuona kwamba tunaimarisha au tunajenga uzio mwengine mpya.
Mhe. Spika, katika hili kulikuwa na baadhi ya watu ambao wakilima katika eneo lile, tayari wameshalipwa fidia na kupisha shughuli za uwanja wa ndege, ili kuona kwamba eneo lile lote linamilikiwa na kuhifadhiwa vizuri ikiwemo hilo suala la kuweka uzio chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Vile vile ni kweli kwamba kuna matatizo ya jengo letu haliko katika hali nzuri sana. Lakini kama tunavyosema kwamba kupanga ni kuchagua, kwa muda huu tumeona kwamba jengo tunaweza kufanya ukarabati mdogo mdogo na kuweza kuhimili kuishi.

Kwa hiyo, tumeona kipaumbele na nguvu yetu kubwa tuelekeze katika upande wa uimarishaji wa taa, ili tuweze kutoa huduma kwa Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa masaa 24, ambapo tunaamini kwamba itakuwa ni kichocheo na kivutio cha wasafiri pamoja na wananchi wengine wanaofuata huduma hizo za usafiri kwa ajili ya ndege.

Nam. 137

Usumbufu Uungiwaji Umeme Zanzibar

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:-

Naipongeza serikali kwa kuchukua juhudi za kuwapelekea wananchi huduma za umeme mjini na vijijini, lakini walengwa hasa hawajafaidika na husababisha wananchi wanapokuwa wanahitaji huduma hiyo kupata usumbufu mkubwa na kuchukua karibu miezi 6 au mwaka.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwapatia huduma hiyo wananchi na kuwaondoshea usumbufu unaowakabili?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 137 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali Nam. 115 wizara yangu itaendelea kidogo kidogo kulingana na hali ya mfuko wa fedha na pale inaporuhusu, wizara yangu itahakikisha kwamba vijiji vyote ambavyo havijavutiwa *line*, basi vitapelekewa huduma hiyo ya umeme.

Hata hivyo, tunakubali kwamba kuna wananchi wengi ambao hupeleka maombi yao ya kuunganishiwa umeme, lakini hucheleweshwa kuunganishiwa umeme huo. Kwa hivyo, tunaahidi kwamba suala hili tutalisimamia na litapatiwa ufumbuzi, na tunahakikisha kuwa kila mwananchi ambaye anayeomba huduma hiyo anaunganishiwa kwa wakati unaofaa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa huduma hii ni muhimu kwa kila mwananchi ambaye mwenye uwezo wa kupatiwa huduma hii.

Lakini Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika kijiji cha Kiuyu Minungwini Shehia ya Kiuyu Kigongoni Fingu mpaka leo hii hakijapata huduma hii ya umeme na tayari wanakijiji hao wameshapeleka maombi yao.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwawekea *transformer* katika kijiji hicho, ili na wao waweze kufaidika na huduma hii ya umeme?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu ni kuwasambazia wananchi wote huduma hii kama nilivyoeleza hapo awali. Kwa

hivyo, hali ya fedha itakaporuhusu basi na kijiji hicho tutakiwekea *transformer* na wananchi hao watafaidika na huduma hiyo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ambayo ametupa Mhe. Naibu Waziri katika kujibu swali mama. Lakini inaonekana kwamba hivi sasa *transformer* maeneo mengi yamezidiwa na umeme ambayo inapelekea kutoa umeme mdogo. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani kuwaondoshea usumbufu wananchi wa Zanzibar? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza tushukuru kwamba wananchi wengi siku hizi wanafahamu umuhimu wa kutumia umeme, na kwa sababu hiyo hata zile *transformer* ambazo zimewekwa katika maeneo mbali mbali zinazidiwa, kwa sababu wananchi wengi wanatumia umeme.

Kutokana na hali hiyo, tumeanzisha mradi wa kubadilisha miundombinu ya umeme, ili kuondoa matatizo haya kwamba *transformer* zimezidiwa na tuweke na nyaya zinazoweza kuchukua uzito wa umeme huo ambao wananchi wanautaka, kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wananchi wanaoishi katika vijiji vingi sana hawana umeme na huenda wizarani kwa sababu ya kuomba umeme, kwa kweli nashukuru hufanyiwa makisio na kila kitu, lakini baadaye hutakiwa wagharamie wao wenyewe.

Je, ni kwa sababu wizara hii safari hii imeshashindwa kusambaza umeme vijijini mpaka wananchi wakalazimishwa wajihudumie wenyewe, wakati gharama za umeme ni kubwa sana, hivi kwa nini haiendelei na mpango wa zamani wa kuwapelekea wananchi umeme wakati wananchi wanalipia umeme ule?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, mwananchi yeyote yule ambaye anayetaka kuunganishiwa umeme baada ya kufanya malipo ya mwanzo hapo shirikani, basi nafikiri Shirika halimlazimishi kulipa malipo mengine ya kuunganishiwa umeme huo.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kijiji ambacho kinachotaka umeme kabla ya shirika kusambaza umeme huo na wakataka kijiji hicho umeme kwa muda ambao wanaoutaka wao, basi shirika hushirikiana na wananchi kwa kuwapelekea huduma hiyo kwa mujibu wa hali ya wakati ule inavyoruhusu.

Kwa mfano, ikiwa fedha zipo basi kijiji hicho hushughulikiwa kwa muda ambao unaotakiwa umeme huo na kama hakuna fedha, basi huwa tunasema, kama hivyo kwamba wananchi wastahamili na wasubiri na baadaye tutawapelekea umeme huo, kwa sababu lengo la serikali kama nilivyoeleza kuwa ni kusambaza umeme vijiji vyote ambavyo huduma hiyo bado haijafika. *(Makofi)*

Nam. 40

Madiko (Bandari za Wavuvi)

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-
Kumekuwa na mazingira yasiyoridhisha katika Madiko (Bandari za Wavuvi), kwani wavuvi, wachuuzi na hata walaji wa samaki mmoja mmoja, hukosa pahala pa kujificha, ama kwa jua au mvua. Kwa kuwa wakuu wa madiko wanajitahidi kukusanya mapato kutoka kwa wavuvi pamoja na wachuuzi katika madiko tofauti.

Je, makusanyo hayo huenda wapi na hufanya kazi gani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba wakuu wa madiko hawakusanyi mapato kutoka kwa wavuvi wala wachuuzi. Madiko ambayo yanakusanya mapato ni mipango yao wenyewe wavuvi juu ya maendeleo ya kijiji chao na wala hayana uhusiano na wakuu wa diko.

Kuhusu suala la sehemu ya hifadhi wizara yangu kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imejenga.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, simsikii vizuri Mhe. Waziri wakati anapojibu, isipokuwa nasikia maelezo au mikutano mingine ambayo Mhe. Hija Hassan Hija anaendeleza.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kuhusu suala la sehemu ya hifadhi wizara yangu kupitia Idara ya Maendelo na Uvuvi inajenga madiko au kwa maana nyengine masoko sehemu mbali mbali kadri ya uwezo unaporuhusu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa katika madiko mengi ambayo wavuvi hupiga kambi kwa maana ya dago hali ya usafi katika madiko hayo huwa hairidhishi, jambo linalopelekea samaki kunadiwa na hatimaye kuuzwa katika mazingira ya hatari.

Je, ni lini wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Afya itakwenda katika maeneo haya ya madiko, kwa ajili ya kutoa taaluma kwa wale wachuuzi pamoja na wavuvi, ili samaki waweze kunadishwa na waweze kuuzwa katika mazingira salama?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi kazi yetu kubwa ni kujenga masoko, ambayo ndiyo yanaitwa madiko na tumejenga sehemu nyingi.

Lakini suala la usafi nafikiri ni jukumu zaidi la wale wavuvi wenyewe, kwa sababu soko ni lao. Kwa hivyo, nafikiri zile fedha zinazokusanywa na kuwa wale wanaokusanya fedha pale sio maofisi, isipokuwa ni Halmashauri kwa baadhi ya madiko au masoko. Kutokana na hali hiyo, naomba kuwashauri wavuvi kwa kushirikiana na Halmashauri, wao sasa ndio washughulikie suala la usafi wa madiko hayo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo, hili ni jambo jema. Lakini kumekuwa na wimbi la kuwachomea nyavu zao wavuvi wadogo wadogo, je huku ni kuwaendeleza au kuwaangamiza? *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kweli wizara inapofanya hayo si kwa maana ya kukomoa au kuangamiza, isipokuwa inakuwa ni wale ambao wamevunja zile taratibu zetu za uhifadhi wa mazingira ya baharini au wale wanaotumia mitego ambayo kwa kweli hairuhusiwi. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba suala la usafi ni la wavuvi wenyewe. Je, Mhe. Waziri katika kuwaendeleza wananchi pamoja na kujenga masoko, basi Malindi pale ni Soko Kuu la uuzaji wa samaki kwa upande wa Zanzibar. Kwa kweli Mhe. Spika Malindi pako katika hali mbaya sana, yaani ni pachafu sana, pamoja na kwamba wizara yake anasema kama siyo inayohusika na usafi.

Je, wizara yake kwa sababu yeye ndiye muhusika mkuu, wavuvi kwa kushirikiana na Manispaa, hivi ni lini watakwenda kujenga vikuta japo si soko, lakini japo vikuta vya kuuzia samaki, ili kuepuka hatari iliopo pale Malindi, kwa sababu ndio macho ya Soko Kuu la Zanzibar, na kwa kweli hali ni mbaya sana, lini watapashughulikia pahala pale?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kweli ni suala zuri na hata mimi naiona hiyo hali ambayo hairidhishi. Lakini kwa sababu si suala la wizara moja inabidi tushirikiane na taasisi nyengine.

Kwa hivyo, nitakaa na taasisi nyengine husika, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sehemu hiyo inakuwa nadhifu kiasi ya kwamba mteja awe hana wasi wasi wa kununua samaki au mtu mwengine yeyote. Kwa kweli hali hairidhishi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, hivyo basi tutakaa na taasisi nyengine, ili kuhakikisha kwamba soko hilo linakuwa katika hali inayokubalika. *(Makofi)*

Nam. 116

Mbegu ya *NERICA* katika Mapinduzi ya Kilimo

Mhe. Abdi Mossi Kombo – Aliuliza:-

Katika miezi michache Rais wa Zanzibar alizindua mbegu ya mpunga iitwayo *NERICA*. Mbegu hiyo inasemekana inaota mpaka sehemu za maweni, ili kukuza kilimo chetu cha Zanzibar na kuweka Mapinduzi ya Kilimo.
Je, ni lini serikali itawapelekea wananchi wanaoishi maweni mbegu hiyo?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 116 kama ifuatavyo:-

Ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amezindua mbegu mpya ya mpunga aina ya *NERICA*. Mara tu baada ya uzinduzi huo Wizara ya Kilimo na Maliasili ilichukua juhudi ya kuizalisha mbegu hiyo ili kuwapatia wakulima kwa ajili ya kupanda katika maeneo ya juu ya kiwemo ya maweni.

Mhe. Spika, kwa msimu huu wa mwaka 2011/2012 wizara imefanikiwa kuzalisha tani 21 za mbegu ya *NERICA* na kuizambaza kwa wakulima, kwa ajili ya kupandwa katika maeneo ya juu ya kiwemo ya maweni kwa wilaya zote za Unguja na Pemba. Aidha wizara imeanzisha Mashamba ya Maonesho katika shehia 230 za Unguja na Pemba, ili kutoa mafunzo kwa wakulima na kuongeza uzalishaji wa mbegu ya *NERICA*.

Mhe. Spika, wizara imepanga kuzalisha mbegu nyingi zaidi kwa msimu ujao, ili iweze kuigawa kwa wananchi na kuharakisha kuenea kwa mbegu hii kwa maeneo ya juu ambapo imeonekana kustawi.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ilivyokuwa kilimo cha mpunga hivi sasa ndicho kinachotiliwa nguvu sana Zanzibar na mbegu mpya hii iliyoletwa Zanzibar ipelekwe mpaka kwenye ukulima wa maweni. Je, Wizara ya Kilimo na Maliasili imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi ambao bado hawajaitambua mbegu hii jinsi ya kuipanda?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeanzisha vishamba vidogo vidogo karibu 230 kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, mara tu wizara ilipopata mbegu hii iliwapa jamaa kwa ajili ya kuizalisha karibu tani 21 za mbegu ya *NERICA* na kuisambaza kwa wakulima wote, ili ipandwe kwa maeneo ya juu yakiwemo ya maweni kwa wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza na hapo hapo kumpongeza waziri kwa kuona kuwa tumezalisha tani 21 za mbegu hiyo. Mhe. Spika, hii ni mbegu mpya na imeshasambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba ili ieneze kilimo cha mpunga.
Je, wizara imefanya utafiti gani katika kuiendeleza mbegu hii na mazingira yake na kuona kuwa itakuwa endelevu ili isije ikatokezea kama tulivyoingia katika mifugo kwa kufanya *cross grading* na tokea miaka ya 80 mpaka leo bado tuna upungufu wa wanyama katika Zanzibar hii. Kwa sababu tu hatukufanya utafiti endelevu, je mbegu hii imefanyiwa utafiti endelevu. Hilo ni moja.

Kwa sababu safari hii wananchi takriban wote waliolima mpunga wamepata hasara mpunga wao haukuwa ni pamoja na mbegu hii kuwa ilipandwa haikuzalisha vizuri?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, napenda nimtoe wasiwasi aliokuwanao kwamba utafiti wa kina kabisa umechukuliwa na hapo hapo kuhakikisha katika shehia zote 230 za Unguja na Pemba kwamba wapate nafasi ya kutosha ya kuiangalia na wizara pia bado inaendelea pamoja na kuzalisha tani 21 na kuzigawa hizi mbegu, lakini baadhi yake bado inafanyiwa utafiti na kwa kadiri ikiwa matokeo yake yatatokea itakuwa serikali iko tayari kuweza kujibadilisha. Wizara pia inaendelea kufuatilia uzuri wa mbegu hizi.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini nimuulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Salim Abdalla amelizungumzia suala la mpunga kwa upande wa Pemba kwamba safari hii kwa kweli wakulima wa Pemba hawana tija hata kidogo mipunga yote imedumaa. Je, Mhe. Waziri maafisa wake walimletea taarifa hizi, kwamba Pemba nzima wakulima wa mpunga kwa kweli wanasikitika.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ukweli sikungojea ripoti bali mimi mwenyewe niliyatembelea mashamba mawili matatu pamoja na Mhe. Rais na pia tunaendelea kuyafanyia utafiti. Lakini kwa ukweli ni kweli kwamba baadhi ya sehemu hali ya mavuno ya mpunga hayakuwa mazuri.

Nam. 189

Vyuo Vikuu vya Zanzibar Kujitoa katika Mfumo wa Udahili Kitaifa

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa Vyuo Vikuu vya Zanzibar vimejitoa katika mfumo wa udahili kitaifa (*Central Admission System CAS)* ndio sababu ya kuwakosesha wanafunzi wa Zanzibar kupata mikopo ya elimu ya juu ya taifa.

(a) Je, kuna ulazima wowote wa kujiunga katika udahili huo.

(b) Je, serikali haioni kuwa kujitoa kwake huko kumewakosesha wanafunzi wengi kupata fursa ya mikopo na kuendelea na elimu ya juu zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 189 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mfumo wa udahili wa wanafunzi kwa kupitia *Central Admission System* ni moja wapo ya utaratibu uliowekwa na Tume ya Vyuo Vikuu vya Tanzania katika Udahili wa wanafunzi wanaotaka kujiunga na taasisi ya elimu ya juu. Utaratibu huu ni wa hiari na ndio maana baadhi ya Vyuo Vikuu vya Tanzania havishiriki katika udahili kupitia *CAS*. Kwa upande wa Zanzibar ni Chuo Kikuu tu cha Taifa cha Zanzibar, *SUZA* ndicho kilichowahi kujiunga na mfumo huu ambapo mwanzoni na baadae kujitoa. Chuo Kikuu cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Ualimu cha Chukwani havijawahi kujiunga na mfumo huu na wanafunzi wake wamekuwa wakipata mikopo ya elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda kutofautiana na Mhe. Mjumbe kuwa wanafunzi wa Zanzibar wanakosa mikopo ya elimu ya juu kutokana na kujitoa katika mfumo wa udahili wa *CAS* kwa vile ni *SUZA* tu ndio chuo kilichojaribu kujiunga katika mfumo huu. Suala la utoaji wa mikopo halina uhusiano na mfumo wa udahili unaofuatwa na vyuo na ndio maana baadhi ya vyuo vya Zanzibar na vya Tanzania Bara vikaamua kutojiunga na utaratibu huu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Uteuzi wa wanafunzi unafanyika baada ya wanafunzi kufanyiwa udahili ama kupitia *CAS* au aina nyengine ya udahili uliokubalika.

(b) Suala la wanafunzi kupata mikopo ya kusoma taasisi za elimu ya juu halina uhusiano na Chuo Kikuu kujiunga au kutokujiunga na udahili kupitia *CAS*. Masharti ya wanafunzi kuomba mikopo inazingatia vigezo vifuatavyo:-

i. Muombaji awe Mtanzania
ii. Awe ameomba mikopo kwa njia ya mtandao
iii. Awe amekubali kujiunga na chuo kilichosajiliwa kwa masomo ya shahada na stashahada ya juu kwa njia ya udahili wa *CAS* au njia nyengine iliyokubwaliwa.
iv. Awe ni mwombani ambaye hana udhamini kupitia chuo au shirika jengine
v. Awe ni mwanafunzi aliyefaulu masomo yake na hivi anaendelea na mwaka unaofuata wa masomo
vi. Awe ni muombaji kutoka taasisi ya mafunzo stad, mafunzo ya amali au aliyemaliza daraja la sita
vii. Awe ni muombaji aliyekubaliwa kujiunga na vyuo mafunzo ya sayansi ya afya, ualimu na sayansi na hesabati.

Kipau mbele katika utoaji wa mikopo kinatolewa katika fani za ualimu wa sayansi na hesabati, udaktari, ufamasia, uhandisi, uchumi na kilimo. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri yanayotia afya kwa wanafunzi wetu naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa umekiri katika swali lako mama kuwa vyuo vyote vya Zanzibar havimo katika *CAS*, lakini *CAS* ndio inayopeleka majina kwenye Bodi ya Mikopo na vyuo vya Zanzibar udahili wenyewe kwa kupata baraka za *TCU* na kupeleka majina yao aidha wamechelewa au wanapeleka mwishoni na kusababisha wanafunzi wengi kukosa mikopo.

Je, wizara yako imejipanga vipi sasa kuweza kuwasaidia wanafunzi wa Zanzibar kuondosha usumbufu wa mara kwa mara unaopatikana.

Lakini swali la pili *COSTEC* ni taasisi inayowasaidia wanafunzi wa Tanzania katika tafiti mbali mbali, ni wanafunzi wangapi wamefaidika na udhamini wa *COSTEC* mpaka hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nimezungumza katika swali mama naomba Baraza lako lifahamu kuwa suala la mikopo na suala la *CAS* ni vitu viwili tofauti. Lakini wizara imejipanga vipi ili kuhakikisha kama wanafunzi wetu wanaoomba kupitia Bodi ya Mikopo ya Bara wanapata mikopo hii.

Mhe. Spika, kwanza wizara tumejipanga kuhakikisha kuwa hii Bodi yetu ya Mikopo ya Zanzibar basi wanafunzi wetu wakiomba wanapata mikopo hiyo. Kwa sababu kwanza tulikuwa bajeti tunayoipata ni ndogo lakini hivi sasa bajeti yetu ni kubwa. Kwa hivyo kwanza tunawaomba wanafunzi wetu waombe katika bodi yetu ya ndani mikopo kabla ya kwenda Bara. Kwa sababu tutakuwa tuna uwezo wa kuweza kuwasaidia, Bara ni bahati nasibu haidhuru ni haki yetu kupata.

Lakini la pili tumezungumza na wenzetu ambao wamo katika kamati kuhakikisha kwamba wanalizungumza suala hili wakiwemo katika vikao vyao kwa nguvu zao zote, kuwa kuna tatizo la wanafunzi wetu kupata mikopo katika bodi ya Bara hivyo wanahakikisha kuwa wanafunzi wetu wanapatiwa hii mikopo.

Kama haitoshi Mhe. Spika, suala hili kama wizara na sisi tumeliona mara ya mwisho ambayo tumekutana na waziri wa Bara tulizungumza kwamba kuna malalamiko ya wanfaunzi wetu kukosa udhamini katika Bodi ya Mikopo ya Bara. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akasema yeye hakuwa na uhakika na hilo lakini atalifuatilia na sio kama atalifuatilia tu, bali atahakikisha kama ni kweli wanafunzi wetu hawapati mikopo hiyo basi atazungumza na bodi kuhakikisha kwamba wanafanya haki sawa kwa wote.

Suala la mwisho kuhusu *COSTEC*. Mhe. Spika, nafahamu taasisi hii kwamba inasaidia si wanafunzi tu, lakini hata vyuo vikuu wanapohitaji kufanya utafiti basi wanatumia taasisi hii. Bahati nzuri sana Mhe. Spika, hawa walikuwa hawana tawi kwa Zanzibar, walikuwa wanafanya kazi zao kwa Bara, lakini hivi karibuni tu *COSTEC* wamefungua tawi lao Tunguu na wamefanya jitihada ya kusudi kuhakikisha kwamba wanakutana na wizara na wanazungumza zile fursa ambazo wanaweza wakazipata wanafunzi wetu lakini vile vile wamepitia vyuo vyote vya Zanzibar kueleza kama *COSTEC* ipo na wako tayari kuwasaidia wanafunzi wetu hao vyuo vyetu kuweza kufanya utafiti.

Sasa ni kiasi gani wanafunzi wetu wamefaidika na ufadhili wa *COSTEC*. Mpaka hivi sasa Mhe. Spika, sijawa na takwimu sahihi ya kujua kwamba ni wanafunzi wangapi ambao wamepata ufadhili kutoka katika taasisi hii, lakini namuahidi Mhe. Mwakilishi kwa hivi sasa wapo Zanzibar, Tunguu tutafuatilia tuhakikishe kama ni wanafunzi wangapi ambao wamepata udahili na pia kuhamasisha wanafunzi wetu ambao wako vyuo vikuu wakitaka kufanya tafiti zao basi watumie taasisi hii. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya kina juu ya suala hili na naomba nimuulize swali moja tu la nyongeza. Mhe. Spika, Elimu ya Juu ni suala la Muungano hadi hivi sasa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano iliyopo na linapatikana katika nyongeza ya kwanza ya katiba hiyo. Sasa kwa kuwa suala hili ni la Muungano na kwa kuwa Zanzibar ilipaswa kufaidika na fursa zote zinazohusu elimu ya juu katika suala hili, na kwa kuwa mara kadhaa majibu ya Mhe. Naibu Waziri yamethibitisha kwamba hakupatikani mashirikiano wanafunzi wa Zanzibar ama kutopata fursa hizi na vile vile kukataa Serikali ya

Muungano kutoa gawio la Mfuko huu likaja Zanzibar ili Zanzibar yenyewe iweze kushughulikia wanafunzi wake. Serikali haioni sasa wakati umefika wa kutoa tamko rasmi kwamba hakuna haja sasa hivi ya kuendelea na Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ile sentensi ya mwisho sikumfahamu Mhe. Mjumbe naomba airudie.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwa sababu ya mwanzo yote kayaelewa sentensi yangu ya mwisho inasema, kutokana na sababu nilizozitaja je, haoni kama kuna haja kupitia Baraza hili hii leo Waziri akatwambia kwamba hakuna haja tena ya suala hili kubakia kuwa la Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, yote ambayo ameyazungumza Mhe. Ismail Jussa nia ya swali lake ni hii sentensi ya mwisho kuwa wizara inaonaje ikatoa kauli ya suala hili. Mhe. Spika, wizara kwa hivi sasa haioni kuwa kuna haja ya kutoa tamko hili kwa sababu ni karibuni tu Zanzibar tutafaidika na kutoa maoni ya Katiba Mpya. Sasa namuomba Mheshimiwa kama suala hili tunaliona ni tatizo kwa Zanzibar suala la Elimu ya Juu basi ni fursa pekee, ni fursa adhimu kwa Wazanzibari kulizungumza kwa upana ili kuhakikisha wanakipata kile ambacho wanaona kina faida na wao kwa maslahi ya nchi yao.

Nam. 149
Ukosefu wa Daktari katika Nyumba ya
Hospitali ya Ukongoroni

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga kituo cha afya na nyumba ya kulala daktari katika kijiji cha Ukongoroni, ili kuwawezesha wananchi wa kijiji hicho kupata huduma hiyo kwa wepesi zaidi. Hata hivyo, kituo hicho kinafanya kazi katika nyakati za mchana tu kwa kuwa hakuna daktari anayeishi katika nyumba hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kutokupatikana kwa daktari wa kuishi katika nyumba hiyo kunawakosesha haki ya kupata matibabu wanakijiji hao pale inapohitajika hasa katika nyakati za usiku.
(b) Je, unaweza kutuambia ni sababu zipi zilizofanya kukosekane kwa daktari wa kuishi katika nyumba hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Bi Panya Viti Maalum Wanawake swali lake Nam. 149 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kituo cha Ukongoroni karibuni tu kilikuwa na daktari mstaafu wa Jeshi ambaye aliajiriwa kwa mkataba na alikuwa akiishi katika nyumba hiyo. Lakini daktari huyo amemaliza mkataba wake na kuondoka. Na mkunga msaidizi mmoja anaumwa na mwengine amejifungua, lakini amesharudi kazini na anaishi Bwejuu alikoolewa.

(c) Wizara ya Afya kutokana na upungufu ulionao bado haijapata daktari wa kuchukua nafasi hiyo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa lengo kuu la serikali ni kuwaondoshea usumbufu wananchi wake na ndio maana kila kilipojengwa kituo ikajengwa na nyumba ya daktari. Je, Mhe. Naibu Waziri atafanya juhudi gani ili wananchi hawa waweze kupata huduma ya kupata daktari huyu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nia ya Wizara ya Afya ni kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata huduma, lakini uwezo wa Wizara ya Afya wa madaktari ambao wanapaswa kuwekwa katika kila kituo haujaridhisha kwa sababu tunatoa wachache, wengi wanaondoka na hatuna chuo chengine ambacho kinatoa madaktari. Lakini hata hivyo, pale ambapo wale wachache tunaowapata huwa tunaangalia hasa zile sehemu ambazo tunahisi kwamba hizi ni ngumu na ni lazima zipatiwe huduma ya haraka ukilinganisha na nyengine ikiwemo Ukongoroni, ndio maana walipopatikana wastaafu walipelekwa Ukongoroni. Lakini wastaafu wana muda wao na wanaondoka na wengine huwa hawajaja bado.

Lakini nataka nimuahidi kwamba tutakapompata yoyote mwengine tutahakikisha tunampeleka huko. Kwa sababu tunajua kwamba Ukongoroni ni sehemu moja ambayo inahitaji mtu wa karibu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Selem Mfenesini tumejengewa nyumba ya daktari na daktari yupo, lakini ukienda usiku na matatizo ya maradhi daktari huamka akakwambia nenda Mnazi Mmoja. Je, dhamira iliyokusudiwa inapatikana kwa majibu kama haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, madhumuni ya kujenga vituo vya afya na nyumba za madaktari ni kuwafikishia huduma wananchi hasa pale wanapozihitaji. Pale ambapo pana nyumba ya daktari na daktari yupo akiendewa usiku anatakiwa aamke amsaidie mgonjwa. Sasa kwa Selem suala hilo sikuwa nimepata malalamiko lakini tutalifuatilia kwa sababu hana sababu ya kuwa awepo pale halafu akatae kumsaidia mgonjwa, anachopaswa kukifanya amuangalie mgonjwa akiona limemshinda lililomleta pale aelekeze mgonjwa aende katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tutalifuatilia na kutoa maelekezo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa lengo la serikali yetu ya *GNU* ni kupunguza vifo vya mama na mtoto na kwa kuwa Ukongoroni kuna akinamama wengi wanaohitaji huduma hii. Je, ni lini serikali itaanzisha *mobile clinics* kwa sababu kuna madaktari wako *Mnazi Mmoja Hospital* kwa nini wasitoe hii huduma ya *mobile clinics* ili kutoa huduma kwa sababu madaktari hawatoshi. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa nyumba hii ilijengwa kwa fedha za walipakodi na mpaka sasa hivi haikai daktari. Je, hayo si matumizi mabaya ya fedha za walipakodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba nimsahihishe mimi ni Naibu Waziri sio Waziri. Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe anasema kwamba Ukongoroni ni sehemu ambayo ina matatizo ya kufikika, tutaangalia utaratibu wa *ZOP* ambao unakwenda kwenye vijiji tuhakikishe kwamba nako wanafika kama una hakika hawafiki kwa sababu *ZOP* wanakwenda sehemu zote. Lakini nitajaribu kuangalia na *ZOP* nione kama hawafiki huko niwaambie wafanye utaratibu ili waweze kufika kuwapelekea huduma hizo unazozisema.

Lakini suala la nyumba, nyumba inakuwa inatumika panapokuwa na mtu kama mtu hayupo nyumba bado itabaki tupu. Waliopo mmoja ana nyumba yake, mwengine kaolewa Bwejuu hawezi kumuacha mumewe akaja akakaa kwenye nyumba ile. Kwa hivyo, tutakapopata daktari ambaye ataweza kukaa pale tutamuweka kwenye nyumba ile, lakini kwa sasa hivi itabidi ibaki tupu kwa sababu daktari wa kumuweka hatujampata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha - Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uzima wa afya njema na kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli yetu hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe mwelekeo mwema na atuzidishie hekima, busara, uadilifu na mashirikiano ili tutekeleze majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba sasa nitumie fursa hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein kwa jinsi anavyosimamia utekelezaji wa mjukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hekima na umakini mkubwa.

Aidha, naomba nimpongeze kwa namna ya pekee jinsi anavyohakikisha kuwa amani, maelewano, utulivu na umoja katika nchi yetu unalindwa na kudumishwa na utaratibu wa kutii sheria unaimarishwa. Mhe. Dr. Shein akiwa Rais

wa Kwanza wa Zanzibar kuongoza Serikali ya Mapinduzi yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa amekuwa kinara wa utawala bora na mfano wa kuigwa duniani kote. Nasaha na miongozo yake ya mara kwa mara anayotupatia imetuwezesha kufanikisha na kutekeleza majukumu ya ofisi yetu ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa umahiri wao katika kusimamia majukumu waliyopewa. Aidha, nawashukuru kwa miongozo na ushauri wanaotupatia mara kwa mara juu ya utekelezaji wa majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa nafasi yako ya Spika kwa jinsi unavyosimamia majukumu na utendaji wa Baraza hili tukufu na kukiwekea heshima chombo hiki kikubwa ambacho ni muhimu kati ya mihimili mikuu ya nchi yetu.
Mhe. Spika. baada ya pongezi zetu kwa viongozi hao wakuu wa Kitaifa, sasa napenda kuchukua fursa hii kuipongeza na kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini na Makamu wake Mheshimiwa Panya Ali Abdalla Mwakilishi wa Viti Maalum - Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja na wajumbe wote wa kamati hii kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia katika shughuli mbali mbali hususan wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 hatua ambayo, imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bajeti hii katika Baraza lako Tukufu. Vile vile nampongeza Mhe. Mohammedraza Hassanali kwa ushindi wa kishindo alioupata katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Uzini uliomuwezesha kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na hatimae kuteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati hii.

Mhe. Spika. mwaka jana Kamati hii ilipata pigo kutokana na kumpoteza mjumbe wake mahiri Marehemu Mussa Khamis Silima ambaye alifariki akiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kitaifa. Naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi – Amin.

MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS - UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.

Mhe. Spika. Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jukumu la kusimamia utendaji wa Watumishi wa Umma ili waweze kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu cha ufanisi na kuimarisha Utawala Bora nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, Ofisi ina wajibu wa kusimamia, kudhibiti, kuratibu na kutathmini utekelezaji na uongozaji wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuzingatia misingi ya Dira ya Maendeleo ya 2020, mipango ya kitaifa kama vile MKUZA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 - 2015 na kuzingatia mikataba na makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

Mhe. Spika. ili kufanikisha majukumu hayo, Ofisi itafuata kikamilifu miongozo ya Katiba, itakayo simamia vyema Sera, Sheria za nchi, Kanuni zake na Miongozo na matoleo mbalimbali pamoja na kufanya mapitio ya Kiutumishi na kuandaa Sera mpya na miswada ya Sheria itakayoweka mfumo bora wa Utumishi wa Umma na kukuza uwajibikaji kwa wananchi. Aidha, Ofisi itaandaa mikakati ya kuzuia rushwa, kusimamia maadili ya Viongozi, kuweka utaratibu wa mawasiliano ya kiofisi kwa kutumia tekinolojia mpya ya mawasilano na mfumo wa elekroniki, kuratibu shughuli za haki za binaadamu na kusikiliza malalamiko ya wananchi katika maeneo mbali mbali ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika. maelezo kamili ya majukumu ya kila Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii yamefafanuliwa katika taarifa za Idara/Taasisi husika.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS - UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

Mhe. Spika**.** Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatekeleza majukumu yake kupitia Idara nane na taasisi nne ambazo ni;

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
2. Idara ya Utumishi na Uendeshaji
3. Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu
4. Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu

5. Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi
6. Idara ya Utawala Bora
7. Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa
8. Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Pemba
9. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
10. Kamisheni ya Utumishi wa Umma
11. Tume ya Utumishi Serikalini
12. Chuo cha Utawala wa Umma.

Aidha Ofisi inategemea kuwa na Taasisi mbili mpya zifuatazo:-

(1) Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi; na
(2) Taasisi ya Mawasiliano ya Elektroniki na Menejimenti ya Taarifa (e–Government and Central Database Management).

Mhe. Spika. baada ya pongezi za Ofisi yangu kwa Viongozi Wakuu, Wananchi na kuelezea majukumu na muundo wa Ofisi, sasa kwa ruhusa yako naomba nifanye mapitio ya utekelezaji wa shughuli za mwaka 2011/2012, maelezo ya Mpango Kazi wa mwaka 2012/2013 na maombi ya fedha za utekelezaji wa mpango huo kwa kila Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - Utumishi Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

UTEKEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2011/2012 NA MUELEKEO WA MALENGO KWA MWAKA 2012/2013 KWA KILA IDARA NA TAASISI.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:
Majukumu ya Idara:

Mhe. Spika. Idara hii ina jukumu la kutoa huduma na utaalamu wa uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na tathmini ya programu na miradi ya Ofisi ya Rais - Utumishi Utumishi wa Umma na Utawala Bora , kutayarisha na kuzifanyia mapitio Sera na kufanya tafiti. Vile vile, Idara inajukumu la kusimamia Mageuzi ya Utumishi wa Umma - Zanzibar na kuandaa mbinu za kutafuta rasilimali na misaada mbalimbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika. kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilipanga kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu na Miradi inayosimamiwa na Ofisi, kufanya mapitio ya Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati - MTEF na tathmini ya Mpango kazi wa Mwaka, kukamilisha Sera ya Usafiri ya Watumishi wa Umma, kutayarisha Sera ya mawasiliano ya elektroniki (e-Government) na kufanya utafiti wa namna Watumishi wa Umma watakavyofaidika na huduma za Bima ya Afya. Vile vile, Idara ilipanga kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa kwa njia ya kompyuta – (Information Management System). Ili kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS. 307,753,900 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo TZS. 234,753,900 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na TZS.73,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika**.** Idara imeandaa Mpango wa Matumizi wa muda wa kati - MTEF (2012-2015), imeratibu na kufuatilia Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma. Vile vile katika hatua za utafutaji wa rasilimali fedha, Miradi minne mipya imewasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Zanzibar na kuingizwa katika Mpango wa utekelezaji wa MKUZA, Miradi hiyo ni; “Digitalization of Zanzibar Archives”, “Enhancing Democracy, Good Governnance and Human Rights Through Capacity Building”, “Comprehensive Capacity Building for Government Institutions” na “Anti-Corruption Initiatives”.

Mhe. Spika. kwa upande wa uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar, ‘’Concept paper’’ yenye kuonesha taswira nzima na hatua zinazohitajika kufuatwa katika uanzishwaji wa Bima ya Afya imeandaliwa kwa mashirikiano kati ya

Kamati ya Wataalamu wa Ndani, Wataalamu wa DANIDA na Shirika la Afya Duniani. Aidha, utafiti wa utayari wa wadau wote wa Bima ya Afya (Watoa huduma, Waajiri na Waajiriwa) umefanyika.

Mhe. Spika. katika kuimarisha mawasiliwano na wadau mbali mbali wa sekta ya utumishi na wananchi kwa jumla, Tovuti ya Wizara imezinduliwa rasmi, Tovuti hiyo ni www.utumishi-utawalabora.com na inatoa fursa za kuwasiliana na kupata huduma za ofisi yetu kama vile; Sera, Sheria, Kanuni, machapisho, matangazo na nafasi za ajira, kuwasilisha malalamiko ya Watumishi na Wananchi kwa ujumla kwa njia ya wepesi zaidi.

Mhe. Spika. hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetumia jumla ya TZS.141,883,545 kwa kutekeleza kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika. kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara imepanga kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kuandaa Mipango ya Ofisi, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ikiwemo programu na miradi. Kutayarisha programu na miradi mipya, kutayarisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya usafiri na Sera ya mawasiliano ya elektroniki na kusimamia uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar.

Mhe. Spika. ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 300,008,000. Kati ya fedha hizo, TZS 165,008,000 ni kwa utekelezaji wa kazi za kawaida na TZS 135,000,000 ni kwa kazi za Maendeleo. Pia tunaomba idhini ya ukusanyaji wa mapato ya jumla ya TZS 1,440,OOO,OOO.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Majukumu ya Idara:

Mhe. Spika**.** Idara hii ina jukumu la kutoa huduma za utumishi na uendeshaji katika Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora , zikiwemo ajira, maendeleo ya watumishi, kupandisha vyeo na kufanya tathmini ya watumishi, kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kuweka kumbukumbu za masuala mbalimbali yanayohusu watumishi. Aidha, Idara inatoa huduma za manunuzi, uhifadhi wa vifaa, huduma za uhasibu, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, mapato na matumizi na matayarisho ya ulipaji wa mishahara.

Malengo ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika**.** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ilipanga kuajiri watendaji wa kutosha na wenye sifa kulingana na mahitaji ya Ofisi, kuweka kumbukumbu za kiutumishi kwa watendaji na kufanya tathmini ya utendaji wa kila mtumishi pamoja na kuandaa ripoti ya hali ya Utumishi wa Ofisi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria. Kuendelea kutoa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa vya ndani ya Ofisi, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wa Ofisi na kupima ufanisi wa utendaji kazi na utekelezaji wa mageuzi ya kiutumishi. Ili kutekeleza malengo hayo, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS. 1,012,416,315. Kati ya hizo TZS. 695,604,315 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na TZS. 316,812,000 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya Mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika. katika kutekeleza malengo ya mwaka 2011/2012, Idara imechapisha na kusambaza vipeperushi vya mradi wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma vyenye lengo la kuelimisha na kuhamasisha mabadiliko katika Utumishi wa Umma, imetoa huduma za uendeshaji na utawala kwa Ofisi. Vile vile Idara imeratibu na kutayarisha mikutano ya ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais - Utumishi Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma SMT Katika uimarishaji wa nguvu kazi ya Ofisi, Watumishi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali. Aidha, Watumishi kumi wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nchi za China, India na Denmark.

Mhe. Spika. hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imetumia jumla ya TZS. 517,543,944 kwa kutekeleza kazi za kawaida na TZS. 113,599,275 kwa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika. katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imepanga kuhakikisha kuwa, Ofisi inaweka mazingira bora na ustawi mzuri wa Watumishi, kuratibu na kuwezesha kufanya mikutano ya kamati mbalimbali zinazosimamia majukumu ya Ofisi, ikiwemo Kamati ya Uongozi wa Ofisi, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Zabuni na Kamati ya Fedha. Vile vile kuratibu na kutayarisha mikutano ya ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma, Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Rais Utawala Bora SMT, kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Ofisi katika viwango mbali mbali ndani na nje ya nchi, kusimamia ujenzi wa makao makuu ya Ofisi yanayokusudiwa kujengwa katika eneo la Mazizini na kuimarisha kamati maalum inayoshughulikia masuala mtambuka.

Mhe. Spika. ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 953,908,000. Kati ya hizo TZS. 893,908,000 ni kwa kazi za kawaida na TZS 60,000,000 ni kwa kazi za Maendeleo

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU.

Majukumu ya Idara:

Mhe. Spika. majukumu ya Idara hii ni kuratibu mafunzo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi kwa watumishi wote wa umma wa ngazi mbali mbali ambayo hugharamiwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo. Vile vile, Idara inajukumu la kuanzisha na kutoa miongozo na ushauri wa kitaalamu kuhusu maandalizi ya mfumo wa kusimamia mafunzo kwa watumishi wa umma katika Wizara na Taasisi za Serikali. Aidha, Idara inajukumu la kusimamia mikataba kati ya Serikali na waajiriwa wanaokwenda masomoni ili mfanyakazi anaporejea masomoni atumikie kwa muda uliotajwa katika mkataba baada ya kumaliza masomo yake. Jukumu jengine la Idara ni kuandaa na kutunza daftari la taarifa za mafunzo ya watumishi wa umma.

Malengo ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika. kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilipanga kuendelea kuratibu mafunzo kwa Watumishi wa Wizara na Taasisi zote za Umma, kuandaa Sera ya mafunzo, kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa umma, ili Wizara na Taasisi ziweze kuratibu mafunzo kutokana na mahitaji sahihi ya Utumishi wa Umma. Pia ilipanga kuwajengea uwezo Maofisa mafunzo wa Wizara na Taasisi za Umma juu ya uandaaji wa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na Mpango wa Mafunzo. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS. 87,300,445 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya Mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika. Idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, imeanzisha vitengo vya mafunzo katika kila Wizara Unguja na Pemba ili kuratibu masuala ya mafunzo kwa watumishi. Katika kuwaendeleza watumishi wa umma, jumla ya Watumishi 179 wamehudhuria mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi, kati ya hao watumishi saba wamepata mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Stashahada ya juu, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili katika nchi za China, Korea ya Kusini, India na Japan, na watumishi 172 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda wa kati katika nchi za Korea, China, Japan, Singapore, Sweden, India na ESAMI Jumla ya Makatibu Mukhtasi 13 wa Ofisi ya Rais - Utumishi Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake wamepatiwa mafunzo ya Uhazili katika Chuo cha Utawala wa Umma. (kiambatisho namba 1).

Mhe. Spika, katika kuwaendeleza watendaji wakuu wa Serikali Idara kupitia Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma Zanzibar iliendesha mafunzo juu ya changamoto za utekelezaji wa mageuzi katika utumishi wa umma (Reinventing Government: Challenges of Implementing Reform in Public Sector) kwa manaibu makatibu wakuu wote wa SMZ. Aidha, wakurugenzi 11 na Maofisa wadhamini watano wanawake walipatiwa mafunzo juu ya

kuwawezesha wanawake, usawa wa kijinsia na utekelezaji wa muongo wa wanawake 2010-2020 (Women Empowerment, Gender Equality and Implementation of Africa Women Decade). Mafunzo yote hayo yaliendeshwa na wakufunzi kutoka ESAMI kwa muda wa wiki moja huko Dar es salaam. Maofisa tawala saba kutoka Halmashauri za wilaya Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya "Result Based Management" huko Bagamoyo. Katika kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa mpango wa mafunzo, Idara inaandaa Sera ya Mafunzo ambapo Rasimu ya awali imekamilika na hatua inayofuata ni kuiwasilisha kwa wadau ili kupata michango zaidi.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu imetumia jumla ya TZS. 60,105,530 kwa kutekeleza kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika. kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imepanga kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma, kuimarisha uhusianao na mashirikiano na vyuo mbali mbali vya kitaaluma na Washirika wa Maendeleo ili kuimarisha upatikanaji wa fursa za Mafunzo kwa Watumishi wa Umma. Idara pia imepanga kukamilisha Sera ya mafunzo na kuandaa Mpango wa Utekelezaji na kuanzisha mfumo wa uwekaji wa taarifa za Mafunzo ya Watumishi wa Umma.

Mhe. Spika. kwa kupitia programu ya kitaifa ya kujenga uwezo katika taasisi za Serikali, Idara itakamilisha zoezi la tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango mkuu wa mafunzo kwa watumishi wa umma. Idara pia imepanga kutoa mafunzo mafupi ya ndani kwa watumishi wa kada mbali mbali Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi hasa wa ngazi za chini. Aidha, kwa kupitia nchi wafadhili na washirika wa maendeleo, Idara inatarajia kuwapatia watumishi 150 mafunzo ya muda mfupi, wa kati na ya muda mrefu katika nchi za Korea, China, Japan, Singapore, India, Bangkok, Indonesia na Israel.

Mhe. Spika. ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 317,180,000. Kati ya hizo TZS 117,180,000 ni kwa kazi za kawaida na TZS 200,000,000 ni kwa kazi za Maendeleo.

IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU.

Majukumu ya Idara:

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kupanga, kuratibu na kusimamia Mipango ya Rasilimali Watu na kuandaa Mpango wa Urithishaji Uongozi - *"Succession Plan"* katika Wizara na Taasisi za Umma kwa madhumuni ya kukidhi malengo na mahitaji ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, majukumu mengine ya Idara hii ni kuchunguza uwezo uliopo wa Rasilimali Watu *"Human Resource Capacity Assessement"* ili kugundua mahitaji ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma, kuratibu na kusimamia mpango wa miaka mitano wa Rasilimali Watu na mpango wa kila mwaka, kuweka kumbukumbu za watumishi wa Umma *"Human Resource Database"* na kuidhinisha ikama (Norminal Roll) za Watumishi wa Umma.

Malengo ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilipanga kuwapatia mafunzo Maofisa Utumishi wa Mawizara juu ya namna bora ya matayarisho ya ikama, kusimamia Mageuzi ya Serikali za Mitaa - Local Government Reform, kuanzisha Utaratibu na Mbinu za Urithishaji wa kazi, kufuatilia uwezo wa Rasilimali Watu ili kugundua mahitaji halisi ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma. Kukusanya na kuweka kumbukumbu na taarifa za msingi za Watumishi wa Umma na kuziingiza katika Mfumo wa Taarifa za Wafanyakazi kwa njia ya elektroniki – "Human Resource Database." Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa na Baraza lako Tukufu jumla ya TZS. 232,506,513 kati ya hizo TZS. 102,940,713 kwa kazi za kawaida na TZS. 129,565,800 kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, katika jitihada za kuimarisha kumbukumbu za Watumishi wa Umma, Idara imeanzisha Mfumo wa taarifa za Rasilimali Watu kwa njia ya elektroniki (Human Resource Data Base), ambao utasaidia kuweka na kuzitumia taarifa hizo katika masuala ya kiutumishi ikiwemo mahitaji ya watumishi, taaluma zao na kuweka makisio ya wastaafu pamoja na muelekeo wa mafao yao. Idara imeorodhesha vijana 5472 walioomba kazi kwa kuainisha viwango vyao vya elimu na fani walizosomea kwa lengo la kufanya mazingatio ya mipango ya baadae. Aidha, mafunzo ya siku 4 kwa Maafisa utumishi na wasaidizi Maafisa Utumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali juu ya utayarishaji bora wa ikama, umuhimu wa kuwa na taarifa sahihi za Watumishi wa Umma na uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma yametolewa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, vikao vya majadiliano kwa wizara 16 kujadili ikama vilifanyika na jumla ya maombi ya nafasi mpya 6817 za ajira yaliwasilishwa, kati ya maombi hayo, nafasi 3356 ziliidhinishwa na nafasi 2552 zimekubaliwa baada ya kuzingatia uwezo wa Serikali. (kiambatisho namba 2). Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya wafanyakazi 418 wanategemewa kustaafu kazi kwa kufikia Umri wa lazima. Wizara 13 zimefanyiwa uhakiki kwa kuyapitia majalada binafsi (*OPF*) ili kubaini usahihi wa taarifa za watumishi zilizopo. Watumishi 133 walifanyiwa uhamisho katika Wizara za Serikali kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. (Kiambatisho Namba 3). Rasimu ya awali juu ya Muongozo wa Mpango wa Urithishaji Uongozi katika Utumishi wa Umma (*Succession Plan*) umekamilika na hatua inayofuata ni kuiwasilisha kwa wadau Unguja na Pemba ili kupata maoni yao.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya TZS. 61,321,565 zimetumika kwa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara imepanga kufanya mapitio ya ikama ya mwaka 2012/2013 na kuidhinisha ikama ya mwaka 2013/2014, kuendesha mafunzo ya utayarishaji wa ikama, umuhimu wa taarifa sahihi katika "*database*", maadili ya utumishi wa umma kwa Maafisa utumishi na kuandaa mpango wa miaka mitano wa rasilimali watu. Kutayarisha taarifa juu ya hali halisi ya uwezo uliopo wa rasilimali watu na kukamilisha Mpango wa Urithishaji wa Uongozi katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 138,868,000 kwa kazi za kawaida. (kiambatisho namba 8).

IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI.

Majukumu ya Idara

Mhe. Spika, idara ina jukumu la kupitia na kusimamia miundo na mifumo ya Wizara na Taasisi za Umma kwa mujibu wa Sera na Sheria zilizopo ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma. Vile vile, kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuendeleza na kusimamia Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya Wafanyakazi.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilipanga kutayarisha muongozo wa kutengeneza mkataba wa kutoa huduma kwa wananchi (*Client Service Charter*), kuratibu na kushauri ajira za Wageni ndani ya Utumishi wa Umma, kuanzisha na kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi "*Performance Appraisal*" katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, idara pia imepanga kufanya mapitio ya kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mawizara na Taasisi za Umma, kutayarisha Sera ya malipo kwa Watumishi wa Umma, kufanya utafiti juu ya masuala ya Mishahara na Maposho, kutoa mafunzo na kufanya ukaguzi wa wafanyakazi na mishahara (*Staff Inspection and Payroll Audit*) na kupitia miundo ya Utumishi (*Scheme of Services*). Ili kutekeleza malengo hayo kwa mwaka 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS. 549,558,469. Kati ya hizo TZS. 105,311,569 kwa kazi za kawaida na TZS. 444,246,900 kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imekamilisha mapitio ya Miundo ya Utumishi kwa kada zote ili kuwezesha watumishi kuzitambua daraja zao, ngazi za mishahara na utaratibu wa upandishwaji vyeo. Kazi ya ukaguzi wa wafanyakazi na mishahara kwa Wizara zote 16 imekamilika.

Mhe. Spika, Fomu ya Upimaji Utendaji kazi (*Performance Appraisal*), Muongozo wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) na Muongozo wa Majukumu na Upeo wa Utendaji wa Serikali (*Role and Scope of Government Operation*) imetayarishwa na imeshapata maoni ya wadau Unguja na Pemba na hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu ili kupata maoni zaidi. Taasisi zote zimeagizwa kuhakikisha kuwa utaalamu uliokosekana na kusababisha kuajiriwa kwa Wageni unarithiwa na Wataalamu wenyeji.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya TZS. 68,461,396 zimetumika kwa kutekeleza kazi za kawaida na TZS. 52,901,000 kwa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inategemea kufanya matayarisho ya kutengeneza mkataba wa kutoa huduma kwa wananchi, kuratibu na kushauri ajira za Wageni ndani ya Utumishi wa Umma, kuanzisha na kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, vile vile idara imepanga kuimarisha mfumo wa Taarifa za malipo ya Watumishi wa Umma, kuwajengea uwezo watumishi juu ya kutumia mfumo wa Taarifa za malipo ya Watumishi wa Umma, kutengeneza Sera ya malipo ya Watumishi wa Umma. Aidha, Idara imepanga kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma juu ya sheria na kanuni za Utumishi wa Umma na kufanya tathmini ya kazi na viwango (*Job evaluation and grading*), kuandaa mkataba wa huduma kwa mteja na kufanya mapitio ya Majukumu ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa Idara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 438,471,000. Kati ya hizo TZS 150,471,000 ni kwa kazi za kawaida na TZS 288,000,000 ni kwa kazi za Maendeleo.

IDARA YA UTAWALA BORA

Majukumu ya Idara

Mhe. Spika, idara ina jukumu la kujenga na kusimamia utekelezaji wa misingi mbali mbali ya Utawala Bora ikiwa ni pamoja na kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni ili kuhakikisha haki za binaadamu zinalindwa. Vile vile, Idara ina wajibu wa kuhakikisha kuwa maadili ya Viongozi yanazingatiwa, amani na utulivu vinaimarishwa. Jukumu jengine la Idara hii ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili waweze kuelewa haki na wajibu wao kwa Taifa.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilipanga kutekeleza majukumu yake ya kuimarisha Utawala Bora, kutoa elimu ya uraia na mafunzo ya Utawala Bora kwa Watendaji Wakuu wa Utumishi wa Umma. Pia Idara ilipanga kuhamasisha na kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu katika Shehia, Vijiji na Taasisi mbalimbali za Umma, kuandaa kongamano kwa ajili ya kuadhimisha siku ya Haki za Binadamu, kutayarisha na kusambaza ripoti ya mwaka ya Utawala Bora na kutafsiri Muongozo wa Haki za Binaadamu kwa kutumia Nukta Nundu (*Braille*) kwa watu wasioona. Ili kutekeleza malengo hayo, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya TZS.301,607,557. Kati ya hizo TZS.271,607,557 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na TZS. 30,000,000 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Idara imetoa mafunzo kwa Makatibu Wakuu wa Wizara za Serikali na imeendesha mafunzo ya Elimu ya uraia kwa Shehia 6 za Unguja na shehia 6 za Pemba. Pia Idara kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa elimu ya uraia katika wilaya 4 za Unguja. Jumla ya vipindi 30 vya elimu ya uraia vimerushwa hewani na Shirika la Utangazaji Zanzibar. Sambamba na hilo, Idara ilitoa elimu ya uraia kwa Jumuiya ya Watu Wasioona (ZANAB). Jumla ya malalamiko 8 ya wafanyakazi yamepokelewa na kufanyiwa kazi (Kiambatisho namba 4A na 4B).

Mhe. Spika, Sera ya Utawala Bora imetayarishwa kwa lugha ya Kiswahili, Kiiengereza na lugha nyepesi pamoja na kutafsiriwa kwa Nukta Nundu (*Braille*). Sera hiyo pamoja na Muongozo wa Haki za Binaadamu uliotafsiriwa kwa Nukta Nundu vilizinduliwa rasmi tarehe 26 Mei 2012. Katika kutekeleza sera ya Utawala Bora, Kamati ya Kitaifa ya Utawala Bora imeundwa na kuzinduliwa tarehe 17 Januari 2012 na tayari imeshaanza kazi. Wajumbe wa Kamati ni Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti na wajumbe kutoka katika Jumuiya Zisizo za Kiserikali. Miongoni mwa kazi za Kamati ni kutoa ripoti ya mwaka ya Utawala Bora Zanzibar. Ripoti ambayo itaonesha utekelezaji pamoja na changamoto zilizopo juu ya Utawala Bora. Idara pia ilishirikiana na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Wenyewe (*African Peer Review Mechanism - APRM*) katika kuhakiki ripoti ya Utawala Bora ya Tanzania.

Mhe. Spika, katika hatua za kukabiliana na suala zima la rushwa na uhujumu uchumi, Sheria Namba 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ya mwaka 2012 imetayarishwa na kukamilika. Sheria hiyo tayari imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 2 Mei 2012. Idara iliandaa Sheria ya Maadili ya Viongozi na imeshaanza kuchangiwa na wadau mbali mbali kwa upande wa Unguja na Pemba.

Aidha, Wizara iliadhimisha siku ya kupambana na Rushwa duniani, ambapo kazi mbali mbali zilifanyika ikiwa ni pamoja na kutayarisha mabango, maonyesho ya sanaa za maigizo, midahalo ya Wataalamu na wanafunzi wa vyuo vikuu vya Zanzibar pamoja na kutoa makala zenye kutoa ujumbe juu ya kupambana na Rushwa na uhujumu uchumi.

Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Utawala Bora imetumia jumla ya TZS. 139,737,226. Kati ya hizo TZS. 90,554,226 kwa kutekeleza kazi za kawaida na TZS.49,183,000 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, idara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imepanga kutoa mafunzo, kufuatilia na kutathmini juu ya uwazi na uwajibikaji kwa watendaji wa utumishi wa umma, kutayarisha vipindi vya elimu ya uraia na kuvirusha hewani kwa kutumia vikundi vya sanaa na ziara za vijijini. Idara vilevile imepanga kufanya kampeni za ushajihishaji wa Haki za Binaadamu kwa njia ya semina, makongamano, kalenda, mikutano na kutoa vipeperushi kwa wananchi. Aidha, Idara itaadhimisha siku ya Haki za Binaadamu na siku ya Rushwa duniani, itafanya mikutano ya robo mwaka kwa Kamati ya Utawala Bora na kutoa ripoti ya mwaka ya Utawala Bora ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa Idara ya Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 177,548,000 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Majukumu ya Idara

Mhe. Spika, idara ina majukumu ya kuhifadhi Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali kama Urithi wa Taifa, kuhifadhi Nyaraka muhimu za kihistoria na kutoa huduma za utafiti, kutumia mbinu za kitaalamu kwa kuzifanyia matengenezo kumbukumbu zilizo katika hali mbaya, kuendeleza, kusimamia na kuelekeza matumizi bora ya kumbukumbu. Idara pia ina jukumu la kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu ili zipewe umuhimu unaostahili.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilipanga kutayarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka katika Wizara na Taasisi za Serikali, Kuimarisha Masjala kwa kuweka mfumo bora wa utunzaji wa kumbukumbu katika Wizara 5 teule, kutoa mafunzo kuhusu umuhimu wa kumbukumbu, utunzaji na matumizi yake kwa Maofisa kumbukumbu. Aidha, kuendelea kufanya kazi za ukaguzi wa kabla na baada ya Mfumo wa usimamizi wa Kumbukumbu na Nyaraka, kuwajengea uwezo wafanyakazi watano katika fani ya Menejimeti ya kumbukumbu, kati ya hao wawili katika ngazi ya Cheti na watatu katika ngazi ya diploma. Vile vile, kuwapatia ushiriki wafanyakazi katika mikutano ya kitaifa, kimataifa na semina. Idara pia ilipanga kuandaa vikao viwili vya Bodi ya Ushauri wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa pamoja na kuwajengea ustawi wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya ofisi. Ili kutekeleza malengo hayo, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 533,485,609. Kati ya hizo TZS.232,795,309 kwa kazi za kawaida na TZS.300,690,300 kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 idara imezifanyia matengenezo Nyaraka 208 na kuhudumia jumla ya watafiti 202. Maeneo makuu yaliyofanyiwa utafiti ni katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na historia ya Zanzibar. Ofisi imefanya ukaguzi wa awali, imekusanya kumbukumbu tuli, imetoa ushauri na maelekezo muhimu kuhusiana na mfumo bora wa utunzaji na hifadhi ya kumbukumbu katika Wizara , Taasisi na Mashirika ya Serikali 20 Unguja na Pemba. Aidha, Idara imetoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi 17 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma - Zanzibar na Wanafunzi 169 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Kitengo cha Taaluma ya Teknolojia ya Uhandisi; wote wakiwa ni wanafunzi wa Fani ya Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka kwa Ngazi ya Cheti na Stashahada. (kiambatisho namba 4)

Mhe. Spika, wizara imefanya mazungumzo na Balozi wa Oman pamoja na Ujumbe kutoka Serikali ya Oman juu ya utekelezaji wa makubaliano ya kubadilishana nyaraka na msaada wa kuimarisha nyaraka zilizopo na kuziweka katika mfumo wa elektroniki. Mazungumzo bado yanaendelea ili kufikia maamuzi ya mwisho juu ya suala hili.
Mhe. Spika, idara imeratibu kikao cha Bodi ya ushauri juu ya masuala ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, matengezezo ya Jengo la Nyaraka yaliyohusisha upakaji wa rangi na ukarabati wa chumba cha kuhifadhiwa Nyaraka zinazotoka Mambo Msiige na malipo ya ada ya uanachama wa ICA yamefanyika. Vile vile, Katika kuimarisha usalama wa Jengo la Nyaraka utambuzi wa mitambo ya CCTV inayotarajiwa kufungwa katika Ofisi ya Nyaraka Unguja umekamilika.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imetumia jumla ya TZS. 133,581,924 kwa kutekeleza kazi za kawaida na 148,512,500 kwa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara imepanga kufanya ukaguzi katika ofisi za kuhifadhia kumbukumbu katika Mikoa na Wilaya, kuzifanyia matengenezo nyaraka na kumbukumbu chakavu na kuweka mitambo ya CCTV kwa ajili ya kuimarisha usalama wa Jengo la Nyaraka. Idara pia inakusudia kutayarisha Sera ya Menejimenti ya kumbukumbu na Nyaraka, kutayarisha Mfumo bora wa Usimamizi wa kumbukumbu na Nyaraka pamoja na kuimarisha Mfumo wa utunzaji kumbukumbu katika Masjala za Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali. Vile vile, kuwapatia mafunzo, warsha na semina wafanyakazi wa Idara na kuwawekea maslahi na mazingira bora ya kazi.

Ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 655,773,000. Kati ya hizo TZS. 230,267,000/= kwa kazi za kawaida na TZS 425,506,000/= kwa kazi maendeleo.

OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA – PEMBA

Majukumu ya Ofisi

Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya utawala na uendeshaji, mipango, sera na utafiti, mipango ya rasilimali watu na maendeleo ya watumishi, mishahara na maslahi ya watumishi, kuimarisha utawala bora na haki za binaadamu na kusimamia shughuli za hifadhi ya nyaraka na kumbukumbu za Serikali.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ilipanga kuimarisha shughuli za kiutendaji kwa kuajiri watendaji wenye sifa kulingana na mahitaji, kuwapatia mafunzo wafanyakazi 5 ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika fani mbali mbali, kuratibu mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa Watumishi wa Umma, kutoa elimu kwa watendaji wakuu wa Wizara na Taasisi za Umma na jamii juu ya misingi ya Utawala Bora, elimu ya Uraia na Haki za Binaadamu pamoja na kufuatilia uwezo wa Rasilimali Watu ili kubaini mahitaji na uwezo katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, Ofisi pia ilikuwa na lengo la kufanya uchambuzi wa kazi, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miundo ya utumishi katika taasisi za Serikali, kuendelea kuweka mazingira bora ya kazi kwa kununua na kuhifadhi vitendea kazi vya ofisi. Aidha, Ofisi ilipanga kuanzisha kituo cha uhuishaji wa kumbukumbu (*Conservation unit*), kuimarisha masjala, kutoa elimu kwa watendaji wakuu juu ya namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu, kutoa mafunzo kwa watunza kumbukumbu pamoja na kuanzisha vituo vya kumbukumbu vya Wizara na Taasisi za Umma. Ili kutekeleza malengo hayo, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 289,713,860 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, ofisi imeratibu mafunzo ya haki za binaadamu kwa shehia 6 za Pemba zikiwemo Kilindi, Ng'ombeni, Vitongoji, Kangagani, Kisiwani kwa Binti Abeidi, na Wingwi-mapofu, Ofisi imeratibu mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya Nchi ambapo watumishi 16 wamepatiwa mafunzo Nchini China na watumishi 8 wamepatiwa Mafunzo ya muda mfupi *ESAMI*, wafanyakazi 4 wa Ofisi wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu Nchini. Ofisi imeratibu matayarisho ya rasimu ya sera ya "*e- government*", Rasimu ya sheria ya kupambana na Rushwa, na rasimu ya sheria maadili ya Viongozi, mafunzo juu ya Utawala Bora yameotolewa na Taasisi ya *''Search For Common Ground''* kwa wafanyakazi 25 wa Ofisi hii. Kwa kushirikiana na Tume ya haki za binaadamu Tanzania Ofisi imetowa mafunzo ya elimu ya uraia na haki za binaadamu kwa wananchi wa Wilaya ya Chake Chake na Wilaya Wete, tathmini ya kumbukumbu katika Wizara ya Afya, Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya - Chake Chake zilifanyika.

Mhe. Spika, ofisi imeratibu ukusanyaji wa maoni juu ya uanzishwaji wa mfumo wa taarifa za Watumishi na mafunzo kwa Maofisa utumishi wa Wizara na Taasisi zake juu ya utayarishaji bora wa ikama, imeratibu mafunzo ya muongozo wa utoaji wa huduma kwa mteja, matayarisho ya fomu ya upimaji wa utendaji kazi na muongozo wa majukumu na upeo wa utendaji wa Serikali.

Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya TZS. 196,861,777 zimetumika kwa kutekeleza kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi kuu Pemba imepanga kuimarisha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano, kuratibu utayarishaji wa Sera ya malipo ya mishahara kwa Watumishi, kuratibu warsha juu ya matumizi ya sheria za utumishi wa Umma na kanuni zake, kuratibu mafunzo ya namna bora ya utayarishaji wa ikama, kuratibu mafunzo kwa Maofisa wadhamini juu ya uandaaji wa mpango wa rasilimaliwatu na mafunzo ya kuwaandaa Maafisa waandamizi kushika nafasi za uongozi.

Mhe. Spika, vile vile Ofisi imepanga kuratibu shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyowekwa. Kuratibu shughuli za Kamisheni ya Utumishi wa Umma na tume ya Utumishi serikalini kwa upande wa Pemba, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 4 wa Ofisi, kuratibu mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya Nchi, kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha kwamba vifaa na mahitaji mengine ya ofisi yanapatikana na kutoa huduma kwa wakati. Aidha Ofisi imepanga kuratibu mikutano ya wazi ya kutoa mafunzo ya

elimu ya uraia na kushauriana na wadau juu ya haki za Binaadamu, kuratibu kampeni juu ya haki za Binaadamu na mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa Serikali kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 489,586,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Majukumu ya Ofisi

Mhe. Spika, Jukumu la Ofisi hii ni kuidhinisha utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo na rasilimali nyengine kutoka Serikalini, Washirika wa Maendeleo kupitia Miradi, Programu mbali mbali na kutoa taarifa za ukaguzi kwa mujibu wa katiba. Lengo kuu la ukaguzi ni kuleta ufanisi katika upatikanaji wa rasilimali za Umma na matumizi yake, ili kuondoa ubadhirifu, wizi, matumizi mabaya ya rasilimali na kutotimiza wajibu wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Ofisi ilipanga kuandaa Mpango Mkakati wa pili wa mwaka 2011 - 2014 ambao utalenga kutekeleza na kushughulikia matumizi na maendeleo ya Ofisi, kuifanyia mapitio Sheria ya Ukaguzi Nambari 11 ya mwaka 2003 ili iendane na mazingira kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar. Aidha, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa kompyuta na ukaguzi wa mazingira. Ili kutekeleza malengo hayo, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 1,284,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Ofisi imeendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2010/2011 katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi. Aidha, Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2009/2010 imekamilika na tayari imeshachapishwa. Jumla ya Watumishi kumi na tatu na wajumbe wawili wa kamati ya kuchunguza Hesabu (*PAC*) walihudhuria mikutano mbali mbali ya kiukaguzi ikiwemo *INTOSAI, AFROSAI – E na SADCOPAC.*

Mhe. Spika, ofisi imeendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ambapo wafanyakazi thelathini na tano (35) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali. Vilevile watumishi ishirini na tano (25) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya ukaguzi yakinifu pamoja na tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi "*Risk Based Audit*". Aidha, jengo jipya lililonunuliwa na kufanyiwa ukarabati limekamilika.

Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya TZS. 1,092,342,235 zimetumika na jumla ya TZS. 15,000,000 zimekusanywa na kuwasilisha Hazina.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi itaendelea kufanya majukumu yake ya kukagua mahesabu ya Serikali na Taasisi zake kwa kupindi cha mwaka 2011/2012, kuwajengea uwezo watumishi wake katika fani mbali mbali, kupitia na kurekebisha muongozo maalumu wa ukaguzi na kutoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi na wadau na kushajihisha utumiaji wa viwango vilivyowekwa kimataifa katika ufungaji na uwekaji wa kumbukumbu.

Mhe. Spika, ofisi itakamilisha marekebisho ya Sheria ya ukaguzi Nam. 11 ya 2003, kuimarisha mawasiliano na wadau wake wote juu ya majukumu na malengo ya Ofisi kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano kama vile tovuti, majarida, vipeperushi, mikutano, makongomano na semina juu ya mwongozo wa ukaguzi. Vile vile Ofisi imepanga

kutoa mafunzo ya ukaguzi kwa komputa, ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa mazingira na aina nyengine za ukaguzi. Pamoja na kutumia muongozo wa kazi za ukaguzi, mafunzo hayo yana azma ya kuongeza ubora wa ripoti za ukaguzi zinazotolewa.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 1,889,000,000 kwa kazi za kawaida na kukusanya TZS.10,000,000.

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Majukumu ya Kamisheni

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni chombo kipya kilichoundwa mwezi Septemba 2011 kwa mujibu wa Ibara ya 116 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, Toleo la 2010, na kwa mujibu wa Kifungu Namba 17 cha Sheria Nam.2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, Majukumu ya Kamisheni ni kumshauri Mhe. Rais katika masuala ya utumishi wa umma, ikiwemo uteuzi wa watendaji wakuu wa taasisi za umma, mishahara ya watumishi wa umma, miundo ya taasisi za umma na mifumo ya utendaji kazi katika taasisi hizo. Kuwezesha na kusaidia utendaji wa Maafisa wakuu wa taasisi za umma ili kufikia utawala unaolenga kupata matokeo bora, kufuatilia na kutathmini utendaji wa Maafisa wakuu kwa kufanya uchunguzi na ukaguzi wa kila mara wa rasimali watu katika taasisi za umma na kushughulikia rufaa na malalamiko dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Kamisheni imeweza kutayarisha Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (*Strategic Plan*) 2011/2016, Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*), matayarisho ya Ikama, Mpango Kazi (*Work Plan*) 2012/2013, na Muundo wa Sekretarieti ya Kamisheni. Aidha, Kamisheni imefanya vikao vya kazi kumi na tano, imefanya uchambuzi yakinifu wa majukumu yake, imeanisha namna ya utekelezaji wake, iliandaa semina elekezi kwa viongozi wa Kamisheni, Uongozi wa Ofisi ya Rais utumishi wa umma na utawala Bora na Tume nne za utumishi wa umma kwa lengo la kupata ufahamu na tafsiri moja (*common understanding*) na kununua vitendea kazi vya Ofisi.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamisheni imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais katika mambo ya utumishi wa umma, kuzitangaza Sheria na kanuni za utumishi wa umma, kutoa miongozo, ufafanuzi na mafunzo kwa mamlaka za ajira na wadau wengine juu ya kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Kufanya uchunguzi na ukaguzi wa Rasilimali Watu katika utumishi wa umma, kupitia miundo ya utumishi, miundo ya taasisi na miundo ya mishahara kama itavyopendekezwa na Tume za utumishi, na pia kufuatilia na kutathmini utendaji wa Maofisa wakuu wa taasisi za umma. Kamisheni imepanga kutayarisha na kuwasilisha ripoti ya mwaka kuhusu hali ya utumishi wa umma kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Namba 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011. Pia itafanya ziara za kikazi kwenye mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 856,484,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Majukumu ya Tume

Mhe. tume ina jukumu la kusimamia utaratibu wa ajira Serikalini na Taasisi zake, kupitia miundo ya Utumishi wa Serikali, kupokea na kujadili malalamiko ya wafanyakazi, kujadili na kuyatolea maamuzi maombi ya muda wa ziada wa utumishi baada kufikia umri wa kustaafu kwa lazima, kutoa miongozo na ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi, upandishaji vyeo, kusimamia na kutoa maamuzi ya haki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazoongoza maswala ya Utumishi wa Umma na kusikiliza rufaa za wafanyakazi na kuzipatia ufumbuzi.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ilipanga kuwaelimisha wafanyakazi juu ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi Serikalini katika sehemu za kazi, kutayarisha mafunzo maalumu kwa Maafisa wenye kushughulikia masuala ya uajiri Serikalini juu ya Uajiri na HIV/AIDS, Uajiri na Jinsia pamoja na Uajiri na Ulemavu, kusimamia haki za wafanyakazi wa Serikali, na masuala yote ya kiutumishi yakiwemo uajiri, kupandisha vyeo, kuthibitisha kazi na kuvushwa vizingiti. Tume pia ilipanga kuendelea kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar katika kuandaa mafunzo na mitihani ya kitaaluma kwa wafanyakazi wa serikali ili kuwajengea uwezo katika utendaji wa kazi zao za kila siku. Ili kutekeleza malengo hayo, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS194,744,361 kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Tume imetoa elimu juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011 kwa Maofisa Wadhamini, Maofisa Utumishi, na Maofisa Tawala – Pemba, imetoa ruhusa ya Ajira mpya 240 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kutoa kibali cha nyongeza ya muda wa Utumishi kwa wafanyakazi 21, vibali 5 vya ajira ya mikataba, kuthibitishwa wadhifa/cheo watumishi 2, kibali cha kufukuzwa kazi watumishi 8, kuthibitishwa kazini watumishi 235, ruhusa ya likizo bila malipo watumishi 18 na kubalidilishwa kada watumishi 2. (Kiambatisho namba 5).

Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu jumla ya TZS.116,006,855 zimetumika kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha 2012/2013, imepanga kutoa mafunzo ya kujenga uelewa kwa Maofisa Utumishi juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake katika sehemu zao za kazi, Kuidhinisha Miundo ya Utumishi ya Mawizara 16 ambayo itakuwa ndio msingi wa upandishaji vyeo, kuthibitisha upandishwaji vyeo kwa Watumishi wa Umma kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi ya Kada mbali mbali, Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Rasilimali Watu na haki za Watumishi Serikalini, Kuandaa taratibu za kuajiri vijana wapya katika Mawizara na Idara zake kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyokubalika, kutoa mafunzo maalum kwa Maofisa wanaoshughulikia masuala ya uajiri Serikalini juu ya masuala mtambuka na kufanya matengenezo ya Ofisi, ili kuwawekea Watumishi ustawi mzuri na mazingira bora ya kazi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS. 253,218,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Majukumu ya Chuo

Mhe. Spika, Chuo Cha Utawala wa Umma kina jukumu la kutoa mafunzo ya kiutawala na kiutendaji kwa sekta za umma na binafsi ili kuwajengea uwezo watumishi wa umma na wadau wengine.

Malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 chuo kilijipangia kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali zikiwemo uhazili na utunzaji kumbukumbu. Chuo pia kilipanga kuipitia mitaala yake ili itimize mahitaji ya utumishi wa umma pamoja matakwa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi-NACTE. Malengo mengine ni kuwapatia fursa za kujiendeleza wafanyakazi wa chuo, kuinua maslahi ya wafanyakazi kwa kuandaa muundo wa utumishi na kufanya uchambuzi yakinifu pamoja na kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano.

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Chuo kimetoa mafunzo juu ya mbinu mpya za ufundishaji kwa wakufunzi wote wa Chuo na kutayarisha hadidu rejea kwa ajili ya zoezi la uchambuzi yakinifu linalodhaminiwa na Mradi wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma. Kwa upande wa kuimarisha mitaala; mitaala ya masomo ya rasilimali watu, utawala wa umma na wa uhifadhi wa kumbukumbu katika kiwango cha NTAL6 (*National Technical Award Level* 6) imepitiwa na kufanyiwa marekebisho. (Kiambatisho namba 6)

Mhe. Spika, Chuo kimefanya vikao vya Baraza la Chuo ambavyo vilijadili na kupitisha matokeo ya Wanafunzi pamoja na kupitia miundo ya Utumishi na bajeti inayojumuisha viwango vipya vya mishahara. Vilevile sherehe za mahafali kwa wahitimu wa mihula ya Januari-Juni na Julai-Disemba 2011 zimefanyika.

Mhe. Spika, kwa upande wa ukamilishaji wa jengo la Chuo – Tunguu, matayarisho ya ujenzi kwa awamu ya pili yameshaanza yakiwemo kupokea makisio ya gharama za kupaka rangi, kuunganisha huduma za umeme na maji, kuweka milango na madirisha na kutia vigae. Jumla ya TZS. 387,000,000 zitatumika kwa kukamilisha kazi hiyo.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kimepata Ruzuku ya jumla ya TZS. 261,466,301.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kimepanga kutoa fursa zaidi kwa watumushi wa umma na wadau wengine kujiunga na chuo kwa mafunzo ya ngazi za msingi, cheti na diploma. Aidha Chuo kitaendelea kuimarisha mafunzo ya muda mfupi ya kujenga uwezo wa watumishi wa umma sambamba na kuimarisha idara inayoshughulikia shughuli hiyo. Wakufunzi 2 watapatiwa mafunzo ya shahada ya pili ya uzamili na fursa zaidi za kuwaendeleza wafanya kazi wa chuo ndani na nje ya nchi zitaendelea kutafutwa.

Mhe. Spika, kazi nyengine zitakazo tekelezwa ni pamoja na kuajiri wakufunzi 10 wenye sifa, kuipitia sheria Namba 1 ya mwaka 2007 ya kuanzishwa kwa Chuo, kuongeza vitabu rejea katika maktaba ya Chuo, kununua vifaa bora vya kufundishia na kutoa huduma za utawala. Aidha, Chuo kinatarajia kuendelea na zoezi la kuipitia mitaala ili iende sambamba na matakwa ya Baraza la Elimu ya juu na Ufundi-*NACTE* pamoja na kuandaa na kuratibu vikao vya Baraza la Chuo, kamati ya uongozi na kamati ya taaluma, kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wa Chuo na kufanya ziara ya kubadilishana uzoefu pamoja kuzidisha mahusiano na taasisi za kimataifa kama vile *ESAMI* na nyenginezo. Aidha, Chuo kinatarajia kuendelea na ujenzi wa jengo la Chuo huko Tunguu.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 1,267,500,000 ambapo TZS 609,500,000 ni mapato ya Chuo na TZS 658,000,000 ni ruzuku kutoka Serikalini. Pia TZS. 300,000,000 zitatumika kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Chuo Tunguu.

TUME YA HAKI ZA BINAADAMU NA UTAWALA BORA:

Mhe. Spika, Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora ni chombo huru kilichoanzishwa kwa sheria ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora namba 1 ya mwaka 2001 ya Jamuhuri ya Muungano na kupewa mamlaka ya kutumika Zanzibar, kwa Sheria namba 12 ya mwaka 2003 ya Zanzibar

Mhe. Spika, Tume ina jukumu la kulinda Haki za Binaadamu, kusimamia Utawala Bora kusimamia haki, kufanya utafiti na pia kuishauri Serikali kwenye masuala yote yanayohusu haki za Binaadamu na Utawala Bora. Majukumu mengine ya Tume ni kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa Haki za Binaadamu pamoja na kufungua malalamiko mahkamani yanayohusu uvunjwaji wa haki za binaadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora.

Mhe. Spika, ofisi yangu imeweza kushirikiana na Tume katika kuratibu na kuwasilisha ripoti ya mwaka 2007/2008 ya haki za Binadamu katika Baraza lako Tukufu. Aidha, Ofisi ilishirikiana na Tume katika kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya haki za Binadamu Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012, Tume ilifanikiwa kukamilisha uchunguzi wa malalamiko 43 ya wananchi kati ya malalamiko 215 yaliyokusanywa, kuanzisha uchunguzi kuhusu uzingatiwaji wa Haki za Binaadamu katika ujenzi na matumizi ya barabara za Unguja na kufanya uchunguzi katika Wilaya za Magharibi, Kaskazini, Kusini na Kati (Unguja), Wete na Chake chake (Pemba) kuhusu uzingatiwaji wa haki za Binaadamu wakati wa kuwahamisha wananchi ili kupisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi ya Tume - Zanzibar imepanga kujikita zaidi katika kushughulikia masuala yanayohusu utekelezaji wa haki za Binaadamu hususan katika biashara.

TAASISI ZINAZOTARAJIWA KUANZISHWA:

Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi:

Mhe. Spika, kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi namba 1 ya mwaka 2012, Ofisi inategemea kuanzisha rasmi Taasisi itakayosimamia utekelezaji wa Sheria hiyo. Majukumu makuu ya Taasisi hiyo yatakuwa ni kuchunguza mambo na vitendo vinachopelekea kuwepo au kuruhusu kuwepo kwa rushwa, kushawishi au kusababisha kuwepo kwa vitendo vya makosa ya rushwa au kosa la kuhujumu uchumi. Aidha Taasisi hiyo itakuwa na jukumu la kusaidia Taasisi yoyote ya Serikali inayosimamia sheria katika kufanya uchunguzi wa kosa la rushwa au kosa la kuhujumu uchumi;

Mhe. Spika, majukumu mengine ni kushauri na kuelimisha wakuu wa Taasisi za Serikali au Binafsi juu ya mabadiliko ya mienendo na taratibu madhubuti katika kutekeleza vizuri majukumu ya taasisi hizo ili kupunguza uwezekano wa kutokea vitendo vya rushwa nchini.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tunaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 220,946,000 kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

TAASISI YA MAWASILIANO YA ELEKTRONIKI (*E-GOVERNMENT AND CENTRAL DATA-BASE*):

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya mfumo wa Serikali Mtandao, mfumo ambao unategemewa kuongeza ufanisi katika utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia mipango mikuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Dira ya 2020, Mpango Mkuu wa Kupunguza Umasikini - Zanzibar (MKUZA II) na kuzingatia malengo ya Milenia.

Mhe. Spika, Mfumo wa Serikali Mtandao sio tu utainufaisha Serikali bali pia wadau wengine mbali mbali kama vile Wafanyabiashara wa kawaida, makampuni ya simu, wazalishaji katika sekta mbali mbali, vyombo vya habari, utalii na wananchi kwa ujumla, hivyo kupelekea kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa uwajibikaji na kupunguza gharama za uendeshaji na utoaji huduma. Mfumo huu pia unajumuisha utunzaji wa pamoja wa kumbukumbu za msingi za serikali (*Central Data-Base*).

MAENDELEO NA MASLAHI YA WAFANYAKAZI:

Mhe. Spika, itakumbukwa Baraza lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011 na kuanza kutumika rasmi Julai 2011. Kupitishwa kwa sheria hiyo kumeleta mafanikio makubwa katika kusimamia masuala ya Utumishi ambapo utaratibu wa ajira kwa sasa uko wazi, kwani zinapotokea nafasi za ajira hutangazwa na kila mwenye sifa ana fursa ya kuomba nafasi hizo.

Mhe. Spika, katika kusimamia vyema utumishi wa umma sheria imeelekeza kuwepo kwa vyombo vya kusimamia masuala ya msingi hasa upatikanaji wa watumishi, haki na wajibu pamoja na rufaa za wafanyakazi. Vyombo hivyo ni Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi ya Mahakama, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na

Tume ya Utumishi ya Idara maalum vinavyosimamiwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Vyombo hivyo vimeshaundwa na vinaendelea kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, katika kuwatafutia ajira vijana wetu waliomaliza mafunzo katika vyuo mbalimbali, Ofisi yangu imefanya mazungumzo na kukubaliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (SMT) juu ya mgao wa ajira wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano - Tanzania kwa Wizara na Taasisi za Muungano (*quota*) kwa uwiano wa asilimia 21 kwa Zanzibar na asilimia 79 kwa Tanzania Bara. Hali hii itasaidia kupunguza idadi ya vijana wa Zanzibar waliomaliza mafunzo yao katika vyuo na taasisi mbalimbali za elimu ya juu ambao hawajaajiriwa na watakaomaliza miaka inayofuata.

Mhe. Spika, serikali baada ya kufanya marekibisho ya mshahara katika mwaka 2011/2012, hatua inayofuata kwa mwaka 2012/2013 ni kutoa nyongeza za mshahara za mwaka na kupandisha vyeo kwa wafanyakazi wote watakaotimiza majukumu yao kwa ufanisi, kuwapanga watumishi kwa mujibu wa miundo ya utumishi na kusimamia upimaji wa utendaji wao.

Aidha, Ofisi itaendelea na zoezi la kupitia na kuyafanyia marekebisho maposho mbalimbali ya watumishi wa umma (zikiwemo Taasisi za serikali zinazopata ruzuku na mashirika ya umma). Zoezi hili linategemewa kupandisha bajeti ya mishahara hadi kufikia Tsh. 139.6 bilioni kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

SHUKRANI:

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii adhimu kutoa shukurani zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa nyengine tena naomba kuchukua fursa hii adhimu kutoa shukurani zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani yake kwetu na kutukabidhi jukumu la kuisimamia Ofisi yake ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pia kwa miongozo anayotupa kila mara inayotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Spika, naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano ambayo yametuwezesha kuwasilisha hotuba katika Baraza lako tukufu leo hii.

Mhe. Spika, shukurani maalum tunazitoa kwa Katibu Mkuu Kiongozi, ambaye ni mkuu wa watumishi wa umma, kwa miongozo yake anayoitoa katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Utumishi wa Umma. Pia namshukuru sana Mwenyeketi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Wajumbe wa Kamisheni na Katibu kwa mashirikiano na ushauri tunaopata katika kufanikisha majukumu ya Ofisi yetu.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziwaendee Wenyeviti, Wajumbe na Makatibu wa Tume za Utumishi zifuatazo:-

- Tume ya Utumishi Serikalini;
- Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi;
- Tume ya Utumishi ya Mahkama; na
- Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Kwa mashirikianao mazuri tuliyonayo katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mhe. Spika, Shukurani za pekee ziwaendee wajumbe na wenyeviti wa Bodi ya ushauri ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bodi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa pamoja na Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma kwa kusimamia vyema majukumu yao na ushauri wanaonipatia katika kufanikisha majukumu ya Taasisi hizo.

Mhe. Spika, shukurani zangu za dhati nazitoa kwa watendaji wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora hususan Katibu Mkuu-Ndugu Joseph A. Meza, Naibu Katibu Mkuu-Ndugu Yakout H. Yakout, Wakuu wa Taasisi

zinazojitegemea, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Zanzibar na Jumuiya za Vyama Huru vya Wafanyakazi kwa mashirikiano na maoni yao wanayotupatia katika kuimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi. Ofisi yangu inafaidika sana na matokeo ya vikao vya mara kwa mara vya mashauriano vinavyofanyika kati ya ofisi yangu na Jumuiya ya Vyama Huru vya Wafanyakazi, ambapo ushauri wao umesaidia sana kufanya mazingatio yanayostahiki katika kushughulikia maslahi na maendeleo ya watumishi wa umma kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwa kuonesha imani yao kwangu na kunichagua kwa mara nyengine tena kuwa mwakilishi wao, na hatimae kwa imani hiyo hiyo, Mheshimiwa Rais akaniteua kushika wadhifa nilionao. Nawaahidi kwamba nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ujasiri na uaminifu. Pia naishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao kutokana na muda mwingi ambao, nalazimika kutumikia Taifa na kuwa mbali nao. Uvumilivu wao na mashirikiano wanayonipa yananiongezea nguvu na ujasiri wa kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Spika, mafanikio niliyoyaeleza katika hotuba hii, yamechangiwa na wengi na kwa namna mbalimbali. Kwa hivyo shukurani maalum nazitoa kwa Viongozi wote wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira na Ofisi ya Rais Utawala Bora za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Norway, USA, Japan, Korea, China, Uingereza, India, Singapore, Uholanzi, Malaysia, Australia, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Tume ya haki za Binaadamu, Benki ya Dunia, *UNDP*, *ADB*, *ILO*, *ESAMI*, *US-AID* na wengine wote ambao tunashirikiana katika kujenga Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, wizara inasimamia mafungu matatu ya Bajeti, fungu 11(Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), fungu 44(Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na fungu 47(Kamisheni ya Utumishi wa Umma).

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato, mafungu hayo yanategemewa kukusanya jumla ya sh. 1,450,000,000/= ambapo sh. 1,440,000,000/= kupitia fungu 44 na 10,000,000 fungu 11. Kwa upande wa matumizi, mafungu hayo yanategemea kutumia jumla ya sh. 7,648,990,000/= kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 6,240,484,000/= kwa kazi za kawaida na sh. 1,408,506,000/= kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, matumizi ya sh. 6,240,484,000/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida, jumla ya sh. 3,495,000,000/= ni kwa matumizi ya fungu 44 (zikiwemo sh. 658,000,000/= za ruzuku ya Chuo cha Utawala wa Umma), sh. 1,889,000,000/= kwa matumizi ya fungu 11 na sh. 856,484,000/= ni matumizi ya fungu 47.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono na sasa tuijadili, tumkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, awali ya yote, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Azza wa Jalla* kwa kutujaalia uhai na afya njema, na kuweza kufika hapa na kuendelea na kazi ya kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Wizara za Serikali na Mashirika yake, na leo hii tukiwa tunaijadili na hatimae kuiidhinishia wizara ya nne kati ya wizara kumi na sita za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pili napenda kuendeleza shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa kuniruhusu nitoe maoni kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini. Aidha, naomba nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa heshima na busara zake za kuiongoza nchi yetu ya Zanzibar, kwa kuheshimu misingi ya utawala bora. *(Makofi)*

Vile vile naomba pia nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kutekeleza malengo waliyojipangia, pamoja na majukumu yao kwa bidii kubwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, pia kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia wakati tulipopitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, nitakuwa sitendi haki ikiwa sitowashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao waliouonesha, wakati wote ambao Kamati ilikuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, na Kanuni ya 113 ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012 kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	- Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	- Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	- Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	- Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	- Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	- Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Mjumbe
8.	Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali	- Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	- Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	- Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi na shukurani hizo napenda sasa nitoe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Idara hii kwa kuwa na lengo la kuimarisha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano serikalini (*E – Government*). Hii ni hatua muhimu iliyokusudiwa kutoa nafasi kwa Viongozi, Watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla katika kuharakisha mawasiliano pamoja na kupata taarifa mbali mbali.

Mhe. Spika, kamati yako inaomba kuwasilisha mbele ya Baraza hili sikitiko lake dhidi ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya kutoipatia Kamati hizi gharama halisi zitakazotumika kwa mradi huo tokea kuanza kwake hadi kumalizika kwake, na gharama kwa kila '*component'* kwa kuwa mradi huu unajumuisha wizara nyingi.

Kwa hivyo, baada ya watendaji waliokuwepo ofisini pale kushindwa kutupatia gharama hizo na badala yake walituelekeza kwamba gharama hizo tutazipata Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa mnasaba huo, Kamati yako kupitia barua yenye kumbukumbu BLW/K.10/4 VOL.I/2 ya tarehe 16 Mei, 2012 iliiomba Ofisi hiyo itupatie gharama hizo ili zitusaidie katika kutelekeza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa huzuni natamka kwamba hadi nawasilisha hotuba hii gharama hizo hatujapatiwa. Kwa kuwa Wajumbe wako wana haki ya kupewa taarifa mbali mbali wanazozihitaji kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria Namba 4 ya mwaka 2007, tunaiomba ofisi hii itoe taarifa hizo katika Baraza hili, ili Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi ambao ndio walipa kodi wajue. *(Makofi)*

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Mhe. Spika, kamati yetu inaishukuru serikali kwa kuipatia idara hii, baadhi ya vitendea kazi zikiwemo kompyuta. Hii ni kutokana na kuwa hapo kabla idara hii ilikuwa na kompyuta moja tu inayofanya kazi, jambo ambalo ni kinyume au haliendani na majukumu mazito ya idara hii.

Mhe. Spika, kwa kuwa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ina jukumu la kutunza na kuhifadhi nyaraka mbali mbali za taifa, Kamati hii inawaomba Watendaji wa Idara hii kupanga vipaumbele vyao kwa kuzingatia majukumu yao.

Mhe. Spika, tunashauri hili baada ya kubaini kuwa watendaji wa idara hii hubaki ofisini kwa takriban miezi sita bila ya kuwa na shughuli yoyote, na hupokea mishahara bure kutokana na ukosefu wa vitendea kazi zikiwemo dawa za kuhuwishia nyaraka. Kwa kuwa Zanzibar inasifiwa katika kuhifadhi nyaraka zake duniani ni vyema hii tukaienzi, ili tusijetukafuata mgema akisifiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa jengo la idara hii ni dogo na limezungukwa na nyumba za wananchi na hata idara hii kudiriki kutumia mlango mmoja na raia, na kwa kuwa wamiliki wa nyumba hizo wamehitaji kiwango kikubwa cha fedha ikiwa ni fidia ya kuliachia eneo hilo serikali. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri serikali kubadilisha miundombinu ya jengo hili, ili mmiliki wa nyumba hiyo asitumie mlango huo kwa lengo la kuimarisha usalama wa idara hii.

Mhe. Spika, sambamba na hilo Kamati yetu imebaini kuwa baadhi ya eneo linalomilikiwa na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa limechukuliwa na wananchi na tayari wamejenga majengo yao. Kwa kuwa wananchi hao wamelitumia eneo hilo kwa zaidi ya miaka 12, na kwa kuwa Sheria za *'Common Law'* za Ardhi zinamruhusu mtu aliyetumia ardhi kwa zaidi ya miaka hiyo kuendelea kutumia ardhi hiyo, ingawa itakuwa inamilikiwa na mwenye ardhi.

Kamati yetu inaishauri Idara hii kufuatilia zaidi suala hili katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili kupata zaidi ushauri wa kisheria. Aidha, tunaishauri serikali kutafuta eneo jengine kwa lengo la kujenga ofisi mpya ya Idara hii itakayoendana na hadhi na majukumu ya Idara. Mhe. Spika, kutokana na kadhia hiyo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba serikali kuwa makini na maeneo yake ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Mhe. Spika, kamati yetu iliripotiwa kuwa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa upande wa Pemba imeliomba jengo la zamani la Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, ili shughuli za idara hii ziendelee kutekelezwa kwa ufanisi zaidi, kwani jengo wanalotumia hivi sasa, ambalo ni ndani ya Ngome Kongwe ya Chake Chake halitoshi, na pia mazingira yake si mazuri kwa hifadhi ya nyaraka.

Mhe. Spika, baada ya kamati yetu kufuatilia hili tulielezwa kuwa mazungumzo bado yanaendelea baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiunduzi na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa kuwa muda mrefu umepita na maamuzi hayajatolewa, kamati hii inaziomba ofisi mbili hizi kukamilisha mazungumzo hayo haraka iwezekanavyo, ili kuzinusuru nyaraka za taifa ambazo kwa kipindi hiki hazikuhifadhiwa katika mazingira yanayostahiki.

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Mhe. Spika, katika kitabu chake cha hotuba Mhe.Waziri ameeleza kuwa Idara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imepanga kusimamia na kuratibu mafunzo ya watumishi wa umma, kamati yetu imetiwa moyo na kauli hiyo. Hata hivyo, inaishauri Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu, kuwa makini zaidi wakati wa kutoa nafasi hizo hususan za nje ya nchi, kwani baadhi ya watumishi wanailalamikia idara hii kuwa inatoa nafasi kwa upendeleo, yaani kwa kujuana zaidi na sio kwa kumuendeleza kiutendaji Mtumishi huo.

Mhe. Spika, hapa tunamaanisha kwamba nafasi za mafunzo hupatiwa mtendaji ambaye hana taaluma na mafunzo husika au kwa lugha nyepesi sio kada yake, isipokuwa hupatiwa nafasi hiyo kwa kujuana. Pamoja na hayo, kamati hii inaishauri serikali kuweka utaratibu wa kuwaalika wakufunzi kutoka nje ya nchi kuja kutoa taaluma kwa watendaji wetu kuliko kuwapeleka huko, ili kupunguza gharama zisizo za lazima.

Mhe. Spika, takriban Wizara nyingi za serikali zinatoa nafasi za mafunzo ya nje ya nchi kwa watumishi wake bila ya kufuata utaratibu unaoeleweka. Kwa kuwa Idara hii ndio hasa yenye mamlaka ya kuwashughulikia watumishi wa umma kuhusiana na suala la mafunzo. Hivyo, tunaishauri serikali kuweka utaratibu mzuri wa idara moja tu kushughulikia suala hili na sio kuendelea na utaratibu unaotumika hivi sasa ambao hauleti tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

IDARA YA UTAWALA BORA

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza idara hii kwa kuandaa Sera ya Utawala Bora. Tunalipongeza hili kwani litaiwezesha Idara ya Utawala Bora kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri idara hii kutumia kamati zake kuchunguza na kufuatilia zaidi mwenendo mzima wa serikali, ili kuweza kupata kipimo cha Utawala Bora na sio kujikita tu katika kuandaa vipindi vya redio na televisheni. *(Makofi)*

Tunashauri hili baada ya kubaini kuwa Idara ya Utawala Bora bado haijayatambua makujumu yake, na inafanya kazi kama Jumuia Isiyo ya Kiserikali. Mhe. Spika, tunadiriki kutamka hivyo, baada ya baadhi ya watendaji wa Idara hii kutamka bayana na kushangazwa na masuala mbali mbali ambayo kamati yetu inayafuatilia, na kuona kuwa hatuna mamlaka ya kufanya hivyo.

Kutokana na hayo kamati yetu inawashauri watendaji wa idara kuitumia Sera ya Utawala Bora kama ni chachu katika kutekeleza majukumu yao kwani idara hii ina jukumu la kushughulikia Utawala Bora katika Wizara zote. Aidha, idara hii inapaswa kufuatilia masuala yote ya ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora katika utendaji wa Serikali na hata Jumuia zisizo za Kiserikali.

IDARA YA MIPANGO NA RASILIMALI WATU

Mhe. Spika, kamati yetu pia imetiwa moyo na utendaji wa idara hii, kwa kuanzisha zoezi la kuwahakiki watumishi wa umma, zoezi ambalo lilibaini mapungufu mbali mbali yakiwemo ya baadhi ya wizara kutowathibitisha kazi watendaji wake, mikataba ya ajira kutosainiwa, na mengi mengineyo.

Mhe. Spika, tunawaomba Makatibu Wakuu kupitia Wakurugenzi wa Idara ya Utumishi na Uendeshaji kuwa na utaratibu wa kuyafuatilia majalada ya watumishi kila baada ya muda fulani, ili kuhakikisha kuwa kila taarifa muhimu inayotakiwa kuwemo katika jalada hilo inapatikana.

Aidha, kamati hii inaishauri serikali kuanzisha utaratibu wa kuwajazisha mikataba watendaji wanaokwenda masomoni, ili kuwabana wale wote wenye nia ya kuacha kazi au kutafuta kazi katika eneo jengine baada ya kurudi masomoni. Hatua hii inaweza ikasaidia kuwadhibiti watumishi wa umma kuondoka afisini kiholela, pia itasaidia kuokoa fedha za serikali zisipotee ovyo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi Kuu Pemba pamoja na idara zake inazoziratibu na kujionea hali halisi ya utendaji wake wa kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mhe. Spika, kwa kiasi fulani tumeridhika na utendaji wa ofisi hii ingawa baadhi ya idara zake zinatekeleza majukumu yake katika mazingira magumu.

Kwa mfano, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, lakini kutokana na umakini, ubunifu na umahiri wa Kiongozi wa Idara hii ndugu Kombo Khamis Bakari, basi Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa - Pemba ilifanikiwa kutekeleza malengo yake kwa asilimia kubwa. Mhe. Spika, Kamati yetu inazishauri Taasisi za Serikali kufuata nyayo za kijana huyo, kwani anafanya kazi kwa kujitolea zaidi na kuweka kando maslahi yake binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, watendaji wa Ofisi Kuu Pemba waliilalamikia kamati yetu kwamba endapo Ofisi Kuu Unguja itaandaa shughuli yoyote Pemba, inawafanya watendaji wa juu wa kitengo husika kuwa kama waalikwa wa shughuli hiyo, wakati kiuhalisia wao ndio wenyewe. Mhe. Spika, kutokana na kasoro hiyo tunashauri kuwe na mashirikiano mazuri baina ya watendaji hawa ili kuleta tija iliyokusudiwa.

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 35 wa kitabu cha Hotuba ya Mhe. Waziri, tumeelezwa kuwa afisi hii itaendelea na jukumu la kukagua mahesabu ya serikali na taasisi zake kwa kupindi cha mwaka 2011/2012, tunaipongeza sana hatua hiyo.

Hata hivyo, tunaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuimarisha Ripoti ya Ukaguzi anazozitoa kwa kuingiza kipengele kinachohusiana na misamaha ya kodi, kuingiza kipengele kitakachopendekeza maeneo ya kupata mapato, na maeneo mengine yatakayosaidia kuonesha maeneo ya uvujaji wa mapato na yale yanayoweza kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunashauri hili baada ya kugundua kuwa Ripoti za Mdhibiti kila mwaka zinaripoti mambo hayo hayo, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya nchi. Kwa msingi huo si vibaya kutamka kwamba, ingawa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*). miongoni mwa majukumu yake ni kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya Serikali na Mashirika yake, na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mujibu wa kanuni ya 118(2)(a) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012. Kamati yetu imegundua kuwa Kamati ya *PAC* inatoa taarifa yenye kina zaidi ukilinganisha na ile ya Mdhibiti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na hayo kamati yetu inaishauri afisi hii kukamilisha marekebisho ya sheria yake kama ilivyoahidi haraka iwezekanavyo, ili nchi yetu iende sambamba na nchi nyengine duniani kuhusiana na masuala ya utendaji wa afisi hii muhimu, kwani muda mrefu umepita bila ya ahadi hiyo kutekelezwa kikamilifu.

Kuendelea kazi hii kusuasua kutaipelekea nchi yetu kushindwa kufuata miongozo inayotolewa katika Maazimio mbali mbali na Jumuia za Ukaguzi Duniani (*Lima and Mexico Declarations*). Mhe. Spika, katika kuifanyia marekebisho sheria hiyo kamati yetu inapendekeza pamoja na mambo mengine uingizwe pia utaratibu wa kupitishwa kwa bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili tuachane na mfumo unaotumika sasa na badala yake bajeti ya Afisi hii ipitiwe mbele ya Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*), na kisha kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kuidhinishwa.

Mhe. Spika, utaratibu huu sio mgeni kwani hata wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanautumia.

Mhe. Spika, kwa kuwa afisi hii inatakiwa kuwa huru katika utendaji wa kazi zake, yaani ifanye kazi bila ya kutegemea msaada wowote kwa kuangaliwa na kuona afisi hii ndio Msimamizi na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, kamati hii inaiomba serikali iwaongezee maslahi watendaji wa afisi hii, ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, tunatoa pendekezo hili baada ya kubaini kwamba Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2011/2012 imewaongezea Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani maslahi yao kwa asilimia kubwa, wakati afisa anayemkagua Mhasibu huyu analipwa mshahara wa mtumishi wa kawaida. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba huwezi kumkagua mtu kwa kufuata misingi ya kazi yako ikiwa wewe mkaguzi maslahi yako ni madogo kuliko unaemkagua.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Mhe. Spika, kamati yetu imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa na chuo hiki ya kwamba wizara za serikali zinashindwa kuwalipia wafanyakazi wake ada ya mafunzo, wakati Baraza la Wawakilishi kila mwaka linaidhinisha Kasma 221100 inayohusiana na Gharama za Mafunzo kwa kila Wizara na Idara ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kupitia wanafunzi wake ambao ni Watumishi wa Umma, kinazidai Wizara za Serikali si chini ya shilingi 26,433,000/- na wizara inayoongoza kutowalipia watumishi wake ni Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambayo katika mwaka wa fedha 2011/2012 tuliidhinishia Ofisi hii shilingi milioni 308,750,000/- kama ni fedha za Mafunzo ya Ndani na shilingi milioni 245,250,000/- za Malipo ya Ada.

Kauli yetu hii inathibitishwa na ukurasa wa 232 wa Buku la Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka 2011/2012 wakati watumishi wake wanadaiwa na chuo shilingi milioni 2,340,000/-.

Mhe. Spika, kwa ujumla deni linalodaiwa serikali na chuo kupitia watumishi wake ni kubwa sana kutokana na uasili *'nature'* wa chuo hiki. Mhe. Spika, kamati yetu inaziomba taasisi za serikali kukamilisha madeni hayo haraka iwezekanavyo. Tukizingatia kuwa chuo hiki kinakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ya ukosefu wa usafiri kwa Mkurugenzi wa Chuo, jambo ambalo linampa usumbufu mkubwa sana katika utendaji wake wa kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 44 wa kitabu cha hotuba cha Mhe. Waziri, tumeelezwa kuwa Chuo cha Utawala wa Umma kitaendelea na ujenzi wa Chuo chake huko Tunguu. Mhe. Spika, kamati yetu haikuridhishwa kabisa na kiwango cha gharama ya fedha kilichotumika hadi hatua ya ujenzi ilivyofikiwa, ingawa hatuna ujuzi *'skill'* wa ujenzi, lakini tuna uzoefu wa kutosha kuhusiana na masuala ya ujenzi, kwani kwenye baadhi ya mambo uzoefu unaweza ukatumika na ukakusaidia au ukakuelekeza ipasavyo.

Mhe. Spika, kutoridhishwa kwetu huko tunadiriki hata kutamka kuwa, kuna ubadhirifu wa fedha umefanyika. Kamati yetu katika kufuatilia hili, ilijibiwa na watendaji wa chuo kwamba kuna baadhi ya gharama hazikuwemo kwenye *'Bill of Quantity – BOQ'* ambazo pia zilizopelekea kuonekana kutumika kiasi kikubwa cha fedha. Gharama zenyewe ni pamoja na ujenzi wa kisima.

Mhe. Spika, pamoja na majibu hayo kamati yako bado haijaridhika na inaiomba wizara kufuatilia kadhia hii kwa kina, hasa tukizingatia kuwa Ofisi hii nayo pia haikuridhika na gharama hizo. Mhe. Spika, naomba kulikumbusha Baraza lako Tukufu kwamba kabla ya Chuo cha Utawala wa Umma kuwa chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kilikuwa chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na huko ndiko kunadhaniwa kuwa kulifanyika mchezo mchafu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, endapo itabainika kuwa kuna wajanja wamezitumia fedha za wavuja jasho wa nchi hii kinyume na utaratibu, basi serikali isisite kuwachukulia hatua zinazostahiki watendaji hao. Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara hii ina jukumu la kusimamia Utawala Bora, ni imani yetu kwamba suala hili litafuatiliwa haraka iwezekanavyo, ili kuzinusuru na shilingi milioni 300,000,000/- tunazomuidhinishia tena Mhe. Waziri kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, kutokana na kadhia hii na nyengine nyingi ambazo zimesharipotiwa mbele ya Baraza hili. Tunaiomba serikali kwa ujumla kuwa makini na kufuatilia kwa karibu zaidi matumizi yote ya fedha za kazi za maendeleo za taasisi zake, ili kuzinusuru fedha za walipa kodi wa nchi hii pamoja na fedha za Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kifungu cha 7(1) (b) cha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma ya mwaka 2007, kinatoa mamlaka kwa Baraza la Chuo kusimamia masuala ya fedha na mali nyengine za chuo baada ya kuidhinishwa na Waziri. Kamati yetu inaishauri wizara kuliachia Baraza la Chuo kusimamia ujenzi wa Chuo, ili kuzithamini na kuzipa nguvu sheria zetu tunazozitunga wenyewe.

Sambamba na hilo Baraza la Chuo ndio chombo cha karibu zaidi katika kufuatilia changamoto za Chuo. Hivyo, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuendelea kusimamia suala hili ni kinyume na matakwa ya sheria hii.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaunga mkono maamuzi yaliyofanywa na Ofisi hii ya kuipa kazi ya ujenzi Chuo cha Mafunzo baada ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo – KMKM kushindwa kulitekeleza hili ipasavyo. Mhe. Spika, pamoja na kuunga mkono kwetu huko, tunakiomba Chuo cha Mafunzo kufanikisha ujenzi huo mapema iwezekanavyo, ili kiweze kutumika kuanzia mwezi huu wa Julai, 2012.

Mhe. Spika, tunashauri hili ili kuondosha usumbufu kwa watendaji wa chuo hiki, kwani kwa hivi sasa Chuo cha Utawala wa Umma kinatoa huduma katika mikondo minne kama ifuatavyo. Katika jengo lake la Mizingani, wanafunzi wanaanza kusoma saa 2:30 asubuhi hadi saa 6:00 mchana, na wengine wanaingia saa 10:00 jioni hadi saa 2:00 usiku. Kwa upande wa Wanafunzi wanaosoma Skuli ya Hamamni, wanafunzi hao wanaanza kusoma saa 7:30 mchana hadi saa 10:45 jioni, na wengine wanaingia saa 11:00 jioni hadi saa 2:00 usiku.

Mhe. Spika, Chuo kuendelea kutumia utaratibu huu ni kwenda kinyume na matakwa ya Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na masuala ya Kazi Duniani *'International Labour Organisation – ILO'* kwani watumishi wa chuo hiki hutumia karibu masaa 55 kufanya kazi kwa wiki badala ya masaa 40 yanayotakiwa.

Sambamba na hilo kumalizika kwa ujenzi wa chuo hiki kutawaondoshea usumbufu wanafunzi wake, kwani Rais wa Chuo hiki pamoja na watendaji wake watapata sehemu ya kufanyia shughuli zao pamoja na kupata sehemu mahsusi ya kutoa huduma ya kwanza *'First Aid'* endapo mtu atafikwa na ugonjwa wowote, kwani mambo haya kwa sasa hayapatikani katika Chuo cha Mizingani.

Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinajihusisha pia kwenye masuala ya ujenzi. Tunaviomba vikosi hivi vitekeleze pendekezo la Baraza la Wawakilishi, la kuviandikisha vitengo vyao vya ujenzi kama Wakandarasi. *(Makofi)*
Mhe. Spika, kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake ya kawaida, ilielezwa na aliyekuwa Kaimu Waziri wa Ofisi hii ambaye pia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kuwa, serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga baadhi ya fedha kwa ajili ya kurekebisha kasoro mbali mbali zilizojitokeza kwenye mambo ya mishahara.

Mhe. Spika, kwa msingi huo kamati yetu inaiomba serikali kuyaangalia kwa kina maslahi ya Wakufunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma, ili kuwe na uwiano baina ya Vyuo vya Serikali. Kwani imebainika kwamba Chuo hiki Wakufunzi wake maslahi yao yapo chini sana ukilinganisha na Vyuo vyengine.

Mhe. Spika, naomba nithibitishe hili kwa kuiomba serikali kuangalia Vyuo viwili vya Serikali vya hapa Zanzibar jinsi vinavyowalipa Wakufunzi wao. Vyuo vyenyewe ni Chuo cha Habari na Mawasiliano ya Umma Zanzibar na Chuo cha Uongozi wa Fedha – Chwaka, na baadae ilinganishe na maslahi anayolipwa Mkufunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba serikali itekeleze hili haraka iwezekanavyo, kwani kwa hivi sasa Chuo kinatumia fedha za matumizi mengineyo *(Other Charges)* kwa kulipia tofauti ya fedha za mishahara kwa wakufunzi.

Mhe. Spika, Chuo ch Utawala wa Umma kinaendelea kutumia fedha za matumizi mengineyo. Kwa ajili hiyo ni kinyume na utaratibu. Sambamba na hilo kunakifanya chuo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
Mhe. Spika, natamka hivyo kwa kuwa ruzuku wanayopewa Chuo ni ndogo, ingawa kwa mwaka huu fedha zinaongezeka lakini Mhe. Waziri katueleza kuwa hadi robo tatu ya mwaka Chuo kimepatiwa Sh 261,466,301/- tu, wakati Baraza la Wawakilishi liliidhinisha Chuo cha Utawala wa Umma shilingi milioni 470.

Mhe. Spika, fedha za matumizi mengineyo zinatumika kwa kulipia tofauti ya wakufunzi na pia wanafunzi wa Chuo ambao ni Watumishi wa Umma wanashindwa kulipa ada za mafunzo yao. Kwa jumla mambo yote hayo matatu yanachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha utendaji wa Chuo hicho.

Kamisheni ya Utumishi:

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza serikali kwa kutengea kifungu Kamisheni ya Utumishi kama Sheria inavyoeleza. Ingawa jana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ametoa kauli mbele ya Baraza lako la kuwataka Wakuu wa Vikosi kutowakata fedha wapiganaji kinyume na utaratibu. Kwa kuwa mwaka jana kauli kama hii ilitolewa hapa hapa Barazani na bado wapiganaji hao wanaendelea kukatwa fedha hizo.

Kamati yetu inaomba Kamisheni iandae kikao cha pamoja na Tume ya Utumishi wa Idara ya Vikosi Maalum ili kuondosha kabisa tatizo la kuwakata fedha zao kiholela wapiganaji wa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
Mhe. Spika, tunashauri hili kwa kuwa Kamisheni ya Utumishi ndio chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi. Pia kina mamlaka ya kusimamia na utaratibu wa mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar. Hivyo Wakuu wa Vikosi hivi kuendelea kuzikata fedha za wapiganaji ni kinyume na taratibu.

Aidha kwa kuwa maslahi yenyewe ni madogo na endepo wataendelea kukatwa kiholela tutawasababisha wapiganaji wetu kuwa omba omba pamoja na kuingia kwenye mambo ambayo yasiyokubalika.

Kwa jumla Kamati imeridhika na Bajeti ya Wizara hii na inaziomba Wizara zote za serikali kusimamia vyema fedha na maposho maalum, viburudishaji, *stationery*, mafuta na vilainisho. Imebainika kuwa baadhi ya Watumishi wa Umma hutumia vibaya kasma hizi.

Mhe. Spika, naiomba Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo kuwa makini wanapoandaa buku la Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi ya kawaida na kazi za maendeleo. Kwani kuna baadhi ya taasisi majina yake yanaandikwa kinyume na yanavyotamkwa kwa mfano: Kamisheni ya Utumishi, Fungu Nam. 47 ukurasa wa 673, neno "Katibu Mkuu wa Kamisheni ya Utumishi", imeandikwa hivyo lakini inatakiwa isomeke "Katibu wa Kamisheni ya Utumishi" na mengi mengineyo.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya Kamati niwaombe sasa wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi tukufu wayakubali na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyoidhinishwa na Kamati yetu ambapo afisi hii imepangiwa kukusanya jumla ya Tanzania shilingi bilioni moja, milioni mia nne na khamsini.

Aidha kwa upande wa matumizi wa kazi za kawaida Afisi imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni sita, milioni mia mbili na arobaini, laki nne na themanini na nne elfu. Na kwa upande wa kazi za maendeleo Afisi imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia nne na nane na laki tano na sita.

Hitimisho

Mhe. Spika, napenda sasa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu. Pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwa niaba ya Kamati, Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini walionichagua naunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Aidha naomba tena Wajumbe wote tuichangie na kuunga mkono makadirio ya bajeti ya Afisi hii ili kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru mchana huu kunipa fursa hii kuchangia mawili matatu katika kitabu hichi cha rafiki yangu Mhe. Haji Omar Kheri, kwa kuanza bila ya kupoteza muda tuangalie ukurasa wa 48 unazungumzia "Maendeleo na Maslahi ya Wafanyakazi".

Mhe. Spika, hapa imepatikana neema kidogo lakini neema yenyewe naona kama ni ndogo kwa asilimia 21 kwa 78 kama Zanzibar ni nchi, hii ni asilimia ndogo. Ukiigawa hii kama kuna wanafunzi 10 waliopelekwa, tutapata wawili tu, angalau ingefika 40 kwa 60.

Mhe. Spika, kuna taarifa kuhusu Chuo cha Diplomasia kumepelekwa wanafunzi 10 wanne wakarudishwa kutokana kuwa hawana sifa, kwa mtoto wa mjomba na shangazi, matokeo yake ndio kama tunavyosema maslahi yatatuweka pabaya. Hapa nitahitaji maelezo kuhusiana na ukweli huu.

Kwa kuwa tumeingia katika fomula ya kusomesha watoto wakati mwingi tumekuwa tukipiga kelele hapa kuhusu nafasi za ubalozi kuwa mgao unakuwa ni mdogo. Lakini wakati huo huo tunawapeleka watu wenye sifa ambazo haziridhishi, tunawaacha watu wenye sifa kuwapeleka kwenda kusoma tunawapeleka watu ambao hawana sifa.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 40, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012, Tume ya Utumishi. Kwanza nikupongeze kabisa Mhe. Waziri wa kuwaajiri walimu 240 lakini hawa walimu wa sayansi na hisabati sijui utawagawa vipi. Hata robo yake wajakidhi kutokana na kilio cha walimu wa sayansi. Sisi sote tumeshuhudia hivi karibuni wanafunzi wa kidatu cha nne karibu wame *disqualified*, hawalaumiki atautafuta mtihani japo kwenda kuukopi au kwenda kuununua kutokana na walimu kutokuwepo. Kwa hapa hii hali hairidhishi kabisa ya walimu 240, tujitahidi kuongeza.
Mhe. Waziri mimi sitaki uje upate shida kama rafiki yetu Mhe. Mwinyi Haji alikuwa anafanya mazoezi ya kuinuka na kukaa kitako. Hili itabidi uje unipe maelezo, juu wa watumishi hawa waliostaafu wana sifa gani hata wakarudishwa. Hawa itabidi utueleze kwa majina kama kweli hatuna watu wa kuwaajiri hapa nafasi hizi au vipi.

Nije katika ukurasa wa 46. Hiki ni kitengo kipya na nimpongeze kwa dhati kabisa kuundwa kwa kitengo hichi cha Mamlaka ya Rushwa. Kwa kweli bajeti uliyoiingiza hii milioni 200, hakikidhi hiki kitengo. Itakuwa hao tunaotaka kuwaajiri itakuwa mtihani, utamkuta mtu anaendesha vespa kama mimi utakuja kumuweka kitengo kama hichi atafanya kazi gani. Vile vile nataka kujua Makao Makuu yake yatakuwepo Unguja au yatakuwepo Pemba, pia katika kitengo hichi tujue ni vijana wangapi utawaajiri. Pamoja na yote suala la mafunzo ni muhimu kwa hichi kitengo.

Kulikuwa kuna askari alikwenda kusoma Moshi baada ya kurudi hapa akawa anahamu ya kufanya kazi. Baada ya kumuhoji mtu akaanza kumpiga virungu, matokeo yake akafa yule mtu ikawa hapana kesi yoyote.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia machache kuhusiana na Wizara hii mpya.
Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutupatia uhai na uzima tukaweza kuzungumza katika Baraza lako tukufu. Wizara hii ni muhimu sana Mhe. Spika. Baada ya kupatikana kwa Sheria ya *Public Service Act No. 2* ya mwaka 2011 iliyofanya kwamba ndio muelekeo wa Wizara hii.

Pia namshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kutuletea hichi kitabu cha Sera ya Utawala Bora. Nikianza katika mchango wangu kwanza natoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Waziri kwa kuweza kuvitaja vitengo vyote kwa ufasaha na kila kimoja akatoa mapendekezo ya matumizi na mapatio ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo bado hatujalisikia ni Kanuni za hii Sheria. Baada ya kupitishwa Sheria hii ilikuwa inahitaji kuwa Kanuni ili iweze kufanya kazi nzuri huko chini ambapo wafanyakazi wapo. Mimi namuuliza Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizochangia kwamba Kanuni zinachelewa mpaka hivi leo na hata hazijatatwa kama zimeshafanyika.

Mhe. Spika, kukosekana kwa Kanuni kumeshaanza kuonekana taathira yake sasa hivi. Karibuni hivi hata Mhe. Waziri mwenyewe alipokuwa akijibu swali hapa katika Baraza lako tukufu alikiri kwamba baadhi ya walimu wamekatiwa mishahara yao kutokana na upekuzi uliofanyika, kwamba hayakutimizwa masharti ya vyeti.

Mimi ningelimuuliza Mhe. Waziri wale walimu walikuwa wanafanya kazi kwa mkataba na wanafanya kazi chini ya walimu wakuu wao. Ni kwa nini mishahara yao ikakatwa moja kwa moja bila ya kupewa barua na kupitia kwa walimu wakuu wao wakajua kwamba kabla hajenda kuchukua ule mshahara kwamba mshahara wake unakatwa kwa sababu kadha, kadha, kadha. Ni sababu zipi za msingi walizokuwa wamekatiwa mishahara yao wale walimu bila ya kupitiwa wao kwa barua na wale walijaza mkataba wa kuingia katika kazi.

Mhe. Spika, la pili la kushangaza ni kwamba kulibakisha mwezi mmoja tu kabla ya bajeti hii kumalizika ya 2011/2012 ni kwa nini Wizara hii ikachukua hatua ya ghafla sana, kwamba katika mwezi ule mmoja uliobaki isiwaachie kwanza ili wakajitayarisha. Moja katika kuwa *treat* wafanyakazi ni kujenga *moral* yao ya kufanya kazi. Kama kuna kosa lililotokezea badala ya kuwakata mishahara moja kwa moja wakenda wakashtukia imekatwa. Ingelifaa wangelipewa barua na mapema kuwe kujulishwa kwamba kuanzia Julai 2012 mishahara yetu itakwenda hivi.

Kwa sababu wamekatiwa katika mwezi huu namuuliza Mhe. Waziri Fedha hizi mbona hakuzirudisha hapa katika Baraza na walimu wameshakatwa. Hizi zimeingia katika mfuko wa nani. Wakati wa kujibu Mhe. Waziri aje atwambie walimu wangapi amewakata mishahara yao na fedha hizo kazipeleka wapi.

Mhe. Spika, jambo jengine kuna msemo unasema kwamba “deni halifutiki” “wema hauwozi” “Fanya upendalo, kadri utakavyofanya na wewe utafanyiwa” Serikali yetu tukufu ilipandisha mishahara kwa fomula ya kiutaalamu lakini bahati mbaya Mhe. Spika, kuna mawizara ikiwemo ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Wizara ya Maji, Ardhi, Nishati, baadhi ya wafanyakazi wake wengi sio wale wenye ngazi ya kitaaluma hata kuanzia *form IV* lakini ni wafanyakazi waliokaa muda mrefu katika kazi, wana uzoefu mkubwa, kuanzia miaka 20 na kwenda juu wamefanya kazi, lakini mishahara yao haikupanda.

Sisi katika kamati tulipofuatilia Mhe. Spika, tulihakikishiwa na Wakurugenzi kwamba hiyo ni kweli na kwa sababu fomula ilimezeshwa *form IV* kikiingizwa chengine chochote formula ile haikubali. Wakurugenzi walikiri kwamba

wamewaandikia Wizara yako ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwaeleza kuhusu tatizo hilo. Humu naomba hukulieleza. Hebu njoo utupe ufafanuzi kuhusu wafanyakazi hawa wamewekewa wapi wao. Ni wafanyakazi ambao wamefanyakazi muda mrefu, wametumikia taifa hili. Hawakukosea wao kuwa hawakufika *form IV* ni mazingira ambayo yaliwafanya wawepo hapo. Lakini wameshafanya kazi muda mrefu na hao waliokwenda *form IV* wanawafundisha wao baadhi ya mambo. Kwa nini formula haikuwameza na wao ikawapa nyongeza.

Kompyuta kwenye hizo *softy ware program* hizi inategemea namna ulivyoitengeneza. Ukiitengeneza kwamba ni *form IV, STD 8* haiwezi kumezwa au *form II* haiwezi kumezwa. Sasa kwa nini hawa hawakutengenezewa *soft ware* yao ili na wao wakapata maslahi ya nyongeza hii. Mhe. Waziri utakapokuja naomba uje utueleze ni kwa njia gani wafanyakazi hawa mmewafikiria na hali ya kwamba Wakurugenzi wa Wizara hizi mbili nilizozitaja tayari wamewandikia na kuwaeleza kuhusu tatizo hili.

Mhe. Spika, hii ni wizara ambayo imeambatanishwa na utawala bora. Kwanza niseme kabisa naunga mkono sana maoni ya Kamati kwamba neno Utawala Bora pale ni kitu mtambuka kwa ile Wizara iweze kushughulikia na Wizara nyengine. Kwamba utawala bora unakuwa unafanya kazi katika kila wizara. Sio utawala bora ndani ya wizara yao tu. Wao wamewekewa dhamana ya kuona kwamba utawala bora unakuwa unafanya kazi katika kila wizara ambayo imo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kama kuna watendaji wanakiuka hivyo au wanaona kwamba wao ni pale tu, hilo litakuwa ni kosa. Bila shaka kitengo hichi au idara hii itakuwa na dhamana kamili ya mafunzo ya kila wizara kuhusu namna gani ya kuendesha utawala bora ndani ya wafanyakazi wa wizara ile.

Mhe. Spika, jengine linalonitia wasi wasi kidogo, ni kupatikana kwa idara mbili zenye madhumuni yanayokaribiana kuwa mamoja, nina wasi wasi juu ya utendaji wao. Kwani kila mmoja atataka ku-*compete* kufanya lile la mwenzake. Ima idara hizi ziunganishwe au zilazimike kushirikiana. Idara ya Mipango na Rasilimali Watu, na Idara ya Mafunzo na Rasilimali Watu. Hizi kidogo naomba Mhe. Waziri aje atueleze ni kwanini zikabaguliwa na hakuna migongano katika kuzibagua Idara hizi mbili, hakuna mivutano, zote zinahusiana na rasilimali watu. Kwa sababu unaanza kupanga, unafundisha, halafu unapata hiyo rasilimali watu. Lakini mipango mbali, mafunzo mbali, wanaoshughulikiwa ni wale wale rasilimali watu. Kidogo miye inanihangaisha kuwepo idara mbili hizi. Ukenda katika watumishi wenyewe watakupa tabu kwa sababu kila mmoja atazuia nafasi yake. Sasa nenda katika *reality* na fanya uchunguzi wako.

Mhe. Spika, jambo moja ambalo nalo vile vile sijaliona katika hotuba ya Mhe. Waziri. Katika idara hizi mbili ambazo zote zinashughulikia rasilimali watu. Sisi tuna vyuo vyetu hapa tayari vinatoa taaluma mbali mbali, nani mwenye dhamana katika idara hizi ya kuona kwamba kunakuwa na uratibu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ni mafunzo gani ambayo nchi yetu inahitaji ili kupata rasilimali watu. Hatuwezi kuwa na vyuo ikawa vinasomesha tu mafunzo yoyote, wakati sisi tunataka rasilimali watu zitufae sisi wenyewe.

Mhe. Spika, hatujaona hapa kwa mfano Chuo cha Uvuvi, wakati sisi tunayo rasilimali kubwa ya bahari. Je, Wizara yako kama hii inayoshughulikia rasilimali watu inaridhika kwamba vyuo vyetu bado havijatoa mafunzo hayo. Hakuna msisitizo mkubwa wa kuhusu mafunzo ya ufundi katika vyuo vyetu. Vyuo vyetu tulivyovijenga hapa ni vya nadharia zaidi, kile Chuo cha Ufundi nilimuuliza siku moja Mhe. Waziri ambacho kinaitwa Taasisi ya Sanyansi ya Teknolojia, je yeye mwenyewe Waziri anaweza akaitizama akaijua kwamba hii ndiyo taasisi au akenda pale akitizama yale majengo yake ni basi.

Siku hizi kidogo angalau lile bweni nashukuru kwamba linatengenezwa linatizamika kidogo. Lakini ukenda kwenye kile chuo na *standard* yake ni mashaka. Je, tuna taasisi kama hii na Wizara ambayo inatayarisha rasilimali watu imesaidia kiasi gani hichi chuo kukua ili kikatoa hiyo rasilimali watu ambao tunawahitaji. Haiwezekani kukaa *stagnant*, hivyo huwezi kupata rasilimali watu ikiwa huna *coordination* na Wizara ya Elimu ambayo ndiyo inayoshughulikia hiyo rasilimali watu. Tungetaka kujua hasa ni nani aliyekabidhiwa katika Idara mbili hizi, imekabidhiwa Idara ya Mipango au imekabidhiwa Idara ya Mafunzo.

Mhe. Spika, moja katika *principle* ya sheria hii tuliyoipitisha hapa, kasoma kifungu cha 5, kwa bahati miye nimeipata sheria yenyewe lakini katika kiingereza.
Kifungu cha 5

(1) "The public service shall be governed by the inherent values in the relevant duties or such values specifically developed and applicable to such duties.

(2) In addition to such values, the service shall be bound by the following common public service values:-

(a) employment decisions in Zanzibar public service is made without patronage, favoritism or political influence."

Uajiri Zanzibar, hauangalii mtu wala, hauna upendeleo, wala hauna mrengo wa kisiasa. Hii ndio sheria inavyosema. Mimi naheshimu sana maoni aliyotoa mwanasheria Mkuu jana kuhusu *position* ya *GSO* kuwa pale ilipo.

Lakini malalamiko yaliyopo kwa vijana wetu wengi wanaokwenda ni kwamba masuali yanayoulizwa bado yanapelekea kuwa na upendeleo fulani. Bado yanapelekea kuwa na mrengo wa kisiasa fulani. Sisi tukisema kwamba tunaajiri lakini baadhi ya vijana wetu hawaajiriwi kwa sababu fulani fulani. Ukifuatilia utaona kwamba *pre-requisite* ya ajira wizara hii haina kauli ya mwisho, kauli ya mwisho inatoka GSO. Kama hajatoa kauli GSO huwezi kuajiriwa, GSO bado maswali yao yana mirengo ya upendeleo. Sasa hapo ndio nilipo miye, miye sipingani na sheria kwamba iliwaweka pale ikawapa majukumu.

Mhe. Spika, nafikiri haya majukumu mengine ikiwa tutaruhusiwa huko siku za mbele basi labda tuje tuzungumze kwamba je, wametekeleza au hawajatekeleza. Mimi nataka niitafute hasa hiyo sheria kwa sababu jana nilipata maelezo mazuri kwamba sheria hii ipo na ndio kuna malalamiko kama hayo. Ndio tukasema kwamba hii *section* ya utawala bora madhumuni yake huyo aliyeiweka mimi namshukuru sana Mhe. Rais sana, kabisa. Tena katika pahali alipopatia kuuweka Utawala Bora kuweka pamoja na Utumishi wa Umma. Hapo ndio penye *central core* ya matatizo ya nchi, ukianza hapo kila mmoja *concerned*

Nasema hivi kwa sababu miye bahati nzuri nilianza na kazi ya uwalimu, tena ya muda mrefu sana. Nikifika hapa wakanambia wale wanafunzi wangu hatukupata ajira kwa sababu kadhaa. Huwa nachukia sana. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aje atueleze hichi kitengo je, madhumuni yake mazuri lakini kazi yake anaifanya kwa uwadili? Kazi yake anaifanya kwa mujibu wa taratibu tulizokubaliana?

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba hii wizara ni muhimu ninukuu kifungu cha 2 katika hapo niliposema

"5(2) (b) *appointments and promotions in Zanzibar public service officers are made on the basic of merit;"*

Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa kusema kwamba kuna kitengo cha kutathmini wafanyakazi. Hiyo nashukuru sana kwamba kimewekwa lakini bado tunaangalia vipi *promotion* za wafanyakazi zitakavyoendelea.

Mhe. Spika, katika kuona kwamba wafanyakazi wetu hasa wataalamu wanabaki nchini ni lazima waone kwamba wametendewa haki. Mimi naamini kwamba kuna wengi ambao ni wazalendo. Lakini baadhi ya nyakati haki inakuwa ni ndogo wanayotendewa. Tuna *level* ya maofisa tofauti katika idara kwa mfano, kuna watu watano ambao wote wana *masters degree*, lakini wakati ikitokezea nafasi ya Mkurugenzi atachaguliwa mmoja wao katika wale watano.

Ndivyo ilivyo kwa sababu ni mmoja tu atakayekuwa mkurugenzi. Lakini tatizo lililopo katika urekebishaji wa mishahara ni kwamba huyu Mkurugenzi anawapita sana wale ambao wapo *level* moja na wale ndio watakaeshirikiana naye katika kazi. Sasa kwa hivyo mimi naiomba sana Wizara hii katika kupanga maslahi haya ione kwamba kuna *gap* ndogo tuiweke ile *appointment gap*, hiyo ni lazima ipatikane. Kwamba kuna *gap* ndogo ya ile *appointm*ent yake kwamba yeye kateuliwa sasa ni hivi. Lakini isiwe kwamba kawapita sana kiasi cha kwamba anawatuma bizari. Kuna lugha ya mitaani kwamba mtu mkimpita sana unamwambia mimi naweza kukutuma bizari tu weye. Hiyo itawavunja moyo wale kwa sababu wapo *level* moja na kazi zinafanywa na wote. Tuangalie mshahara anaobakishwa nao pale yule ambaye ana *Master degree* lakini kapata *Presidential appointment* anakwenda vipi.

Suala la mwisho ambalo mimi nataka nilizungumze sasa hivi ni kumuuliza tu Mhe. Waziri mbona hii kazi ya mafriji inaendelea. Huo ni mpango maalum uliopangwa? Hebu njoo utupe habari kidogo Mhe. Waziri ununuzi wa mafriji unaendelea na humu 28 milioni lipo, 30 milioni lipo, mafriji haya yalikuwaje? Mhe. Waziri vichaka vinaonekana.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri na nimuombe sana kwamba hii wizara ni tete sana kwa sababu karibu asilimia nzuri ya wafanyakazi wa Zanzibar wapo Serikalini na wanatizama mambo gani yanavyokwenda. Namuomba sana awe na *coordination* ya karibu sana na wizara nyengine kupata busara. Haidhuru watendaji wako wamepewa *mandate* ya kufanya baadhi ya mambo, lakini kunatakiwa ushirikiano mkubwa katika mawizara.

Mhe. Spika, kila pahala kuna *culture* yake. Ku- *deal* na walimu kuna *culture* yake, ku-*deal* na wafanyakazi wa ngazi ya chini kuna *culture* yake. Ku-*deal* na wataalamu kuna *culture* yake, haidhuru wizara hii imepewa *mandente* lakini inafanya kazi katika karibu na wale watendaji wakuu wa mawizara ili kuweza kuona kwamba wanakwenda kwa pamoja. Kwa mfano kupelekewa barua yenye madai kama hayo ikawa haijajibiwa si aibu hiyo. Mkurugenzi anaandikiwa barua wa wizara yako, anakaa miezi miwili mitatu haijibiwi barua ile.

Mhe. Spika, nakushukuru, nitaunga mkono hoja itakapokuwa mambo haya ya mafriji yatakapokaa sawa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wawakilishi wa upande wa CCM kwamba kile kikao ambacho kiliakhirishika jana leo kipo pale pale mara baada ya kuakhirisha kikao hichi. Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote wajibu wetu kushukuru kwa Mwenyezi Mungu kutufikisha leo hii alhamdu lillahi roho ziko salama na tuna afya hilo ni moja ambalo ni tukufu kubwa la kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwenyekiti aliyoitoa hapo eo asubuhi na mimi imenibidi niunge mkono kwa maelekezo aliyotoa. Mheshimiwa hii ndio ofisi ya utawala bora, ofisi hii *include* na sheria. Ofisi hii Mheshimiwa watu wengi labda inakuwa hatufaham nini dhamira ya utawala bora. Lakini mimi Mheshimiwa ninafaham nini dhamira ya utawala bora, kwa Kiswahili cha kwetu utawala bora ni utawala ambao unakwenda na sheria. Ni utawala ambao hauendeshwi mabavu ndio ninavyofaham mimi. Na ndio maana dhana hiyo ikawepo na Mhe. Rais akaweza kutafuta Wizara husika akaipa kwa jina la upande wa pili kuwa ni utawala bora wa usimamizi.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika utawala bora mna haki nyingi mule ambazo sisi wazanzibari tunawajibu tuweze kuzipata. Na hasa katika huu mchakato wa Katiba sasa hivi na hasa mambo ambayo ya sheria kuweza kuyatambua hapa ndio pahali pale Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kuwa palipokosewa pamekosewa lakini sasa tusirejee kosa kwa sababu unaporejea kosa unaonekana ndio jeuri sasa hivi. Maana ya kusema tuna mchakato wa kurekebisha baadhi ya vifungu vya katiba hapa ndio pahali pale Mheshimiwa tujitahidi kuwasaidia Wazanzibar ili kufahamu hasa ndani ya dhamana ya utawala bora. Mheshimiwa mara nyingi sana wazanzibari hawajui masuala haya hasa Katiba, hata hiyo Katiba ya Zanzibar hawaijui lakini wanaisikia Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini hawaijui. Lakini kumbe kulikuwa na vyombo ambavyo ni rahisi sana Mheshimiwa vingeweza kuwaelimisha wazanzibari basi wangejua haki zao zikoje.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar si visiwa vya kuwa maskini, Zanzibar si visiwa vya kuwa na upungufu wa wataalam. Nimshukuru sana Rais aliyepita Mhe. Rais Salmin ametuanzishia vyuo vikuu, sasa tumo katika jamhuri ya Muungano tuna elimu ya juu ambao ndani yake tunapata mafungu yetu ya kuweza kuwasomesha watoto wetu lakini hatimae hatuna.

Lakini mimi nataka kumuuliza husikia zogo kuwa Mhe. Waziri Mkuu alitoa tamko lakuwa tupewe bilioni kumi na nane, hebu naomba Mheshimiwa wangu waziri na wewe kama ulikuwemo kwenye kikao hicho, kama kuna *minutes* ya kikao hebu tunaomba tuletewe kwenye Baraza ili tuone uthibitisho ni kweli au tumedanganywa. Kwa sababu

kusema si hatua ya utekelezaji lakini ukiandika kama ninavyojua Mwanasheria Mkuu alivyonifundisha andiko ni andiko halitoweza kufutika. Na ndio maana mara nyingi sana mimi huwa nina wasiwasi yale majadiliano tunapokaa na wale wenzetu kuwa hakuna *minutes* za kikao ndio mimi ninakuwa ninashtuka, au hakuna *agreement* fulani kusema kuwa mwaka huu tumetia mkataba wa kumaliza suala hili. Sasa mimi hapo Mhe. Naibu Spika, huwa ninakasirika sana linaniuma sana jambo la Zanzibar na kila nikisimama hii ndio itakuwa slogan yangu kuzungumzia tunataka haki zetu tupewe wazanzibari tupewe ili tuendeleze maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, hichi kisiwa dakika mbili tu ukipata fedha ambazo tunadai huko basi ninakuhakikishia itakuwa ni *half* London ndani ya Zanzibar, tukizipata tu hizo pesa. Na tutazipata kwa uwezo wa Mungu viongozi tupo, na tunaambiwa wananchi watuamini na tutafanya kazi hiyo na fedha tutazitia mambo kidogo kidogo tu. Tume imekuja wananchi wende wakatoe maoni ya kwa salama salmin bila ya matatizo yoyote, litazunguka mwisho wa habari litaingia kwenye shimo hili. Sasa hapo watuone viongozi tunawadaia haki yao Wazanzibari ili kupata maslahi yao ndani ya muungano wao.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi niende katika mchakato wenyewe hasa, nikiingia katika ukurasa wa tatu lakini kabla sijaingia ukurasa wa tatu leo asubuhi kulikuwa na vichekesho. Mheshimiwa wangu mmoja alianza vichekesho hivyo, lakini mimi nilivyoona katika lile buku kubwa kuona friji linanuliwa kwa pesa nyingi Mhe. Naibu Spika, nilianza ku-*freeze* mimi mwenyewe kwanza. Nikasema labda kuna *technician* nyengine ya babu kubwa, kwenye buku kuu humu mna pesa nyingi sana ya mafriji haya, sasa sijui Mheshimiwa wangu waziri atakuja kunieleza vipi au la fungu hilo tuje kuliondoa kama tulivyoondoa mengine jana? Atakuja kutueleza vizuri kama yeye mtaalam wa kuzungumza basi tunaomba ajitayarishe atuondoshee mafriji tena high cost na wakati huku tuna upungufu wa matatizo ya fedha.

Sasa ninaingia ukurasa wa tatu Mhe. Naibu Spika, katika majukumu ya Ofisi yenyewe sasa ya utumishi ndio maana nikasema utawala bora wenyewe ndio huu hapa. Mheshimiwa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora una jukumu la kusimamia utendaji watumishi na umma ili waweze kuwahudumia wananchi wa kiwango cha juu cha ufanisi na uimarishaji wa kiwango bora nchini katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa hapa pana walakin, tafsiri nimesema zamani inaeleweka, lakini twende katika utendaji wenyewe Mheshimiwa hauridhishi. Mheshimiwa wangu mimi siku zote humwambia mimi hapa na mara nyingi sana hunambia sikubaliani nalo Mhe. Mshimba ninamshukuru kwa hilo hunambia sana kwamba sikubaliani nalo lakini hajui kwamba na yeye anadanganywa kwa sababu Wizara zipo nyingi. Sasa na wizara zikiwa nyingi mambo mengine mimi anikubalie waziri mambo mengine yatampenya tu. Katika utendaji Mheshimiwa katika watu ubinafsi umo hili tukubaliane na wewe ukubali. Kuna watu wana choyo hataki mwenzake apate, hataki mwenzake walingane lazima utapigwa changa la macho huna vya kufanya lazima utapigwa changa la macho hili ulikubali tu. Sasa naendelea na safari zangu utaona jinsi gani unavyopigwa changa la macho na utaniamini, nitapokuuliza maswali baadhi ya maneno mengine utakubaliana na mimi.

Lakini twende zetu katika hichi kipengele cha tisa kinazungumza hivi, ili ufanikishe majukumu hayo Ofisi itafuata kikamilifu muongozo wa katiba. Sasa hapa katika inasema, itakayosimamia vyema sera sheria za nchi na kanuni zake na miongozo ya matokeo mbali mbali. Mheshimiwa tuna katiba yetu ya Zanzibar kweli lakini kama kweli tunafuata katiba, Mheshimiwa mimi nina wasiwasi mmoja na hili Mwanasheria ninamuomba aje kunisaidia. Kuna Tume ya Mahkama sasa sijui tafsiri inakuwaje au hizi lugha zinakuwaje, kuna kipengele 102 kutakuwa na Tume ya Mahkama lakini tunaambiwa kikiwemo kwenye katiba kinakuwa tayari na nguvu zake.

Lakini kwa Tume hii kwa mtazamo sasa hivi inavyoendeshwa kuna huku kwenye Utumishi ndio wanaowaendeshea wale, wanavyosema katika upandaji wake wa kada za mishahara na ndio maana utakuta kuna matatizo kati ya *difference* zake mimi ninashindwa kufaham, kwa sababu juzi moja nilisema Mhe. Abubakar hayupo, alisema yeye aliliona na atalifatilia sijui atakuja kunipa jibu gani wakati wa Wizara yake. Kweli kuna hawa mahakimu wa mwanzo lakini hakimu wa mwanzo tayari yule ana diploma. Sasa mimi hujiuliza je wanapewa kutokana na level ile ya ujaji ya kuwa mahakimu wa mwanzo anapewa kiasi kadhaa au wa Wilaya anapewa kiasi kadhaaau anapewa kutokana na ile *qualification* yake aliyofikia. Na ndio maana nikawa mchanganyiko kwa hapa ndio maana katiba nikasema mwanasheria wangu naomba ukija unitulizie unifahamishe vizuri nikufaham. Ndio maana ninakaona mkorogo wenyewe uko hapa.

Kwa sababu angepanga mwenyewe huyu Tume ya Utumishi tungeipa fursa ile ya mwenye mahkama basi angepanga vizuri kwa sababu hata mle wale makarani wana difference ya mishahara vile vile na karani mwengine katika level ya juu wa mahkama nyengine ana mshahara wake. Hata hawa maseketari vile vile naomba Mheshimiwa wangu hili hebu tuliangalie kwa makini, ili tusiharibu katika yetu basi ituongoze kama inavyotuongoza hali halisi ilivyo, naomba sana Mheshimiwa hilo na wewe umesema hatutoweza kuingilia muhimili mwengine, tuifanye kazi hiyo ili kunusuru kwa sababu mahakama ni kitu ambacho muhimu sana. Wizara ya Afya ni kitu muhimu sana sasa vitu kama Mheshimiwa wangu inatubidi lazima tuweze kuvisimamia tusione ubahili.

Mheshimiwa kwa mfano viwango vya mishahara katika hospitali na hasa hawa wazee wangu ma-*orderly* wallahi kwa kweli nao hawa hatuwatendei haki. Ma-*orderly* walitaka kusoma katika kipindi cha nyuma miaka iliyopita lakini yakatokea mambo wakawa wasisomeshwe tukawaminya wale, sasa hivi je tunawaweka *level* gani na wa ni watendaji kama manesi kama madokta. Maana yake Mwenyezi Mungu alivyowapa *power* au alivyowapa akili wale first aid ya mwanzo wanaanza kutibu wao kabla nesi kufika au *doctor* mwenyewe au *specialist* kufika.

Sasa hebu tuangalieni hawa mazingira tunawaweka wapi, katika hii Idara hii kifungu cha 19 Idara ya Miundo ya Taasisi Maslahi ya Watumishi, tuangalieni madereva wetu nao halikadhalika na wao hawakusoma lakini wana muda mrefu katika kazi zao hasa wanaokundesheeni nyinyi mawaziri na wao tunawaweka level gani jamani. Ikiwa tunawaangalia level ya *form four* kwenda juu hawa it means watakuwa hawana maana yake hiyo. Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri tusiwaangalie wasomi tu na hawa na wao wavuja jasho tuwaangalie. Kwa sababu na wao tayari wametumika katika kuligomboa taifa lao, madereva tumewatupa vibaya sana hasa nyinyi mawaziri madereva wenu mmewatupa hamjawasemea hamjawalinda basi mnawatuma tu 24 hours hamuwafikirii angalau na wao wakapandishwa mishahara Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kusema la ukweli maskini ya Mungu hawana pa kwenda shamba lao ndio lile hawana upenzi kusema mimi ninamuendesha Waziri hapana. Sasa nafikiri mimi nalo hili hebu tukae tuwape na wao katika *standard* zao za kuwasaidia mishahara yao.

Mheshimiwa kuna matatizo matatizo ya ajira ya walimu wetu na tena basi nilikuwa nitumie kifungu kila 120 lakini nimeangalia kwanza hapa si pahali pake hapa naanza transit tu ipite ili kukuonesha jinsi gani waziri wangu watu wanavyokupiga chenga ya mwili. Kuna watu wameajiriwa tangu tarehe 2/4/2012 wamelipwa mshahara leo na mshahara wenyewe umelipwa umekatwa haukuwa full. Sasa niulize vocha gani waliyotumia from where Wizara ya Fedha au vocha hiyo imetumiwa wapi, sasa hapo mimi nilikuwa nataka niunde kamati teule lakini nikasema aa hapa nipeleke massage hao walimu wamedai haki zao mwisho wanatishiwa kuwa ukisema tu kudai haki yako kesho utafukuzwa kazi, unyanyasaji huo wa nini tunafanyiana jamani.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengine yanasikitisha mtu haki yake mwenyewe hivi mimi nikisema nikidai haki yangu niambiwe Makame sie nawaseme sie potelea mbali lakini haki yangu nitaidai. Unaambiwa usipoidai haki yako hata kwa Mwenyezi Mungu anakutia katika kosa kwa sababu ni haki yako usijidhulumu, walimu wanadai haki zao katika Wizara husika wanaambiwa wao watafukuzwa kazi, halafu leo wasikimbie nchini wanangoja nini jamani Mwenyezi Mungu katupenda nchi ya Zanzibar sikufichini kusema ukweli lakini nyoka huyo anakuja, sitaki kutoa mfano lakini tizameni jana nani alijua Baraza litakaa asubuhi mpaka jioni nani alitabiria hapa. Sasa leo siku tunawabughudhi iko siku watakuja kugoma hawa inshaalla wasigome lakini watagoma maudhi yamekuwa makubwa. Kwa sababu watadai haki zao tunawadharau lakini kwa nini mimi nashangaa sana wakati mtu ni sheria ni wajibu wake anadai haki yake sisi tunambeza.

Jana wamedai haki zao posho la gari hawana wanachokipata chochote wewe tangu tarehe 2/4/2012 anaajiriwa mtu unakwenda kumlipa fedha leo, unamkusudia nini yule mtu pengine yule mtu kaoa, pengine yule mtu kaolewa pengine yule mtu ana familia nyuma inamngojea ili kwenda kumlishia anashindwa na mtu kasoma sayansi tunayoipigia kelele jamani tutakimbiwa na wataalam, wataalam watatukimibia Zanzibar tena wameshatukimbia mimi nitakupeni mfano mmoja tu nikisema wenyewe wanasema nitasema uongo lakini kweli nitawatolea mfano watu wa hospitali, na wakamtafute dokta wa mifupa yuko wapi mtu anachukua likizo miaka miwili unaye huyo.

Nina orodha iko siku yao nitawatolea orodha yao mpaka manesi sasa hivi fuu wameenda zao tunafanya sitizai tunafanya just joking tu tutaua, tutakosa wataalam wa kutuendeshea nchi yetu tutaua. Mheshimiwa hilo nimesema kuwa nitaendelea kulisema katika Wizara husika na pasipokuwepo na jibu sahihi Mheshimiwa mimi shilingi yangu nitaitoa kabisa kwa sababu tunawatafuta wataalam kumbe tunawabeza kwa makusudi. Tunawacheleweshea kuwalipa mishahara yao asiulize mtu katika mishahara hii watu wanapishana huyu kafika kidogo kasoro shilingi kumi, huyu anafika kasoro shilingi saba maana yake nini munatufanyia na hebu nipe sheria kuna sheria ya kumpa

mtu pesa nusu naomba Mhe. Waziri uje kunijibu ipo sheria hiyo mimi sijaiona kwenye *dictionary* langu sijui mwanasheria kama anayo hiyo atakuja kunambia. Kama ukiajiriwa mwezi wa kwanza upewe pesa nusu labda inawezekana siku hizi mambo yanabadilika sheria kila leo siku hizi zinabadilika, tumeshabadilisha sheria mara ngapi sisi hapa. Inawezekana kwamba tumebadilisha sheria mimi nimelala usingizi lakini sidhani kama kuna sheria hiyo inayoweza kufanya mtu ukiajiriwa tu na ukifika mwezi upewe pesa zako nusu mimi sijaona sheria hiyo. Lakini la kuchekesha yaumu shaka nasikia fedha zile zote zimeingia kutoka Wizara ya Fedha zimekwenda katika Idara husika. Mhe. Naomba hilo nije nipewe jibu zuri sana.

Lakini Mheshimiwa niseme tunapoamua kuwafukuza watu kazi kwanza ujiridhishe na hii imo basi tu wewe utakasirika nyumbani huko ukija pale *one mistake* ya mtu unamfukuza kazi, utasema ile kazi yako. Au utamsingizia kesi maskini ya Mungu ata-*servive* na kesi ile mwisho akishinda sasa kumpa pesa zake kishindo hicho. Wewe uliona vizuri pale ulipomfukuza kazi sasa mrudishie mafao yake unashindwa. Mheshimiwa hilo lipo wimbi kubwa wanafukuzwa watu kazi ovyo ovyo tu. Mimi lile la nyuma silisemi nina jipya, lile la nyuma niseme *alhamdulillahi* nimshukuru Waziri kama kalifikisha kunakotakiwa, au hakulifikisha famanillahi yeye na mungu wake. Lakini kalipokea vizuri na mwanasheria wake, lakini kalipokea vizuri na Mwanasheria wangu wamesema watamsaidia yule kijana ili wamuinue katika maisha yake. Kama hawakumsaidia msahafu upo walokulanao amini wauwogope ule na naamini watafanya hivyo kumsaidia hilo mimi sizungumzi.

Lakini jengine kuna kijana amefukuzwa kazi zamani sana KMKM na nilisema sana na Mheshimiwa wangu alisema hapa Dr. Mwinyi ngoja tukutane yule mtoto anahangaika. Ameandika mabarua amefika kukuletea wewe naukasema sijui hatujaunda hiyo Tume hatujakaa sawa na nini lakini cha kushangaza tume inasema kuwa haipokei kesi za miaka fulani 2007 sheria ya rufaa how many years ina-*expire*. Naomba Mheshimiwa unisaidie, Mhe. Mwanasheria hebu niambie rufaa ina-*take time* kwa muda gani ina-*expire*. Kwa nini msimsikilize nyie msikilizeni mimi sikubaliani na Tume na kifungu hiki mimi ninakizuia.

Hii jeuri mngemsikiliza kwanza ana haki yake na yule binaadamu, Tume unakwenda kujibu na unatoa barua rasmi kumueleza yule mshtakiwa haiwezekani unamwambia haiwezekani. Wewe ungekaa ukamsikiliza ametoa *history* tangu alivyoanza kupita huku kupita huku amefata utaratibu amefika kuomba ule mwenendo wa kesi alivyohukumiwa kule kazini kwao hakupewa ule mwenendo wa kesi halafu leo Tume inakuja inamtupilia mbali hatukubaliani na suala hilo. Mimi sikubali kabisa tena kwa hili ni mkali, ilikuwa niipitishe bajeti hii dede niunge mkono, lakini kwa maovu haya sili dhambi nimeapa kwenye msahafu hata siku moja, lazima watu wapewe haki zao, kila anaedhulumiwa apewe haki yake. Tusione uzuri wa kumfukuza mtu kazi mistake ndogo unafukuza mtu kazi ifatilie ushahidi hebu fuata utaratibu kwani kitu gani. Mwizi hukamatwa *red handed* na kitu lakini sio kuwa una shaka na mimi basi tena kesi zenyewe hazina mpango wowote, hatutaki kesi zisizokuwa na mpango bwana. Lazima Tume iwajibike imwite kijana imsikilize ndio imtie hatiani.

Si yule aliyepita amefukuzwa kazi akenda mahkamani maskini ya mungu ikenda kesi mwisho akashinda akaambiwa arudishwe serikalini, serikali haikuwa na uwezo wa fedha akasema si tatizo nilipeni hicho hicho mlichokuwa nacho. Wallahi kairidhia serikali yake Mhe. Naibu Spika. Na serikali imempokea, yule pale Waziri na Mwanasheria waseme uongo na Waziri asiponijibu hapa kunambia kweli Mhe. Mshimba tumempokea ninazuia kifungu, itakuwa hajanipokea kwa insafu nataka atamke hasa katika hoja yake anambie kweli Mhe. Mshimba huyo mtu wako tumempokea na tumo katika *process* ya kumrudisha hapo mimi nitamuunga mkono. Kwanza mimi natia mkono wangu ndani ya mfuko sikunyooshei kukuunga mkono mpaka uje kunijibu pale kwenye kiriri.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache ninakushukuru sana najali wakati wako usije ukanipiga penelti. Nasema siiungi mkono hii na ninazuia kifungu cha Tume mpaka nipte jibu rasmi la hawa watu. Ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kwa jioni hii ya leo ili kuchangia hotuba hii, kwa kweli kabla sijenda mbali nimpongeze sana Mhe. Waziri alivyosoma na jinsi alivyowasilisha vizuri. Lakini pia jinsi Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki kilivyojipanga maana yake kimejipanga vizuri, kimetoa maelekezo, maelezo ambayo hupati shida. Kwa hivyo niseme kwamba ninampongeza sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake na nina imani kwamba hii wizara anaiweza Mhe. Haji Omar Kheri. Kwa sababu mtu ambaye anajifundisha na akiambiwa anasikia na anafatilia.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa sababu ni miaka mingi zilikuwa zinangezwa ongezwa nyongeza za mshahara. Lakini kwa kweli

Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein amefanya mabadiliko katika mishahara ghafla na kwa Wizara zote hakumega kwamba huyu apate hichi na huyu apate hichi kwa mujibu ambapo kisomo chake na uzoefu wake na nini kafanya kazi miaka mingapi, kwa hivyo nimpongeze sana Mhe. Rais.

Lakini niseme Mhe. Naibu Spika, katika Baraza lako hili tukufu lianze mwaka 1980 kwa kweli sijapata kuona historia kama ya jana, jana ilikuwa ni historia ya pekee kuwa na mabuti sabiini nimshukuru sana aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Ali Mzee alikuwa ana-note kila buti linalokuja yeye ana-note, lakini kwa nini nikasema hivi niwapongeze sana wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwamba wameonesha yale mafunzo wanayoyapata basi wanayafanyia kazi ipasavyo. Nakupongezeni waheshimiwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nije katika ajira, na mimi nathubutu kusema kwamba ajira zinatolewa kwa madhumuni ya kusaidia serikali namna gani uendeshaji wake wa shughuli kila wizara. Lakini nimwambie tu Mhe. Waziri kwa sababu tunapomuelekeza Mhe. Waziri anakubali na anaelekea. Mhe. Waziri wa wizara hii tunakwambia hivi, uwe *very careful* na ajira, kuna upendeleo fulani ndani yake, watoto wa shangazi na mjomba, aliyekuwa mnasema mnataka ma-*PhD* si kweli hamkuwachukua mmekwenda kuchukua watu ata jina lake mtu hajui kuandika. Sasa naogopa kwa sababu nchi hii kwa mtazamo wa sasa wa karne hii ya 21 tunataka twende kwenye sayansi na teknolojia.

Mhe. Naibu Spika, kwenye mambo ya ajira nije tena hapo hapo, kuna malalamiko na hii ni Wizara ya Utawala Bora, kuna malalamiko kule Pemba. Mhe. Hija Hassan Hija jana alizungumza hapa kuna malalamiko kwamba kuna vijana wetu wanajenga taifa kwa nia safi kabisa lakini matokeo yake wanachukuliwa vijana ambao siwo, wengine watoto wetu sifa wanazo hawachukuliwi, wengine watoto wa jirani zetu. Sasa tunapofika wakati kama huu kwa kweli kumnyima haki mtu ambaye ana haki katika nchi yake ni tatizo Mhe. Naibu Spika. Namuomba sana Mhe. Waziri, kwa sababu hii ni bajeti yake ya pili ile ya kwanza ilikuwa haijakaa sawa vizuri, bajeti hii imekaa sawa nakuomba sana kama mnavyosema tutamchukua mfanyakazi kwa mujibu wa *qualification* alizonazo basi naomba mfanye hivyo ili tuweze kujenga mustakabali mzuri.

Mhe. Naibu Spika, kumepandishwa mishahara Mheshimiwa wa Jimbo la Ziwani alizungumza hapa. Lakini Mhe. Naibu Spika, miaka ya nyuma nchi hii ilifanyiwa kazi sana na watu ambao hawana ma *PhD*, hawana *Diploma* ambao ndio waliofanya kazi kuweka *red carpet* kuwawekea hao wenye *PhD* na *Diploma*. Tumewapitisha lakini tunawafanya hawakufanya chochote katika nchi hii. Nitatoa mfano mdogo sana Mhe. Naibu Spika, sisemi kwa kitu cha kubahatisha. Tuseme mfano Shirika la Umeme Pemba.

Shirika la Umeme Pemba lilikuwa na wataalamu kidogo sana wanaoweza kufanya ujuzi ule, lakini watu walikuwa na uzoefu na kama hakupatikana yule mwenye uzoefu basi kitu hakiwi. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na *diploma* na *PhD* wale watu ambao wamesaidia kuiendesha nchi hii mpaka ikafika hapa na wao tuwaangalie kwa jicho la huruma kwenye nyongeza za mishahara, tusiwa-*betray* tukawaona hawana haki kwa sababu kisomo chao ni cha chini. Na mimi nathubutu kusema darasa la nane la zamani ni *PhD* ya sasa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika nilisema hili nilizungumze.

Lakini nije katika nitatoa katiba kidogo hapa, kwa sababu hivi karibuni mwaka 2010 tulibadilisha katiba tukawafanya Wakuu wa Mikoa kwamba wasiwe wanasiasa. Sasa kuna sura ya kumi hapa imeeleza vizuri tutasoma samahani Mhe. Naibu Spika, nitasoma kifugu kidogo cha (4). "Mtu yoyote aliye katika utumishi wa idara maalum haruhusiwi kujishughulisha na mambo ya siasa isipokuwa kupiga kura katika uchaguzi wowote kulingana na masharti ya kifungu cha Nam. 7 cha Katiba".

Sasa suala langu liko hapa, ni kwamba tulikuwa na Wajuu wa Mikoa humu ambao walikuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, siwagusi vikosi kwa sababu vikosi imeshaeleza waziwazi. Lakini namuomba Mhe. Waziri akija hapa katika majumuisho anambie je, hawa Wakuu wa Mikoa wanaruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa na Wakuu wa Wilaya. Kwa sababu kwa mujibu wa katiba tuliyoibadilisha kwamba wasiwe wana siasa na ndio maana hawakuingia safari hii humu katika Baraza lako tukufu. Sasa nitamuomba Mhe. Waziri aje anifafanulie vizuri na anielimishe.

Mhe. Naibu Spika, nitamuomba Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu takwimu zote ziko katika Wizara ya Elimu wale vijana wetu waliomaliza masomo, waliokuwa hawana kazi nafikiri na wizara yake itakuwa wanao, naomba sana Mhe. Waziri, kwa sababu sasa hivi tuna matatizo ya watumishi ambao

kwa ajira kama ulivyosema katika suala lako paliulizwa swali hapa kuhusu habari ya walimu wa sayansi. Sasa nakuomba ushirikiane na Wizara ya Elimu ujue waliosoma *engineer* ni wangapi, waliosomea Wizara ya Afya wangapi na waliokuwa wana sifa za Wizara ya Afya wangapi, sifa ya *engineer* wangapi, ili mnapotaka sio mtafute mtoe matangazo wakati watoto tunawasomesha sisi wenyewe katika nchi hii. Naomba twende katika mambo ya utandawazi ya kujua kila kitu, ukiulizwa hapo Mhe. Waziri watu ambao wamesomea *engineer* wangapi uthubutu kusema mia tatu, sio mpaka tena wende ukawasiliane ufanye nini wakati watoto tunawasomesha wenyewe.

Kwa sababu kuna vijana wetu wengi sana Mhe. Naibu Spika wanazururа ovyo hawana kazi na sifa wanazo za kufanya kazi. Nitoke hap oleo nachangia kidogo kidogo tu. Nitoke hapo nije katika mafunzo.

Tuna vijana wetu wakimaliza kusoma tunawapa mafunzo kuna mafunzo ya udaktari miaka saba mpaka kumi na ngapi sijui, kuna mafunzo ya injinia miaka mingapi, sasa tunaiomba serikali kwa sababu vijana wetu tumewasomesha wenyewe tumepoteza fedha nyingi za serikali hii lakini baadae akishakusafirishwa kwenda nje hawarudi tena kuja kuitumikia serikali yao. Naomba sana Mhe. Waziri sasa kuwe na mikataba maalum ambayo mtu akitaka kwenda kusoma nje ahakikishe anarudi katika nchi yakekuifanyia kazi. Kila mtu ambaye tumemsomesha, tumepata shida, kwa sababu na sisi tunatoka huko, sisi Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukipokea *gross* 134, shilingi 144 mimi nilikuwa napokea mshahara kama ni shida sote tunakula shida lakini unapotakiwa kujenga nchi yako basi usikimbie wakati wa shida, ule shida nchi yako ikuone halafu ikutamanie kitu lakini sio ukimbie.

Mhe. Naibu Spika, uzoefu nimeshalizungumza lakini kubwa nadhani nilizungumza hapa. Mimi jana nilisikitika sana na wala simlaumu Mhe. Saleh Nassor kwa sababu wakati wa kuchangia saa nyengine jazba huwa na ile hisia, sikufikiria kama litatoka tamko kwamba *GNU* mimi niko tayari ivunjwe kwa sababu ya kitu ambacho kwa kweli yeye ni mheshimiwa anataka apewe maelezo arekebishe, mpaka wakulibaliane na yule mhusika. Kwa hivyo basi, naomba sana na naomba hii mara ya pili nilisema katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Waziri wa Utawala Bora mana huu ndio utawala bora ushirikiane na Makamu wa Pili wa Rais mtupe mafunzo maana ya *GNU* ni nini, watu tunatakiwa tuweje. Kuna wengine hawaipendi Mheshimiwa, aliyekuwa haipendi potelea mbali samahani kusema neno hilo, ndio ishakuwa *GNU* wala haifi tena hii labda turudi tena kwa wananchi. Sisi ndio tunaojua dunia wale wengine walikuwa hawajui dunia, hakuna nchi kama kuwa katika hali ya amani na utulivu na usalama.

Kwa hivyo mimi nasema bado ile timu ya Bwana Ali Mzee na timu yake, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ndiye huyo namtaja nay eye atupe mafunzo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tena si mafunzo ya siku moja na wewe mwenyewe uzuri wenyewe Waziri wa Utawala Bora. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naliomba tena hilo tusilidharau ni muhimu sana watu wanabenza humu Serikali ya Umoja wa Kitaifa waliokuwa hawaitakii mema Zanzibar, kweli nakwambia Mhe. Naibu Spika, na wewe mwenyewe Mhe. Naibu ulikuwemo kwa hivyo hio kazi kwako.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nilichangie ni kuhusu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana yule mama, tulimfanyia kazi kubwa sana akinamama waliokuwemo kwenye Baraza la Wawakilishi kuhakikisha yule mama ukaguzi anaupata na tukaomba kwa sababu yeye uwezo anao, lakini la kusikitisha naiomba serikali akileta mambo yake muyachukulie hatua. Kuna madhambi kayaeleza lakini hakuna hatua inayochukuliwa kwa nini. Namueleza Waziri wa Utawala Bora mana kuna siku hapa tutacheza kinyakamsewe, hatutokubali kwa sababu yule mama mumpe zana mumsaidie ili afanye kazi zake vizuri, japo kusoma kwangu kwa chini ya miembe mnam *let down* sijui kwa Kiswahili maana yake nini?

Wajumbe Fulani: Kumuangusha.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mnamuangusha hamumsaidii. Sasa niombe sana Mhe. Naibu Spika, asaidiwe yule mama, yeye anawajibika kuonesha nini, kuonesha njia njema kwake. Naomba sana wamsaidie.

La mwisho katika hiki kitabu chake Mhe. Waziri orodha ya malalamiko yaliyopokelewa na kufanyiwa kazi kwa kipindi cha januari orodha hii ni watu wanaodai haki zao humu, watu moja, mbili, tatu, wengi kidogo mama yangu wee. Kuna Manispaa na hii Manispaa kila pahala imetapakaa jamani, kuna wizara gani sijui, naomba sana tusinyime watu haki zao kwa matakwa yetu binafsi. Jamani tumuogope Mungu, wadhifa huu kama ni waziri kamuamrisha Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein Mungu akuteuwe wewe na mimi mwakilishi kaamrisha Mungu hivyo hivyo, kuna baadhi ya mambo jamani tutakwenda kuulizwa huko akhera tusione leo hapa duniani.

Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu kibaya kama kumdhulumu mtu haki yake, mtu kafanya kazi kwa bidii na miaka yote umemrushia bomu si la ukweli leo halikuonekana kama ni la ukweli umlipe haki yake unamnyanyasa. Mhe. Waziri bajeti hii naiachia lakini bajeti ijayo ushirikiane na kima wizara na Waziri wa Fedha ananisikia huyo hapo yuko chini ya mkono wako wa kushoto. Kwa hivyo naomba sana wale waliodhulumiwa haki zao Mhe. Naibu Spika, wapewe haki zao. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru tena binafsi kwa kunipa fursa hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kusema maneno machache kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wziara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa kuanzia nataka nianze na ukurasa wa tisa.

Ukurasa wa tisa Mhe. Naibu Spika, kuna malengo ya Idara ya Mipango na Sera ambalo naomba nitaje hili moja tu nalinukuu hili. "Kutayarisha Mpango Mkaakati wa Utekelezaji wa Sera ya *E-Government*" wanaita Serikali Mtandao. Huu ni mkakati wa utekelezaji. Mwaka jana kulikuwa na utayarishaji wa sera, mara hii kuna mkakati wa utekelezaji wa sera.

Mhe. Naibu Spika, *E-Government* ni jambo moja muhimu sana katika nchi yetu na kama siku moja Mwenyezi Mungu atatuwezesha kulimudu hili litaturahisishia mambo mengi sana. Lakini nimepata hofu kidogo na naomba nimtanabahishe waziri au niitanabahishe serikali. Nina wasiwasi Wazanzibari wasiopungua asilimia 97 hawajui hata ABC ya kompyuta. Sasa je, serikali au Mhe. Waziri ambaye sasa hivi yuko katika mkakati wa kutekeleza sera ya *E-Government* amejipanga vipi angalau kuwahamasisha Wazanzibari kuanza kuchukua mafunzo kwa wingi ya kompyuta. Kwa sababu mimi sijui *E-Government* ni kitu gani lakini nina wasi wasi kuwa itakuwa inapitia kwenye kompyuta na *internet.* Sasa hiyo ilikuwa natoa kama angalizo tu kwamba kwa huku tunakoelekea kuna umuhimu sasa kwa Wazanzibari wote au angalau kwa kuanzia wale ambao wako kwenye maidara na taasisi za serikali wawe wanapata mafunzo ya kujua namna ya kutumia kompyuta na *internet*.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nataka niende ukurasa wa 22 ambapo pale pana Idara ya Utawama Bora. Idara hii ina kazi kubwa sana ya kufanya katika nchi yetu na ni idara mtambuka. Nadhani idara hii ingepaswa kuwepo katika kila taasisi ya serikali mana utawala bora unatakiwa utekelezwe katika kila taasisi ya umma sasa sijui idara hii ambayo iko kwenye ofisi ya waziri wa utumishi wa umma pekee kama itaweza kumudu kuusambaza utawala bora katika taasisi nyengine za serikali. Lakini moja katika malengo makuu ya idara hii ni kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa tena kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, haki za binadamu ni nyingi sana kwa mfano, haki ya kupata huduma za kijamii, haki ya kupata ulinzi yaani kila raia anapaswa kulindwa yeye pamoja na mali yake, haki ya kuishi, haki ya kupata taarifa na nyengine nyingi. Sasa mimi naomba nigusie kidogo kuhusu haki ya raia kupata ulinzi wa yeye mwenyewe na mali zake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata hofu kidogo, nilipata hofu katika kipengele hiki cha ulinzi wa raia na mali zao. Wahusika wakuu wa kulinda raia na mali zao ni kuanzia vyombo vya ulinzi wakiwemo polisi lakini na Mahkama. Kwa sababu muhalifu anapofanya uhalifu wake unaepaswa kumkamata ni Askari Polisi, siku hizi pengine wanaanzia kwenye Askari Jamii lakini hatimaye watapelekwa polisi na hatimaye watapelekwa mahkamani. Sasa uzoefu mdogo nilionao Mhe. Naibu Spika, nimepata mashaka kidogo kwamba kuna viashiria vya rushwa katika mfumo mzima wa uendeshaji kesi na rushwa ni adui wa haki.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina mifano, kuna wahalifu wanauza bangi na kwa kuwa kuna muuza bangi kuna mhalifu mwengine anayevuta bangi ananunua kwa yule muuza bangi, akishavuta bangi anakwenda kufanya vitendo vyengine vya uhalifu, sasa kesi zote hizi zinapitia polisi zinakwenda mahkamani. Muuza bangi anakamatwa na askari polisi anapelekwa mahkamani na mteja wake naye anakamatwa na askari polisi anapelekwa mahkamani, lakini huyu mvuta bangi akishavuta bangi mara nyengine hufanya uhalifu mwengine huiba, lakini kwa kitendo cha kuiba na yeye hukamatwa akapelekwa mahkamani.

Sasa bahati mbaya iliyopo sikupenda hata kidogo kuzungumzia masuala ya mahkamani kwa sababu mimi naamini ni kwahali kwa kutoa haki, lakini Wallahi utashangaa anayekuja kumkamata muuza bangi ni *RCO* wa Mkoa. Anamkamata anampeleka mahkamani anatoa ushahidi yeye *RCO,* lakini bado mahkama inafika pahala inamuachia yule muhalifu. Sasa mimi nilikuwa naona siku zote mahakimu au majaji watu wao wa karibu sana ni askari polisi na

askari polisi mara nyingi ushahidi wake hauna utata kule mahkamani. Lakini kwa misingi gani muhalifu kama yule anaachiwa.

Mhe. Naibu Spika, hii naona ni *indicator* ya rushwa kwa sababu hata *RCO* akitoa ushahidi mahkamani na usipokubalika mimi sidhani kama kuna ushahidi wa mtu mwengine au ushahidi mwengine wowote utakaokubalika mbele ya hakimu kama huyo. Sasa kinachotokea ni kitu gani? Kuna mambo yanatokea hapa kwa mfano huyo mhalifu anakamatwa mara ya kwanza anapelekwa anaachiwa, anakamatwa mara ya pili anapelekwa anaachiwa, mwisho anatoa jeuri hasa anasema mimi bwana msinikamate bure sifungwi. Sasa na kwa sababu yeye ni chemchem ya kuzalisha uhalifu mwengine ambao unawagusa watu moja kwa moja watu wakichoka kumpeleka mahkamani Mhe. Naibu Spika, watafanya jambo jengine wanaloweza wao wenyewao na ndivyo inavyotokea.
Mara moja nilimwendea *RPC* nikamwambia bwana kijiji fulani simtaji *RPC* wa wapi mwenyewe akinisikia atajua huyo ananitaja mimi, nilimwendea nikamwambia kuna uhalifu unafanywa pahali fulani na nikamfahamisha na mwenyewe akakiri kwamba hili tatizo lipo kweli na nikampa angalizo nikamwambia msipochukua hatua maneno ninayosikia watu wakiyasema hatimaye watahukumia mikono yao kwa sababu watakuwa wamepoteza imani na polisi, wamepoteza imani na mahkama, mwananchi akifika hapo ni pahala pabaya sana.
Mhe. Naibu Spika, kijiji hicho juzi nimepata taarifa yule mhalifu raia wema mimi nawaita raia wema sijui kama watakuwa ni wema kweli au vipi, lakini walikwenda wakamkamata usiku wakampiga sana mpaka jicho lake moja kwa taarifa nilizonazo limepotea. Sasa ndio nikasema hii haki ya ulinzi wa raia na mali zao ni haki muhimu sana na isipofanyiwa kazi itasababisha mambo mengine kwa sababu sasa imempotezea hata haki na nadhani walikuwa wanakusudia kumuuwa yule, lakini zake zingaliko. Jicho hana sasa hivi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kama nilivyosema hii ni idara mtambuka mimi nina hakika mahkama haiku wizarani huku lakini Idara ya Utawala Bora ipo, kwa hivyo ifanye kazi kuwanasihi mahakimu wajitahidi sana wahukumu kwa mujibu wa sheria tamaa nyingi mbaya. Mtu kaiba ng'ombe ushahidi *ready handed* ng'ombe huyu aliyemuiba huyu, mashahidi hawa. Wewe unakwenda kumwambia ushahidi hautoshi.

Kumbe kumuachia, akaibe ng'ombe mwengine akauze ampelekee pesa. Jambo baya sana kabisa. Matokeo yake ni kumpoza atakufa mwisho wake, atauliwa kwa sababu watu hawakubali kila siku kuibiwa ng'ombe wao. Na atakayelaumiwa ni Hakimu aliyemuachia, maana angemfunga, angekaa kule jela akatoka na macho yake yule.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Tume ya Utumishi Serikalini. Hii ipo kwenye ukurasa wa 39. Moja katika majukumu yake tumeambiwa ni kusimamia utaratibu wa ajira serikalini. Lakini kama alivyosema mama yangu pale Mhe. Asha Bakari Makame, kwa kweli utaratibu wa ajira bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu.

Tuna misingi mizuri, sera nzuri, na tunapohubiri tunahubiri vizuri sana, lakini tukija kwenye utekelezaji Mhe. Naibu Spika, sera zetu na kila kitu tunakiacha, tunaangalia zaidi ubinafsi wetu. Ukichungulia kwenye Idara za serikali basi ajira zinazotoka Mhe. Naibu Spika, zinakuwa za upendeleo sana.

Niliwahi kusema juzi moja hapa. Ninadhani ni kutokana na hizi ajira kuwa ni chache zimebanwa sana. Sasa kila mtu anawinda ajira. Kwa hivyo ikitokezea nafasi ya ajira, mara nyingi mtu kwanza hutafuta jamaa zake. Sasa tatizo liliopo katika nchi yetu, hivi ni wangapi ambao wana jamaa wakubwa huko serikalini na kama mtu hana jamaa kigogo, ndio jamani asiajiriwe.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lina utata sana. Nilikuwa naomba sana wakubwa wenzangu wawe waadilifu katika suala hili. Wanapotangaza tunahitaji mtu, kwa sababu wanatangaza, ndio nikasema mitandao yote ni mizuri. Wanatangaza kwa mfano tuna shida ya mtu mwenye sifa hii na hii. Sasa wanajitokeza watu, vijana wapo tele wanapeleka maombi yao, lakini *at the end of the day* anakujia kijana anakwambia bwana zimetakiwa sifa hizi hapa. Mimi kwa mujibu wa vyeti vyangu hivi hizi sifa ninazo, nimeachwa kachukuliwa fulani aliye na kasoro ya sifa hizi, lakini kwa sababu bosi mmoja ni ndugu yake.

Sasa sisi huwa tunawapa moyo ngoja tufuatilie lakini kwa kweli pa kwenda hatuna. Sasa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nilikuwa naomba uwe mkali sana katika hili. Kama mtu ndugu yake ana sifa zile zilizotakiwa basi na amuajiri, lakini jamani hata haya hana huyo mtu hana sifa za kuajiriwa, unamuacha mwenye sifa unamchukua yule kwa nini? Unampa mtu *argument* ya kudai.

Halafu Mhe. Naibu Spika, jambo jengine nataka niishukuru sana serikali, kwanza kwa kuongeza mishahara ya wafanyakazi. Ni jambo zuri sana ambalo kwa kweli wafanyakazi wengi wamepata moyo. Lakini sambamba na hilo kuna ukaguzi wa wafanyakazi umefanyika, ninafikiri miezi mitatu mfululizo hapa nyuma. Wamebaini mambo mengi.

Miongoni mwa mambo waliyobaini kuna watu walighushi elimu zao. Mtu akawa anajitaja ana Diploma kumbe hana Diploma, kafanya mipango yake na Mhasibu na *Cashier* akawa anamlipa mshahara wa Diploma, lakini kumbe hana Diploma yamegunduliwa. Ninapongeza sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo kwamba ninakumbuka sisi tulipokuwa katika utumishi wa umma, mtu anasoma kwa mfano anasoma *form five* au *form six*, halafu anafanya mtihani na wenzake wanamaliza, wengine wanapata vyeti na wengine hawapati vyeti.

Lakini wote serikali inawaajiri. Ikishawaajiri yule aliyekuwa na cheti anakuwa na ngazi yake ya mshahara, ipo juu kidogo na yule *form six* aliyekosa cheti, anaondoka kutoka kwenye mshahara wa *form four* aliyekuwa nao anapanda juu kidogo lakini hamfikii yule aliyekuwa na cheti cha *form six*. Lakini ile elimu yake serikali inaijali, ule muda wake wa kusoma miaka miwili na yeye mwenyewe anapata moyo kwa kusoma. *Infact* anaitumia ile elimu hata kama hakupata cheti, lakini pengine utendaji wake yeye aliyekuwa hana cheti na aliyekuwa na cheti ni sawa sawa. Maana kupata cheti sio kwa sababu unajua sana. Mara nyengine inatokezea bahati tu mtu anafeli, kumbe taaluma yake ni kubwa zaidi kuliko yule aliyepasi.

Sasa kilichofanyika baada ya ukaguzi huu, wale walikuwa wanataka kile cheti binafsi, kama wewe unasema umemaliza Diploma lakini sikupata cheti, wanakurudisha mpaka kule kwenye ngazi uliyotoka, kama ni *form four* au *form six*. Kama mtu kamaliza *form six* lakini hana cheti, wanamrudisha mpaka kwenye *form four* ambapo ndio anacho cheti.

Kwa hivyo kuna watu wamepata *demotion* kweli kweli ya mishahara yao. Kuna mwalimu kanijia analia, mshahara wa mwalimu unaujua vile ulivyo, kakatwa mtu shilingi sabini elfu, pana kitu tena atakachokipata. Pengine hata ule kabla ya nyongeza ya serikali sasa kashuka chini zaidi. Sasa mtu kama huyu unafikiri atafanya nini pale skuli. Hasomeshi tena, atakwenda akibabaisha tu.

Sasa nilikuwa naomba sana hawa watu, hata kama mtu hana cheti lakini *at least* aangaliwe kwa vile alivyo. Hana cheti lakini ile elimu yake isiyokuwa na cheti anaitumia kwa kazi, tusimrudishe nyuma sana.
Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ni muhimu sana, kuna watu kwa kweli hawana elimu. Kwa mfano kazi zao ni nguvu nguvu kama madereva wa magari. Siku nyengine mtu anaendesha gari miaka thalathini iliyopita lakini hata ile *certificate* ya *driving* hana. Lakini uzoefu wake ni mkubwa sana, na anaweza kuendesha vyombo vile vizito vizito kama bulldozer, gari zile za kubebea makontena na vitu vyengine. Lakini ilipokuja nyongeza akadaiwa cheti hana hakuangaliwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninadhani si kumfanyia haki yule. Keshatumia muda mwingi serikalini, taaluma yake ni kubwa sana na pengine dereva huyo ukimkosa bulldozer halina mtu wa kuliendesha. Mtu na *digirii* yake hawezi kwenda kukaa kwenye bulldozer akaendesha bulldozer.

Sasa kwa nini na wale hawaangaliwi. Wananung'unika na wanatung'unikia sisi Wawakilishi. Kwa hivyo sisi wajibu wetu ni kuyasema, mambo kama haya ijapokuwa hawana elimu lakini waangaliwe mchango wao kwa serikali ni mkubwa na tukiwakosa ni pengo kubwa.

Lakini jambo jengine Mhe. Naibu Spika, muda unakwenda. Nimefurahishwa kidogo na kauli ya Mhe. Waziri, kwamba sasa anakusudia kuanzisha mfumo wa kupima utendaji kazi katika taasisi za umma. Mimi ninavyoamini utendaji mzuri wa wafanyakazi ni chachu ya maendeleo katika nchi, na unaweza ukaleta *impact* katika uchumi wa nchi.

Lakini katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika, kuna watu wanajituma hasa, na unajua kuwa huyu anajituma kwa uzalendo, lakini kuna wengine wanakwenda kazini wakiondosha njiani. Kazi mtu anayotakiwa kuifanya kwa siku moja anaweza akachukua wiki hajaimaliza.

Sasa tukifika hapo tusitarajie kabisa kama siku moja tutapiga hatua ya maendeleo. Sasa nilikuwa naomba sana mtu akipewa majukumu, na yale majukumu yanakuwemo ndani ya mkataba wake wa kazi. Basi ni vyema akafanya kazi kwanza halafu ndio akadai haki.

Halafu jambo jengine kuna vijana Mhe. Naibu Spika, ambao ni vijana wetu wasomi anamaliza digirii yake anaomba ajira, anapewa lakini pale taasisi aliyofika wanaomuongoza ni watu ambao hawana digirii. Sasa inamjia kwenye akili kwa kuwa mimi nina digirii lazima taasisi hii niiongoze mimi. Asipopewa wadhifa wa kuongoza inakuwa ni taabu mule kazini.

Fitna na majungu haishi, kila mara kusumbuana. Sasa nilikuwa sana vijana wawe wavumilivu kuna *probation period*, kwanza hadi mtu aangaliwe utendaji wake, nidhamu, juhudi yake ya kazi. Sio ukifika wewe upewe cheo tu, kwa kuwa una elimu na ikionekana utendaji wako ni mzuri basi wangapi mbona wamepata vyeo. Sasa basi wasikimbilie sana kuwa na cheo kwanza mtu huangaliwa kidogo.

Jambo la mwisho Mhe. Naibu Spika, ninataka nizungumze kidogo kuhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ofisi hii Mhe. Naibu Spika, ni nyenzo muhimu katika utawala bora, kwa sababu ukiangalia kazi zake ni kudhibiti matumizi ya serikali.

Sasa tabaan kazi yake ni kupambana na matumizi mabaya ya fedha za umma, ni kazi muhimu sana. Tukifanikiwa hapa basi tunaweza tukajikwamua katika mambo mengi. Lakini sasa ofisi hii inakabiliwa na changamoto nyingi.

Moja ya changamoto, ofisi hii hivi sasa inageuza mfumo wa utendaji wake. Wanatoka kwenda kukagua mahesabu yale ya kawaida na hivi sasa wanakwenda katika *performance auditing*. Sasa *performance auditing* ni mambo ya kitaalamu ni *value for money* hii Mhe. Naibu Spika.

Value for money kama huna watathmini wanaoweza kutathmini viwango vya fedha vilivyotumika na kazi iliyofanywa, basi kwa kweli itakuwa kazi ya *auditor* hapa haiwezi kwenda vizuri.

Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri hili alione. Sasa ili wapatine wataalamu basi lazima kuwe na bajeti maalum ya kumpatia ma-*auditors* wataalamu. Sasa naomba sana hili aliangalie kwa kina.

Lakini jambo jengine ambalo mimi bado ninaliona kama ni changamoto, hata kama sheria ipo ya CAG. Lakini CAG kazi yake ukiangalia imepishana kidogo na kazi ya Baraza la Wawakilishi ya *over site*.

Sasa Baraza la Wawakilishi lina nguvu, maana yake lina nguvu, kwa vile ni muhimili mzima wa dola. Lakini CAG ambaye anafanya kazi ya *over site* kwa upande mmoja, yeye hayupo huru, yupo ndani ya *executive*. Sasa kwa sababu yuko mule, mimi ninahisi kidogo kanyimwa uhuru kidogo wa kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Sasa nilikuwa ninadhani Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika, walikalie kitako hili na wataalamu wake. Kulikuwa kuna haja ya Ofisi ya CAG, ama ichanganywe na Baraza moja kwa moja au iwe ni muhimili mwengine. Lakini isiwekwe chini ya *executive* itakuwa hana uhuru wa kufanya kazi zake vizuri.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia mawili matatu juu ya Wizara hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na mwanana, imepangika, kitabu chake kizuri kuliko vyote vilivyokuja. Lakini ni bajeti ambayo imeelezea malengo ya mwaka uliopita na utekelezaji wake, lakini pia imetueleza na malengo ya mwaka huu 2012 anakusudia kufanya nini. Kwa hivyo ni bajeti ambayo kwa kweli imetimia hasa. Kwa hivyo nikupongeze sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kitabu chake hiki cha sera ya utawala bora, ambacho tumegaiwa na kina lugha mbili. Lugha ya kigeni na lugha ya kwetu, nacho ni kitabu kizuri. Lakini pamoja na uzuri wa kitabu hiki cha sera ya utawala bora, naona haya mambo yamekwenda vizuri lakini ningemshauri Mhe. Waziri,

sera hii ya utawala bora ambayo tayari tumeshapewa, na kwa mujibu wa maelezo yake hatimaye wataandaa sheria inayohusu suala la utawala bora.

Lakini ni vyema na hii si kwa Waziri wa Sheria tu, hata Mawaziri wengine basi Baraza la Wawakilishi ni wadau wakubwa kwa sera zote, kwa sababu sera hii maana yake itakuwa ndio kipimo cha sheria watakazotuletea hapa kwa ajili ya kuzitunga, maana sisi ndio watungaji wa sheria.

Sasa sera ikiwa haikuja hapa *at least* kwa semina tu, tukapata maelekezo basi inaweza kuleta matatizo au inaweza kuwa na *in put* nzuri au haina michango. Kwa hivyo sera yako Mhe. Waziri sera ya utawala bora ni vyema ukawaandalia semina Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili *at least* tukapata mwanga, haidhuru inatakiwa kabla ya utayarishaji wake. Kwa sababu Baraza hili ni wadau wakubwa sana katika jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu sheria Na. 1 ya kuzuia rushwa na kuhujumu uchumi ya mwaka 2012, ambayo tayari imeshapitishwa na Baraza lako Tukufu, na tayari Mhe Rais kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri ameshatia saini yake tokea tarehe 2 Mei, 2012. Sheria ambayo inakusudia kuanzisha taasisi au mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa na kuhujumu uchumi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ni muhimu sana, na hapa ndipo hasa penye ile dhana ya utawala bora. Kwa sababu sote tunafahamu nchi yetu hii imekumbwa na janga kubwa sana la rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo, wizi wa mali za serikali, ukiukwaji wa taratibu za sheria na kanuni ambazo zinapelekea mambo haya mengine ambayo yamejitokeza.

Sasa mimi kwa maoni yangu Mhe. Naibu Spika, naona zoezi hili linakwenda taratibu mno, halilingani na umuhimu wa jambo lenyewe. Kwa sababu taasisi hii tumeipigia kelele kwa muda mrefu sana. Wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanayo taasisi hii ya kupambana na rushwa muda mrefu, yaani TAKUKURU.

Lakini sisi tumekuwa tukisuasua sana. Sasa tumekuwa na mashaka, usuajisuaji huu unatutia mashaka, hata utekelezaji wa majukumu wa hii taasisi unatutia mashaka Mhe. Naibu Spika, na zaidi ukizingatia hata bajeti yake hii imetengewa shilingi milioni mia mbili na ishirini, tunahisi ni ndogo. Kwa sababu taasisi hii inatakiwa iwe ina-*cover* Zanzibar nzima.

Kiwango hiki ambacho tumewapangia hapa tena kwa kuanzia ni kiwango kidogo. Sasa sijui Mhe. Waziri alikuwa na kipimo juu ya kiwango kama hiki na taasisi muhimu kama hii, ambayo inashughulikia na kupambana na rushwa, rushwa ambazo nyengine zinatakiwa kusimamiwa ipasavyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, juu ya suala la muundo wa taasisi na maslahi ya watumishi. Pana kilio hapa kwa wasaidizi wetu hawa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilshi ambao walikuwa bado hawajazingatiwa. Tunashukuru kwa mujibu wa taarifa tulizozipata ni kwamba wizara yako imejaribu kufanya kila inavyowezekana katika bajeti hii wameweza kuzingatiwa na wao, ile tumbaku wataweza kuipata kuanzia mwezi huu. Sasa sijui kama tumbaku ile imezingatia na *arrears* zao ili waende sambamba na watumishi wengine.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, ofisi yetu hii imeanzisha *scheme of service* kwa ajili ya watumishi wake ambapo tunategemea itafanyiwa kazi na ofisi yako. Mimi niombe kwa Mhe. Waziri kwamba suala la *scheme of service* kwa wafanyakazi wa hapa ni muhimu, na wala tusione taabu kuzingatia yale mapendekezo ambayo yamewasilishwa. Kwa sababu ni lazima viwango vya maslahi vya ofisi hii vilingane na ofisi yenyewe. Huwezi ukafananisha ofisi hii na ofisi nyengine ya serikali. Kwa hivyo naomba ofisi yako Mhe. Waziri basi izingatie viwango vilivyopendekezwa na ofisi hii ili ioane na ofisi yenyewe ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, tunaishukuru serikali imetenga fedha kwa wastani wa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kuwafanyia masahihisho wale wafanyakazi, au kwa jina jengine kwa ajili ya kuwapandisha *grade* wale wafanyakazi ambao tunaowazungumza, wafanyakazi wa muda mrefu, elimu zao ni za *form four* lakini wana miaka mingi, ambao wanaonekana hadi leo viwango vyao vya mishahara bado viko chini kulingana na muundo huu ambao hivi sasa munakwenda nao.

Mimi nimeridhika sana na viwango ambavyo vilivyowekwa, lakini naomba ofisi yako hii Mhe. Waziri basi itumie kiwango hiki cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwanufaisha wale ili wapate haki zao. Kwa kweli inakuwa haipendezi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu ilipotembelea katika Karakana ya Matrekta hapo Mbweni, ilikutana na wafanyakazi wa aina hii ambao ni mafundi na wanategemewa, wamesoma pale *trade* Mikunguni *form four*, lakini ana miaka ishirini au thalathini wapo pale, lakini ukiangalia viwango vyao vya mishahara ni vidogo mno.

Kwa hivyo ninaamini marekebisho haya ya *grade* ambayo yatafanywa yatawasaidia sana wafanyakazi wa aina hii. Kwa sababu hawa ni watumishi ambao wana uzoefu mkubwa na kufanya kazi muda mkubwa, lakini inasikitisha kuona bado viwango vyao vya mishahara vinakuwa vidogo, na ukizingatia kwamba hivi sasa wanaelekea kwenye kustaafu.

Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri uwaangalie hawa, uwaangalie kwa jicho la huruma, ili kuona na wao mishahara yao inatononeka, kwa sababu inafika pahala wanashindwa mishahara na watoto wao au wajukuu zao ambao wameanza kazi juzi. Kwa hivyo kiwango hiki kilichotengwa kwa ajili ya hawa wafanyakazi basi kiwanufaishe, ili *at least* wajisikie kwamba ni sehemu ya uhuru wa nchi hii.

Lakini hapo hapo Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika, kuna kilio cha wahasibu. Kuna wahasibu ambao katika marekebisho haya yaliyofanywa viwango vyao vya mishahara vimekuwa ni kidogo mno kulingana na wenziwao. Kuna wahasibu wanapata zaidi ya shilingi milioni moja kwa mwezi, lakini kuna wahasibu wanalipwa mishahara ya shilingi laki mbili kwa mwezi, na wote ni wahasibu na pengine hao waliokuwa wanalipwa viwango vya chini elimu zao ni kubwa zaidi kuliko wale waliokuwa wamepewa viwango vikubwa.

Halafu ukiangalia tofauti ni kubwa mno, na Wizara yako inasimamia utawala bora. Hii dhana ya utawala bora Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika ni pana sana, na kwa kweli una jukumu kubwa sana ulilopewa na Mhe. Rais. Kwa hivyo lazima maofisa wahasibu hawa waangaliwe tuone uwiano kati ya mhasibu na mhasibu. Kwa kweli inasikitisha kwamba wafanyakazi hawa elimu yao inafanana lakini wameachana sana kwa mishahara. Kwa hivyo ofisi yako iangalie jambo hili, ione kwamba wote wanakuwa katika *level* ambazo zinafanana. Haiwezekani mhasibu mmoja anapata shilingi milioni moja, na mhasibu mwengine anapata shilingi laki mbili mshahara na wote ni wahasibu, na wakati mwengine hata huyo wa chini yeye elimu yake ni kubwa kuliko yule aliyepewa shilingi milioni mbili. Kwa hivyo hapa kidogo kipimo kimekosekana.

Jengine Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba safari hii ataajiri wafanyakazi elfu mbili mia tano na hamsini na mbili. Katika kitabu chake ametoa mgao hapa, jinsi gani nafasi hizo zitagaiwa. Tunakupongeza, kwanza kwa kutenga nafasi hizi sio nyingi lakini ni wastani, vijana wetu watapata ajira kwa kiasi fulani.

Lakini ningekuomba sana Mhe. Waziri, kuna eneo moja ulipe kipaumbele, Wizara ya Afya. Bado Wizara ya Afya kuna kilio cha kada moja ambayo wanaita ma-*orderly*. Inaonekana kwa muda mrefu eneo hii halijapata kibali cha ajira, na ma-*orderly* ni wasaidizi wakubwa sana kwa hizi kada nyengine za ma-*nurse* pamoja na madaktari. Kwa hivyo, kuna kilio cha ma-*orderly* ambapo maombi yao yameletwa kwa muda mrefu, lakini inaonekana bado hakujatoka kibali cha kuruhusu. Kwa hivyo, nadhani hawa wanahitaji kupewa kipaumbele, kwa sababu sekta ya afya hii pamoja na kwamba sekta zote ni muhimu, lakini hii ina umuhimu wa aina yake kwa sababu inagusa maisha ya watu moja kwa moja. Kwa hivyo, hili linatakiwa Mhe. Waziri tulipe kipaumbele wakati tutakaporuhusu ajira hasa katika maeneo ya afya. Suala la madaktari hili halina ubishi, lakini hawa ma-*orderly* nao wanahitaji sasa kuangaliwa, kwa sababu ni maombi ambayo yamekuja kwa muda mkubwa, lakini inaonekana bado kibali hakijatolewa.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa upande mmoja niwapongeze sana ofisi hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kufanya ukaguzi au kudhibiti fedha za serikali. Lakini nimekuwa na mashaka juu ya shughuli hii, kimtazamo Mhe. Naibu Spika, utaona wanafanya kazi nzuri, wanachimbua wenyewe wanaziita *query* nyingi. Lakini mbali ya kujirejearejea hizi *query*, lakini utakuta kuna mambo mengine mazito wenzetu wanakuwa hawayaoni, sasa hapo ndipo wanapotupa mashaka.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako hili la Wawakilishi katika kipindi hiki tumeunda tume tatu juu ya ufuatiliaji masuala mbali mbali, lakini tume hizi pamoja na kwamba hazina utaalamu, zimeweza kugundua mambo mengi ambayo

yanakwenda kinyume na taratibu za fedha. Zimegundua fedha nyingi ambazo zinapotea, lakini tunajiuliza huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haya ambayo yanaibuliwa na hizi kamati zetu ambazo zinakwenda na Tume ambazo zinaundwa na Baraza kwa ajili ya kuchunguza jambo fulani, wao wanakuwa hawayaoni. Kwa hivyo, sasa tumeanza kuwa na mashaka, kwamba wanaangalia yale mambo madogo madogo, lakini yale mambo makubwa ambayo yanaweza kuizamisha nchi hii, wanakuwa hawatuletei. *Query* zao zile za mahesabu zilizokuwa hazina stakabadhi sijui shilingi ngapi. Lakini wakati tunaunda tume kwa ajili ya kuchunguza jambo basi tunagundua fedha nyingi, mamilioni ya pesa zinakwenda za serikali, lakini kwenye ripoti zao hatuzioni.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kweli wafanye kazi vizuri na kwa uaminifu, watakapokuwa waaminifu na kufichua yale maovu ya serikali, ndivyo watakavyoweza kuisaidia nchi hii. Vyenginevyo tukiona muhali katika kuchunguza mali za serikali, tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, kuna fedha nyingi sana za umma zinapotea katika Wizara na taasisi za serikali, lakini ripoti zake hapa haziji. Kwa hivyo, wafanye kazi kwa bidii, wasijaribu kufichaficha baadhi ya mambo kisha wakafichua yale mambo madogo madogo, lakini mambo makubwa yapo. Mhe. Naibu Spika, utakapokuja kusikiliza ripoti za kamati mbali mbali katika kikao cha mwezi wa kumi utajua kama mambo yapo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Waziri ametueleza kwamba serikali imeruhusu ajira 240 za walimu, nadhani ndio wale walimu wa sayansi ambapo hata ile idadi ambayo ilikusudiwa haikuweza kutimia. Mimi napenda kumwambia Mhe. Waziri kuwa walimu wa sayansi wapo wengi Wazanzibari, lakini walimu hawa sasa hivi wanahama Zanzibar wanakwenda Tanzania Bara na wanaitana, mwalimu mmoja akifika Bara akipata maslahi mazuri, anampigia simu mwalimu mwenziwe na kumwambia mimi huku nalipwa hivi na hivi wanahama wanakwenda zao Bara. Kwa hivyo, kama hatutobadilisha maslahi ya walimu, watamalizika na kutukimbia. Hao walimu wa sayansi tunaowahitaji watatukimbia na hatuwapati, kwa sababu wakisikia kwamba Bara mwalimu wa sayansi analipwa kiasi fulani, basi hawakai wanaondoka na kwenda zao, huku wewe utatangaza na matokeo yake watakuja walimu hawa hawa wa Art, lakini walimu wa sayansi hawakai wanakwenda zao Tanzania Bara.

Kwa hivyo, mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri hebu jaribu kuweka maslahi mazuri kwa walimu hususan hawa wa sayansi, ili kiwe kivuto, wapate mvuto wa kurudi kwao. Hakuna mtu anayekataa kwao, lakini wanaangalia zaidi maslahi. Kwa hivyo, ukiweka maslahi mazuri kwa walimu hususan wa sayansi, kwa hivyo hata wale waliokuwa Bara watarejea Zanzibar kuja kufanya kazi na ndugu zao.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Waziri amezungumzia suala la vibali vya kuongeza muda, vibali 21. Mimi kidogo sikuelewa hawa wafanyakazi 21 walioongezewa vibali ni wale waliokuwa wameshastaafu wakaongezewa vibali vya muda, au vibali hivi vipi mimi sijaelewa. Lakini pia ameeleza kuna vibali vitano vya ajira ya mikataba. Sijui hivi vibali vitano vya ajira ya mikataba ndio wale waliokuwa wamestaafu wakajazishwa mikataba, kwa kweli hapa Mhe. Waziri tunahitaji ufafanuzi. Kwa sababu inavyoonekana sasa hivi ni kwamba suala la kuwajazisha mikataba wafanyakazi waliostaafu, zoezi lake haliendi vizuri. Pamoja na kwamba Mhe. Waziri wakati tulipokuwa tukipitisha sheria tulimtahadharisha sana na tukamwambia, tunapitisha sheria hii ya kuwaajiri wafanyakazi waliostaafu na wewe ndio dhamana juu ya watu hawa, tukija tukibaini kwamba vigezo havikufuatwa na kigezo kikubwa ni utaalamu, tukija tukiona watu wanajazishwa mikataba, wafanyakazi wa kawaida bila kuzingatia vigezo basi Mhe. Waziri tutakula sahani moja. *(Makofi).*

Lakini Mhe. Naibu Spika, inaonekana zoezi haliendi vizuri, kwa sababu kuna wafanyakazi wamerejeshwa kazini, wamejazishwa mikataba na sio wataalamu. Sasa hivi kuna kichaka kimoja kinatumika cha uzoefu, utaalamu na uzoefu. Inaonekana ile *term* ya uzoefu ndiyo inayotumika, sivyo. Sisi tunataka waajiriwe watu wale wataalamu ambao wanaweza kusaidia katika nchi, na wataalamu katika fani hiyo hawapo na wataalamu hapa waliokuwa wanahitajika wanafahamika. Sasa mtu asiwe mzoefu vipi, keshafanya kazi mpaka kastaafu, kwa hivyo kwa maana hiyo utaajiri wote, kwa sababu mtu aliyefanya kazi mpaka akafika muda wa kustaafu, tayari keshakuwa mzoefu. Sasa kichaka hiki cha uzoefu kinachotumika kitatupeleka pahala pabaya.

Sisi Mhe. Naibu Spika, tunataka waajiriwe watu ambao ni wataalamu na wanahitajika katika eneo hilo. Maeneo mengine basi yatumike kwa ajili ya vijana wetu tunao wasomesha ambao sasa hivi wako wengi wanahitaji kujaza nafasi hizi.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja ya kamati yako, ya kulifanyia kazi suala la wale wafanyakazi wa Idara ya vikosi maalum. Kamisheni hii ya Utumishi wa Umma isimamie tume ya utumishi wa idara maalum juu ya

suala zima la askari wetu katika vikosi. Pamoja na kwamba jana Mhe. Waziri alijibu vizuri, lakini mimi nimepata meseji nyingi kutoka kwa maaskari wa vikosi, na wananiambia hivi hivi Mhe. Waziri kakudanganyeni, pesa tunakatwa, hatulipwi pesa zetu vizuri, meseji zilikuwa zinatiririka kwenye simu zangu. Kumbe na Waheshimiwa Wajumbe wengine simu wamezipata. Wanatuambia hivi hivi Mhe. Waziri kakudanganyeni sio kweli, pesa zinakatwa za *ration* shilingi 35,000/-. Askari anahamishwa hapa kwenda Bara anapewa shilingi 10,000/- na huku anatakiwa akakodi nyumba na mambo mengine. Kwa kweli hawa hatuwafanyii haki. Kwa hivyo, Kamisheni ya Utumishi wa Umma, kwa kuwa yenyewe ndio inayosimamia hizi tume za utumishi zote, basi iangalie tume ya utumishi wa idara maalum, kwa kweli kule hakwendi vizuri, hakuna utaratibu mzuri wa fedha za wapiganaji wetu, mishahara yao haiendi vizuri, kunatumika kamandi tupu kule.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, isipokuwa tu moja aje atupe maelezo katika idara ya utawala na rasilimali watu, juu ya eneo la posho maalum *special allowance*, ambapo kiwango kilichopo ni kikubwa mno, ambapo *special allowance* katika bajeti iliyopita ilikuwa ni milioni 40 na mwaka huu iko milioni 132. Kwa hivyo, tofauti inaonekana ni kubwa mno. Kwa hivyo, tunahitaji maelezo ya kina juu ya ongezeko hili kubwa kiasi hiki, kutoka milioni 40 hadi milioni 132 katika idara ya utumishi na utawala wa rasilimali watu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii.
Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa namna alivyowasilisha na mpangilio wa bajeti yake umepangika vizuri, na hata namna alivyowasilisha, kwa kweli kawasilisha katika namna ambavyo inatuwia rahisi Waheshimiwa Wajumbe katika kufanya uchambuzi wa bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii aliyokabidhiwa Mhe. Haji Omar Kheri ukiiangalia ni wizara ndogo, lakini imebeba mambo makubwa. Kwa sababu kama jina lilivyo ni Wizara inayohusiana na utumishi wa umma pamoja na utawala bora. Mhe. Naibu Spika, ni dhana ambayo ni pana sana, na msingi wake hasa maana ya utawala bora ni kuwaridhisha wananchi, msingi wake kwa kweli ni kutoa huduma zinazowaridhisha wananchi, kwa hiyo hiyo ndio maana ya utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, utendaji wote wa serikali kuanzia serikali kuu hadi serikali za mitaa, utendaji wake unajumuishwa na Wizara hii. Watendaji wanapofanya kazi vizuri na hatimaye wananchi wakaridhika ndipo pale tunaposema kwamba nchi yetu inaongozwa chini ya msingi ya utawala bora. Kama ilivyo kawaida kwamba kila penye mkusanyiko wa watu huwa kunahitaji kiongozi. Pia ni hivyo hivyo hata kwenye serikali inaonekana ni lazima kuwe na wizara inayoongoza. Kwa hivyo, ukiachia mbali wizara zile za viongozi wetu wakuu, inaonekana kwa umuhimu na jukumu la wizara hii, basi wizara hii inabeba jukumu kubwa sana la kuzikusanya wizara zote.
Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe pendekezo, kwa sababu kipimo cha utawala bora ni kigumu sana kupatikana, unaposema unataka kupima utawala bora, kwa sababu utawala bora unaonekana na wananchi. Sasa wapi tutaweza kupata hasa kipimo cha kuweza kujitathmini kwamba mwaka huu tumekwendaje, nadhani ni ngumu sana. Kwa hivyo, naomba nitoe rai kwa serikali, iandae utaratibu maalum kwa kupitia wizara hii, kila mwaka itoe ripoti inayohusiana na utendaji wa serikali katika mwaka mmoja. Serikali imefanya nini katika wizara zake, serikali imefanya nini katika mikoa yake, na serikali imefanya nini katika ngazi za shehia, hapo tunaweza tukapata utawala bora katika nchi yetu, *fomular* watafanya vipi, hilo nawaachia wenyewe. Kama watakwenda kwa wananchi au watakwenda kwenye taasisi hilo nawaachia. Lakini ni muhimu sana tuwe na kama vile tunapata ripoti zile zinazohusiana na haki za binadamu kila mwaka, ndivyo hivyo hivyo tunavyolazimika kupata kipimo kinachoelezea utawala bora, kwa maana hisia za watu katika utawala wao huu wa awamu ya saba, chini ya Wizara hii ya Mhe. Haji Omar Kheri.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba nitoe pendekezo hilo kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kufanya kazi hiyo, kwa sababu wizara yako hii ni wizara mtambuka kwa wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Baada ya pendekezo hilo Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kama nilivyotangulia kueleza kwamba uwepo wa utawala bora, kuna suala zima la uwajibikaji na hususan katika suala zima la kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. Huwezi kuwa na utawala bora kama hakuna nidhamu katika matumizi ya fedha za wananchi, na ndivyo hivyo maana serikali zote katika dunia, pamoja

na serikali yetu ikaanzisha Ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Maana yake kubwa kwa kweli ni kuzichunga fedha za wananchi, ili wajanja walio wachache wasipate fursa ya kuzitumia vibaya kwa maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, tafiti zinaonesha kuwa fedha zinazoidhinishwa katika Mabunge yetu haya, Tanzania mwaka jana walitoa, kwamba asilimia 30 ya fedha zinazoidhinishwa takriban hazifiki kulikokusudiwa. Ama zinachotwa fedha hizo, au matumizi yake hayalingani na kile kitu ambacho kimekusudiwa. Wataalamu walisema ni asilimia 30. Kwa hivyo, tuangalie asilimia 30 ya fedha zinazoidhinishwa kuwa hazifiki kwa walengwa ambao ni wananchi au kwa huduma ambayo imekusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo, basi tunapaswa kuekeza sana katika kuijenga na kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nchi yoyote iliyokuwa na chombo kama hiki na kikawa kina uwezo mzuri. Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa kamalizia kwa kueleza dosari, lakini mimi nasema pamoja na dosari zote, ni lazima serikali ielekeze macho yake katika kuhakikisha kwamba inaiwezesha ofisi hii kwa gharama yoyote, kwa sababu upande mmoja unapotoa fedha ni lazima upande mwengine serikali ihakikishe kwamba fedha hizo zinafikia katika lengo lililokusudiwa. Vipi itafikiwa ni kwa kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi Mwenyekiti huzungumza kwamba mambo kadhaa ambayo yanahitaji kuyafanyia marekebisho ni pamoja na kujenga maslahi ya watumishi wa ofisi hii. Hawa ndio wanaokwenda kukagua hao wanaotumia. Siku zote husema kwamba mtu mwenye njaa, hawezi akamkagua mtu aliyeshiba yaani mtu tajiri, haliwezekani. Ili upate ukaguzi uliotukuka na ukaguzi wa haki, ni lazima umfanye mkaguzi na yeye awe na uwezo wa kumkagua yule ambaye anahitajika kukaguliwa bila ya kumrubuni na kumuhonga.

Mhe. Naibu Spika, kama vile serikali ilivyofanya katika taasisi nyeti kama vile ZRB, Benki na mwahala mwengine, basi huwafanya watendaji wake kuwawezesha ili wakaondokana na tamaa, na hivyo ndivyo serikali inavyopaswa kuwafanya watendaji wake hawa nao wakaondokana na tamaa, ili kufanya haki na kuwafanyia wananchi kile wanachotarajia. Inasikitisha leo ofisi kama hii muhimu, kuna watendaji kwa kweli utasikia mtu kapewa jina Mkurugenzi. Huyu ni Mkurugenzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini mshahara anaolipwa ni sawa sawa na mfanyakazi mwengine yeyote. Ukurugenzi wake haulingani na kile cheo chake, malipo yanaendana tu na elimu na vitu vyengine ni sawa sawa na watumishi wengine wa umma. Kwa nini? Kwa umuhimu wa ofisi hii Mhe. Naibu Spika, kwa vile kuna Mkurugenzi katika taasisi hii, kwa nini *level* yao haifananishwi sawa sawa na Mkurugenzi mwengine katika taasisi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani wakati umefika Wakurugenzi hawa pamoja na maofisa wengine, kwa umuhimu wa ofisi hii basi wakawekewa maslahi maalum ili kuwafanya wafanye kazi zao vizuri bila ya kurubuniwa na mambo mengine. Kwa hivyo, rai yangu ambayo naendelea kuitoa Mhe. Naibu Spika, ni serikali kuipa umuhimu ofisi hii hasa hasa kwa kuboresha zaidi maslahi ya wafanyakazi, ili waondokane na vishawishi na vitu vyengine vinavyoweza kuwapelekea wakaweza kurubuniwa kwa urahisi na hivyo ripoti za Mdhibiti zikaonekana kuwa ni ripoti za kichekesho tu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina hofu kwamba huenda kuna siku hapa Wajumbe wakaikataa ripoti ya Mdhibiti kama haikuwa na *content* ambazo Wajumbe wanategemea. Kwa hivyo, ili tusifikie huko Mhe. Naibu Spika, napendekeza serikali iliangalie suala hili kwa umakini sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sasa hivi duniani kama alivyosema Waziri katika bajeti yake, tumetokana na ule ukaguzi tuliouzoea, sasa hivi tunaangalia suala zima la ukaguzi yakinifu. Sasa hivi mambo mengi ya malipaji na mambo ya malipo na vitu vyengine vya masuala ya kupokea fedha, huwa yanaendana katika *system* ya kompyuta, ni ulimwengu wa kompyuta. Ndio maana wataalamu hawa wakasema tuwe na *Computerized Auditing.* Siku hizi mambo ya mazingira yanapewa umuhimu mkubwa. Ndio maana wataalamu wakasema kuwe na ukaguzi ambao unazingatia mambo ya mazingira. Kwa vyovyote vile na sisi sio kama kisiwa tu, ni kidunia. Ni lazima tufike pahala tuendane na dunia inavyokwenda. Kwa hivyo, tunahitaji na sisi mara moja kuanzisha ukaguzi huo, bahati nzuri tayari tumeanzisha, lakini tunapaswa sasa tuendeleze kwa nguvu zetu zote, ili dunia isije ikatuacha nyuma katika mambo hayo.

Hoja yangu Mhe. Naibu Spika, katika hili ni kwa nini hivi sasa tuna ukaguzi wa aina hiyo na tunaelekea huko, lakini serikali haikutenga fedha katika bajeti ya maendeleo. Kwa sababu kwa vyovyote vile nilitegemea kwamba ndani ya bajeti hii, katika kuimarisha kuelekea huko tunako kukusudia kutakuwa na fungu maalum linaloweza kuifanya ofisi hii tukaingia katika miradi hiyo muhimu, ili kuufanya ukaguzi ukaendana na wakati. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anielezee kwa nini serikali haikutenga bajeti katika miradi ya maendeleo ya kuimarisha ofisi hii.

Baada ya kuondoka hapa kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, basi nirudie tu yale yaliyozungumzwa na wenzangu kuhusu suala zima la rushwa. Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana serikali kwa kuleta sheria ile na hatimae Baraza hili kupitisha sheria ile ya rushwa na sheria tayari imeshatiwa saini, sasa tunataka kuunda taasisi. Tunataka kuunda taasisi ya Tume ya Kupambana na Rushwa, niungane na wenzangu wote waliozungumza kwamba fedha zilizotengwa hizi ni fedha kidogo sana kwa ajili ya kuanzisha taasisi hii muhimu. Wasiwasi unakuja pale pale, kwamba tusijekuwa tumeanzisha taasisi ya kupambana na rushwa, baadae kwa kukosa fedha nayo ikaja ikawa ndio taasisi ya kuomba rushwa. Tukifikia hapo Mhe. Naibu Spika, itakuwa tumerudi hatua kumi nyuma.

Kwa hivyo, mimi niungane na wenzangu kwamba fedha zilizoainishwa kwa ajili ya uanzishwaji ofisi hii ya 220 ni fedha kidogo sana, hasa kwa vile huku sijui zilipangwa pesa kidogo sana kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi. Katika hilo naomba nimuulize Mhe. Waziri, inapoanzishwa ofisi hii inatarajiwa kuwa na wafanyakazi wangapi ambao wamepangiwa kutumia mishahara yao ya shilingi milioni 8,988,000/- kwa mwaka, hawa wataajiriwa ni watumishi wangapi katika taasisi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hoja hii kwa kusisitiza kwamba sheria ya maadili ya viongozi, tunaomba iwasilishwe Barazani haraka. Kwa sababu pasi na kuwa na sheria ya maadili ya viongozi, mara nyingi sana tunaoharibu ni sisi viongozi na tunaokula rushwa ni sisi viongozi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ili kuwepo kwa Tume ya rushwa kuwe na maana kamili, ni lazima sheria inayohusiana na maadili ya viongozi iwasilishwe Barazani haraka sana. Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo sasa naomba nielekee kwenye Tume ya Utumishi. Niungane na wenzangu wote walioonesha wasiwasi wao juu ya kuongeza vibali, pamoja na kutoa nyongeza kwa watumishi na vibali vitano kwa ajili ya ajira ya mkataba.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba hizi habari za kuwaongezea watumishi ambao wameshamaliza muda wao, sasa hivi sisi hatuzitaki. Kwa sababu tunachoamini kwamba kila mwaka tunazalisha vijana wengi wasomi, vijana wetu wanapinda mgongo kwa ajili ya kusoma. Kwa msingi huo wanapomaliza kusoma ni matarajio yetu wakamate nafasi ambazo wazee wao wameziacha. Leo kurudia tena kuwaongezea mikataba, kwa kweli ni kuwafanya vijana wale waliosoma wavunjike moyo, na ikifika katika hatua hiyo basi elimu katika nchi yetu itakuwa haina maana yoyote. Watu wote wataona basi ni afadhali waje kwenye siasa huku tupigane vikumbo.

Mhe. Naibu Spika, suala tunalozungumzia pamoja na mambo mengine, Baraza hili lina hamu sana ya kupunguza matumizi ya serikali kama vile tulivyozungumza katika bajeti ya serikali. Kuna kadhia hii ya posho mbali mbali zinazotolewa, na hasa naomba nizungumzie posho maalum kwa ajili ya mafuta. Wakubwa wa nchi hii ambao hupewa posho hizi kwa mahesabu yangu mimi ni karibuni 350, wakubwa hao mbali mbali ambao hufaidi posho hizi tofauti za mafuta pamoja na vitu vyengine. Mdogo wao hupewa lita 15 kwa siku, huyo ndio mdogo kwa siku tu hiyo, kwa mwezi sijui inakuwa ni kiasi gani na kwa hesabu yake sijui kwa lita 15 kwa siku kwa mwezi kiasi gani fedha zake mtazijua.

Lakini kinachosikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba baada ya wakubwa hao kupewa posho za mafuta, hurudi mawizarani kwao wakaenda kuchukua mafuta ya mawizara. Mhe. Naibu Spika, naomba nirudie hili, wakubwa hawa hupewa posho na hilo posho ni fedha kwa ajili ya mafuta na wanapopewa fedha zile, badala ya kutumia kwa ajili ya mafuta, wao hurudi maofisini kwao na maidarani kwao kwenda kuchukua mafuta. Mhe. Naibu Spika, mafuta yale tuliyoyaidhinisha humu kama vile kuna mafuta ya *petrol*, *diesel*, vilainishaji pamoja na vitu vyengine.

Mhe. Naibu Spika, hapa ukifanya tathmini utaona ni kiasi gani gharama zinavyoongezeka. Suala hili mimi mwenyewe binafsi nimeshalifanyia utafiti, na ninayo orodha mkubwa kwa mwezi mpaka kwa miezi sita, na wakubwa wanaohusika, kwamba mkubwa huyu amekwenda ofisini leo, kesho na kesho kutwa amechukua lita ngapi. Vile vile tunapofuatilia upande mwengine tunaona zile posho wanazopewa kwa ajili ya mafuta. *(Makofi)*

Sasa mimi nitakuwa mgumu Mhe. Naibu Spika kwa kulipitisha fungu hili la mafuta. Kwa kweli sitaki niseme kwamba yaliyopita, isipokuwa nataka niseme tu Mhe. Waziri atakapokuja atoe kauli kwamba ama wakubwa hawa nasema ni wengi zaidi ya 350, wakubwa hawa wakubali kuchukua fedha za posho na posho wanazopewa kwa ajili ya mafuta wanunue mafatu au waache posho, ili waende wakachukue mafuta wizarani au maidarani ama kwenye mashirika yao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atakapokuja suala hili alitolee msimamo wa serikali mambo yako vipi? Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja Mhe. Waziri atoe kauli kwamba tufanye nini katika hili au msimamo wa serikali ni upi, kwa sababu vyenginevyo itabidi nije na orodha, na niseme kwamba huyu amepewa kiasi hiki na ametumia kiasi hiki, na hapa amekwenda kuchukua mafuta lita 200 au 300 kwa mwezi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, suala jengine la mwisho kwa kuheshimu muda wako, naomba niseme kwamba nipatiwe ufafanuzi katika haya ambayo nitaeleza.

Kwanza naomba nikumbushe watendaji wote kwamba kuna Sheria ya Manunuzi inayosema kwamba, matumizi ya kila mwaka Afisa Mhasibu hutakiwa aweke *Procurement Plan,* na hayo ni matakwa ya kisheria kwa kila taasisi. Mategemeo yangu kwamba haya tuliyoyafanyia makisio yametokana na *Procurement Plan* zilizomo katika taasisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo maana yake Kamati zetu baadae zitatoka na kwenda kuangalia Mpango wa Manunuzi (*Procurement Plan*) na kulinganisha na hiki ambacho kimeletwa, tukikuta kuna kasoro maana yake ama itakuwa watendaji hawakufanya wajibu wao au Wizara ya Fedha imetudanganya, itakuwa wamekiuka sheria. *(Makofi)*

Katika hilo naomba niseme kwamba Mhe. Waziri atakapokuja, kuna hili posho la vikao na kamati. Kwa mfano, Idara ya Utawala Bora kuna posho la vikao na kamati mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 3 mpaka milioni 16, sasa hizi kamati ni kamati gani? Hivi vikao ni vikao gani?

Kwa kweli tunavyoamini katika idara hata kama kuna vikao vya kiutendaji, basi ni vikao vya utendaji, lakini hatuamini kama kuna vikao vya kulipwa posho, pia na kama ni kamati ni kamati zipi, ambazo zimetoka kwenye milioni 3 mpaka milioni 16 zaidi ya mara 4 kutoka mwaka jana na sasa. *(Makofi)*

Vile vile kuna ununuzi wa kanda za kurekodia na santuri he! Hizi santuri zimeshapitwa na wakati sana na sijui kama zipo au hazipo. Lakini hizo kanda zinarikodiwa kitu gani, sehemu za kurekodia sijui na wala si *studio* humu au kama ofisi zetu zimegeuka *studio* sijui. Mhe. Naibu Spika, tunataka maelezo haya kutoka shilingi 360,000/= mpaka shilingi milioni 2,350,000/=. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia naomba ufafanuzi kwenye Idara ya Utawala Bora, kuhusu posho la vikao na kamati kutoka shilingi 200,000/= mwaka jana mpaka shilingi milioni 21 mwaka huu, ambayo 107.

Naomba tena ufafanuzi Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja Mhe. Waziri, kuhusu vyakula na vinywaji kutoka shilingi milioni 3 mpaka shilingi milioni 13 zaidi ya mara 10 kwa mwaka huu. Pia kuna vifaa vya kuandikia (*stationary*) kutoka shilingi 715,000/= mwaka jana mpaka shilingi milioni 9,900,000/= kwa mwaka huu, Mhe. Naibu Spika ni nyingi.

Tukiondoka hapo pia kuna chakula na vinywaji kutoka shilingi milioni 3,900,000/= mwaka jana mpaka shilingi milioni 29,000,000/= kwa mwaka huu. Kwa kweli posho hii inakuwaje kule au kunapikwa ama ni kitu gani? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapo kwenye chakula na vinywaji mwisho kuna vitu viburudishaji. Sasa hapa nazidi kuchanganyikiwa na hivi viburudisho ni vitu gani? Au vile vya *comedy* viburudisho vya 960,000/= kwa mwaka jana mpaka shilingi milioni moja. Mhe. Naibu Spika, ni mengi na kwa kuheshimu muda wako naomba niishie hapo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, nasema kwamba nitaunga mkono iwapo *Alhaqiir* Mhe. Waziri atakapokuja kunipa maelezo ya kina katika hoja nilizozitoa. Nakushuruku Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante na sasa nafasi tunampa Mhe. Suleiman Hemed Khamis, afuatie Mhe. Hamza Hassan Juma na muda ukiwepo amalizie Mhe. Hija Hassan Hija. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu. Vile vile nikushukuru wewe ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kitabu chake, ambacho kimetoa maelekezo pamoja na maelezo ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa ina imani kubwa sana na Ofisi hii ya Mkaguzi Mkuu, kwa sababu kinachotendeka hapa ni suala zima la fedha za serikali, na serikali inamuangalia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ambaye ni mkubwa kabisa jinsi gani fedha za nchi hii kwa njia yoyote ikiwa kwa salama au si kwa salama, ikiwa kwa wizi au ubadhirifu serikali inaiangalia kwa macho mawili.

Lakini ninachotaka kukuzindueni Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba, Ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kazi au majukumu yake makubwa aliyotengewa ni kuleta ufanisi wa shughuli zake alizopangiwa, lazima ufanisi upatikane na wala hakitakiwi chochote zaidi ya ufanisi.

Vile vile ofisi hii inatakiwa kwa namna moja au nyengine jinsi gani rasilimali za umma zinavyopatikana, ni juu yake yeye kutuelezea katika ripoti zake. Kwa maana ya kwamba ni jinsi gani rasilimali za umma zinavyopatikana.

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii pia imepewa majukumu ya kuona namna gani matumizi ya fedha na rasilimali zote zinavyotumika. Kwa hivyo, haya ni majukumu yake Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mambo haya yatasaidia ikiwa yatashughulikiwa sawa sawa kuondosha ubadhirifu wa fedha za umma, rasilimali zote zilizomo ndani ya wizara mbali mbali pamoja na wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma. Haya yote itakuwa ni miongoni mwa majukumu yake.

Lakini katika ripoti yake ambayo tunategemea mara nyingi huwa anaandika, linakosekana suala zima ambalo ndani ya ripoti yake halionekani, ni suala zima la misamaha ya kodi haielezewi.
Mhe. Naibu Spika, ripoti ionekane kwamba suala hili la misamaha ya kodi limo pamoja na maeneo ya uvujaji wa mapato hatuzioni kwenye ripoti. Kwa hivyo, tunahitaji masuala haya mara nyengine wanapoandika ripoti zao tuoneshwe mambo hayo kwenye ripoti hizo.

Katika ripoti hizo pia ioneshe sehemu ambazo mapato yanapatikana, kwani kwenye ripoti zao hawaandiki maeneo ambayo mapato yanapatikana.

Mhe. Naibu Spika, pia tuangalie si peke yao kwamba hawa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ambaye yeye anasimamia fedha za serikali kwa njia yoyote ile ya ubadhirifu au ya wizi, lakini kuna Kamati nyengine ya *PAC*, ambapo tunaipongeza kamati hii kwa majukumu yake makubwa ya kuchunguza na kutoa taarifa zake. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri wanapopata ripoti zao baada ya kukamilika zinaletwa katika Baraza la Wawakilishi kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapitia kwa njia hizo.

Kwa kweli utaona hii *PAC*, ambayo ina majukumu takriban sawa sawa na hii katika shughuli zake, ukilinganisha ripoti zao wao na ripoti ya *PAC* utaona inatoa maelezo ya kina, ya ndani zaidi yenye uchambuzi wa hali ya juu na kuliko ile Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa kama hali ni hiyo, inaonesha kuna mambo yanafichwa na bado hayajatolewa juu, uwazi haujapatikana sawasawa kuliko taarifa wanazozitoa *PAC*.

Kwa hivyo, kama hali ni hiyo, basi ushauri upo. Mhe. Naibu Spika, tunasema kwamba ripoti itolewe bila ya kuficha, upatikane ukweli ndani ya ripoti hiyo na mihali iondoke ya kikazi, kwa sababu tunaona tukilinganisha baina ya

ripoti mbili. Kwa kweli watu wa *PAC* wanakwenda *deep* zaidi katika uchambuzi wao na mambo mengi yanaonekana. Lakini ukija kwenye ripoti zao zinakuwa kama ni ripoti za kawaida (*shallow reports)*, na wala hazifichui mambo.

Sasa tunataka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika shughuli zake mambo yake ayaweke yawe wazi na ukweli, na kila mtu ayaone, yaonekane bayana.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine kwamba Ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuna ripoti ambayo inatakiwa ikamilishwe juu ya marekebisho ya sheria yake kama ofisi ilivyoahidi, ambapo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliahidi kwamba itatayarisha au itakamilisha marekebisho ya sheria katika ofisi hii, ahadi hii bado mpaka leo haijatekelezwa.

Kwa kweli ikiwa akichelewa huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kukamilisha marekebisho ya sheria ina maana atakwenda kinyumenyume na nchi nyengine na ulimwengu na mambo ya sasa, kwa sababu huyu Mdhibiti ni *answerable* kwa mambo mengine, nchi yote inamtizama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa hivyo, kama yeye anakuwa anajificha kwa mambo ya Zanzibar na wala hajitokezi nje kiulimwengu akaonekanwa, kwamba yale wanayofanya nchi za nje katika kazi aliyonayo kama yake yeye, itakuwa bado hajaenda sambamba, tunaweza kutumia neno sambamba.

Kwa maana hiyo, tunamshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awe tayari kwa kutuletea marekebisho ya sheria kama ahadi yake yeye mwenyewe alivyoitoa, ili iweze kulingana na nchi nyengine ulimwenguni.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba bajeti ya Mdhibiti tunasema kwamba ipitiwe na *PAC*, ili waione bajeti yao, kwa sababu hii ni Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika.

Kwa hivyo, tunahisi kwamba jambo la msingi hii Kamati ya *PAC* iweze kuiona ripoti ile, na wakae pahala pamoja waiangalie na baadae iweze kuletwa katika Baraza la Wawakilishi imetimia kwa pande zote mbili, na wala isifanye ripoti peke yake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bila ya *PAC* kuiona ripoti yake na kuzungumza kwa pamoja na kuweza kubainisha matatizo yote, halafu baadae ndio iletwe ripoti ile katika Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kujadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa suala la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nimalizie hapo, na hivi sasa nizungumzie kuhusu Chuo cha Utumishi wa Umma Tunguu. Mhe. Naibu Spika, chuo hiki kina wanafunzi na hao wanafunzi wenyewe ni watumishi wa umma, ambao wengi ni wafanyakazi wa serikali wamepata nafasi ya kuingia kwenye chuo hiki.

Lakini chuo hiki ambacho kinatajwa kwa jina hilo baada ya kuhama katika eneo lake la awali, ilibidi serikali ifanye utaratibu wa kuweza kuwajengea jengo jengine. Mhe. Naibu Spika, tokea kipindi hicho mpaka hii leo jengo ambalo walitegemea wanafunzi, wafanyakazi wa Chuo cha Utumishi wa Umma kuweza kupata mafunzo yao katika chuo hicho kipya, bado mpaka leo chuo hicho hakijaweza kupatikana, hakijamalizika, muda umefika wanafunzi wako tayari.

Mhe. Naibu Spika, mpaka hivi sasa wanafunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma mfano wake ni kama wanafunzi wa wanaosoma *Primary*, kutokana na hali ilivyokuwa ni ngumu na chuo bado kumalizika, imebidi wanafunzi hawa na wafanyakazi wapangishwe kwenye skuli tofauti, ili waweze kupata mafunzo yao na imekuwa mashaka tu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hapo tuone kwa nini hili jengo bado halijamalizika. Mkandarasi ambaye amekabidhiwa ambaye ni KMKM tangu kipindi hicho kuweza kulimaliza jengo lile kwa ajili ya wanafunzi waweze kuhamia kwa wakati uliopangwa imeshindikana, fedha zilizotolewa si kidogo ni nyingi.

Lakini ukitathmini jengo lenyewe na fedha ambazo tayari zimeshatoka hazilingani, tukija kwa wale wataalamu *value for money*, utahisi kwamba fedha nyingi zimepotea kuliko kazi ile ambayo iliyokadiriwa na wala haikufikia kiwango.

Kwa hivyo, hii ni moja katika hasara kubwa sana, kwamba tunakubaliana kwa fedha kiasi kadhaa na wakati fulani fedha zimekwisha au karibu ya kwisha jengo halijamalizika, wanafunzi hawajapata pahala pa kusoma.

Mhe. Naibu Spika, KMKM ameshindwa kukamilisha kazi ile, lakini wizara imeingilia kati kuona ni lazima jengo lile liweze kumalizwa. Kwa hivyo, mkandarasi mwengine ambaye ameingia baada ya hawa KMKM ni Chuo cha Mafunzo wamepewa wao, ili kulimaliza jengo hili kwa fedha ambazo zilizokuwa zimebakia shilingi milioni 300/=.

Waheshimiwa Wajumbe, hii ni kuonesha jinsi gani fedha za serikali zinavyobabaishwa bila ya wakati maalum na bila ya madhumuni ambayo wizara ilikuwa imekusudia. Sasa hawa Chuo cha Mafunzo wamepewa kwa ajili ya kuikamilisha kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sisi kama kamati tumehisi kwamba jengo hili au wanafunzi hawa ama chuo hiki hakikutendewa haki. Kwa kweli inaonesha kwamba baada ya muda mfupi labda baada ya mwezi mmoja au miwili kazi itakuwa imemalizika, na wanafunzi hawa watakwenda katika jengo lao ambalo wamepangiwa.
Lakini sisi hatukuridhika na hayo kwenye hali ya ujenzi huo wa chuo, kwa sababu fedha nyingi zimetumika na lile lengo halikupatikana. Kwa hivyo, tunaiomba wizara iweze kuchukua hatua kwa huyu Mkandarasi wa kwanza ambaye alikabidhiwa jengo na kushindwa kulikamilisha.Kwa hivyo, wanafunzi waliopo ambao wamepangwa katika sehemu mbali mbali wanakwenda katika mafunzo kwa mikondo minne, Mizingani na Skuli ya Sekondari ya Hamamni huko ndio waliko.

Mhe. Naibu Spika, tunasema hali ni ngumu kwa wanafunzi kimasomo na hali ngumu kwa walimu ambao wanatoa mafunzo yale.

Walimu hawa kutokana na kuhangaika na wanafunzi ni wengi ambao wamepangishwa katika maeneo mbali mbali, imebidi walimu wahangaike huku na kule katika kutoa huduma ya elimu. Kutokana na hali hii muda wa wafanyakazi hawa walimu ambao wanaosomesha muda wao wa kazi umepindukia muda wa kawaida, yaani kiwango cha kawaida wanatakiwa masaa 40, lakini walimu hawa wanafanyakazi kwa masaa 55.

Kwa hiyo, hili ni suala ambalo Mhe. Waziri lazima alifikirie jinsi gani walimu hawa katika Chuo hiki cha Utumishi wa Umma wanavyopata tabu, yaani kuhangaika katika kusomesha masomo yao *up and down*. Mhe. Naibu Spika, utaona walimu hawa wanapoteza masaa mengi zaidi kuliko yale ya kawaida.

Jambo jengine ambalo tunaliona Mhe. Naibu Spika, ni kwamba maslahi ya walimu hawa ni madogo ukilinganisha ya walimu au wanafunzi walioko katika vyuo vyengine. Kwa mfano, ukilinganisha Chuo hiki cha Utumishi wa Umma na Chuo cha Habari na Mawasiliano ya Umma Zanzibar au Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, utaona maslahi yao yako tofauti na wala hayalingani na hivi vyote ni vyuo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aangalie maslahi ya walimu hao, kwa sababu ni jambo la msingi tena ni muhimu sana.

Nikiondoka hapo sasa nizungumzie sehemu ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Mhe. Naibu Spika, idara ina jukumu la kutunza na kuhifadhi nyaraka mbali mbali za kitaifa. Kwa kweli hali ambayo tunayoishuhudia katika sehemu hii ya kuhifadhia kumbukumbu, waliopo pale wanajitahidi kuendesha kazi zao vizuri, lakini bado mahitaji ya kuweza kupanua shughuli zao yanahitajika kutokana na ufinyu wa nafasi iliopo.

Vile vile baada ya kuangalia katika Idara hii ya Nyaraka tumegundua kwamba kuna wafanyakazi wanapoteza muda wao mwingi bila ya kupata vifaa vya kufanyia kazi ambavyo ni muhimu. Kwa mfano, baadhi ya nyaraka nyengine zinazokwenda pale huwa ziko katika hali mbaya sana na zinahitaji kuhuishwa, ili angalau ziweze kutumika au kuonekana kile kilichomo katika nyaraka hizo.
Kwa hivyo, kuna dawa maalum ambazo hao maafisa wanahitaji kuzipata dawa hizo ili kuweza kuwasaidia katika kazi zao. Kwa taarifa yako Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi hawa wanaweza kukaa zaidi ya miezi 6 bila ya kazi kutokana na ukosefu wa dawa za kutengenezea karatasi zilizokuwa zimeharibika vibaya.

Mhe. Naibu Spika, suala hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa macho makini, kuona kwamba masuala haya ya masaa ya kazi hayapotei bila ya kazi. Kwa maana hiyo, idara hii imekosa vitendea kazi kama vile dawa za kuhuishia nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Pemba tunashukuru kwamba zinaendelea vizuri na anajitahidi sana katika kazi zake. Vile vile nataka niseme kwamba afisa huyu ambaye amekabidhiwa jengo ambalo lilikuwa la wilaya, anayo kazi kubwa sana ya kulitengeneza jengo lile.

Kwa hivyo, ningemuomba hapa Mhe. Waziri katika ofisi ya Pemba kwa huyu mtendaji ambaye ni mzuri, basi idara hii iwezeshwe vizuri kifedha, kwa sababu jengo lenyewe liko katika hali mbaya na linahitaji marekebisho, ili liweze kukidhi haja au mahitaji ya kuwekea nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nataka nitoe pongezi kwa Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala tunaipongeza idara hii kwamba imekuwa na malengo mazuri ya kuimarisha Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Kwa hivyo, tunaijua hii serikalini au serikali inaelewa kwamba kuna hii *E – Government*, hivyo Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Serikalini. *(Makofi)*

Kwa hivi sasa hatua iliyochukuliwa ni muhimu, kwa sababu ya kutoa nafasi kwa viongozi hii *E – Government* inatoa nafasi kwa viongozi, watumishi wa umma pamoja na wananchi. Kwa hiyo, suala hili litaharakisha maendeleo au mawasiliano pamoja na kupata taarifa mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo iwape fedha hawa kwa ajili ya kukamilisha shughuli zao, kwa sababu gharama ni kubwa na hii ni hali halisi, fedha zitakazoweza kusaidia mradi huu ambao utajumuisha wizara nyingi zitakuwemo kwenye hii *E – Government*. Kwa hivyo, wanahitaji fedha kwa ajili ya kukamilisha mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kwa kupitia Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili idara hii iweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe: Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii jioni hii na mimi nikazungumza machache katika Wizara hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze na nimpe pole Mhe. Waziri kwa majukumu mazito ambayo aliyotwisha na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kuhakikisha anasimamia suala zima la utawala bora katika Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi kama alivyoanza yeye mwenyewe katika hotuba yake nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuweza kukabidhiwa hii jahazi ambayo yeye akiwa ni nahodha mpya kabisa.
Mhe. Naibu Spika, tulipounda mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa tulikuwa peke yetu. Ingawa katika mchakato huko ndani na yeye alishiriki. Lakini katika utekelezaji waliotandika hii *carpet* kwa bahati wamekaa upande, sasa hivi amekabidhiwa yeye majukumu. Tunashukuru kwa kuwa miongoni mwa walioandaa hii *carpet* yupo pembeni yake anamsaidia, naamini jukumu hili litakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba somo la Utawala Bora ni somo kubwa sana. Kwa bahati nzuri mimi Mhe. Spika, aliwahi kunipa nafasi nikapata kuhudhuria katika Mkutano wa Mabunge ya CPA. Moja katika taaluma tuliyoipata kule ni suala zima la Utawala Bora. Kwa bahati nzuri katika mkutano ule wenzetu Bunge la Jamuhuri ya Muungano hawakupata nafasi. Mimi ndiye nilikuwa mwakilishi pekee ambaye niliyepata nafasi ile.
Mhe. Naibu Spika, moja katika kitu ambacho kilichotolewa mfano katika mafunzo yale ilikuwa ni Zanzibar kuingia katika Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mmoja katika miongoni mwa wakufunzi wetu katika mafunzo yale

kwa bahati nzuri alikuja kuwa ni mwangalizi mpaka katika uchaguzi wetu Mkuu. Aliposikia mimi natoka Zanzibar aliniita akanihoji na akanambia kwa kweli hongereni sana lakini bado mnazo changamoto kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kweli changamoto tunayo. Bado elimu ya mfumo wetu tulionao wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hii ni changamoto kubwa. Iko haja kushuka chini watu waende wakafahamishwe kule tulikotoka sasa hivi kule tumeshapiga mstari. Mstari tulionao sasa hivi ni mstari wa kuhakikisha kwamba tunasimamia utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni ilitokezea purukushani kubwa hapa Zanzibar, kila mtu alizungumza maneno yake. Kila mtu alikuwa na mawazo yake, lakini tunamshukuru Mhe. Rais wetu kwa busara zake. Alitulia akaagiza vyombo vyake vya ulinzi kulishughulikia suala lile ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote atakayezikwa katika purukushani ile. Tunashukuru sana, demokrasia kubwa Zanzibar sasa hivi, watu wanasema wanachotaka lakini wanachosisitiza kwamba wasivunje sheria za nchi.

Mhe. Naibu Spika, kuna wengi na kuna mengi, wengine wanamlaumu Mhe. Rais kwa nini hukuchukua hatua hii, kwa nini hujachukua hii. Ndiyo yale tuliyopata katika mafunzo moja katika suala zima la utawala bora tumeambiwa uvumilivu, kuvumiliana. Mtu maoni anayoyatoa yeye kama wewe huyapendi unatakiwa ustahamili, sasa huo ndio utawala bora na hapa kwa kweli kunahitajika elimu kubwa.

Mhe. Naibu Spika, utawala bora umejengwa zaidi mpaka ndani ya Katiba zetu zote mbili ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Ukiangalia kifungu cha 18 kwenye Katiba zote mbili zimetoa uhuru wa wananchi waweze kutoa maoni, waweze kutoa hisia zao kile ambacho weo wanakiamini na wanachokitaka. Mimi nashukuru kwamba hilo linasimamiwa mpaka sasa hivi na serikali yetu bila ya bughudha ya aina yoyote.

Mimi naomba na natoa wito hasa kwa wananchi wa Zanzibar tuitumie fursa hii ya kutoa maoni bila ya kubughudhi mtu, bila ya kumtukana mtu wala bila ya kumnyanyasa mtu yeyote, wala bila ya kuonesheana vidole. Nafikiri sasa hivi tupo kwenye lile daraja la kuvuka kuangalia huu utawala bora tutaufanyia vipi.

Sasa katika utawala bora huu na changamoto zake. Wenzetu kule sisi walivyotusomesha walitwambia katika suala zima la utawala bora zinatakiwa haki za binaadamu kwa wananchi wote, kuanzia maskulini, wafundishwe somo la haki za binaadamu lakini vile vile somo la uraia. Mtu akisoma somo la uraia na haki za binaadamu basi huko mbele anapokwenda ataweza kuwa mvumilivu katika hali yoyote itakayoweza kujitokeza.

Sasa wenzetu kule katika sheria zao, hapa sijui labda Mhe. Waziri utakapokuja unifahamishe. Mimi nilisoma *western*, huku hatuko *western* wala *eastern* sisi tuko katika *middle*, *m*aana yake sisi siasa zetu hatukufungamana na upande wowote, lakini sisi bado tunafuata Mabunge ya Jumuia ya Madola.
Wenzetu kule kunasheria za migomo katika Utumishi wa Umma na taratibu zake, sasa hebu huku kwetu tufahamishwe. Kwa sababu Waswahili wanasema ukisikia nyoka huyo, hadithi za zamani unaambiwa na apite, sasa hivi nyoka yupo Dar-es-Salaam, kuna mgomo wa madaktari. Juzi hapa Mheshimiwa uliulizwa swali hapa, ukasema mgomo wa madaktari hakuna. Lakini nataka nikuthibitishie Mheshimiwa nusa nusa, Mheshimiwa wewe ni msikivu sana mimi nakujua, nusa nusa, baridi ulikuwepo, nusa nusa. Hili nakupa la kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema je, katika sheria zetu za Utumishi wa Umma kuna kitu kama hicho kimetolewa muongozo. Kama kumetolewa muongozo basi ni lazima ujulikane. Hatutaki tuje tusikie wagonjwa wetu wanaanza kupata matatizo kama wanavyopata wenzetu upande wa pili. Hili kama utaweza kulijibu sawa lakini naomba ulifuatilie zaidi, lakini kulikuwa kuna harufu harufu. Mimi siku hiyo ambayo nilipata hiyo harufu nikampigia Mhe. Jaku kwa sababu yeye ndiye Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya. Nikamwambia Mzee hebu fuatilia kidogo kuna mama katoka kenda Mnazi Mmoja, sijui kenda wapi mwisho nikamwambia nenda Kwamtipura hakuna mgomo. Mhe. Jaku, alikuwa ana shughuli zake muhimu, akafatilia akanambia duu, harufu ipo. Ndio maana nikakwambia Mheshimiwa sisi ndio wasemaji wa wananchi. Mwananchi keshakwenda hapa anaambiwa daktari anahivi, kenda hapa daktari ana hivi. Sasa hii isije kutufikisha pahala pabaya.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala jengine linahusiana na sheria zetu. Katika hii sheria ambayo inayoruhusu watu kufanya maandamano, tunaomba uje ututolee ufafanuzi mzuri wa maandamano. Maandamano yanatakiwa vipi, sheria iko vipi juu ya hili. Ili hawa wanzetu tupate kuwaelimisha vizuri ili tusije tukaharibikiwa huko mbele. Hizi nilikuwa nazungumza hizi changamoto.

Jengine kubwa linapokuja suala la *transparence*. Moja katika kitu walichotueleza kwamba nchi zenu za Kiafrika mnapata tabu sana kwa sababu hampo wawazi, mambo yenu mengi mnayaficha ficha. Mhe. Naibu Spika, suala zima la *transparence* hapa juzi rafiki yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, swahibu wangu, mimi nikiwa kama Mwenyekiti wake wa Kamati ya Wenye Viti, tulipokuwa tunazungumzia Bajeti Kuu ya Serikali. Tukamuhoji mambo mengi, lakini tulipokuja Barazani kuna Waheshimiwa fulani waliuliza kuhusu fedha za Rada. Je, Zanzibar kwa kuwa ile Rada ni masuala ya Muungano sisi tutafaidika vipi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Fedha alitujibu vizuri, akasema kaja Mhe. Mgimwa, Waziri wa Fedha wa Muungano, wamezungumza wakakubaliana wakasema kwamba ataangalia uwezekano wa kupatikana hizo pesa. Mimi ninavyojua Waziri wa Fedha wa Jamuhuri ya Muungano pamoja na kwamba yeye ndiyo msimamizi wa fedha za Muungano lakini hawezi kufanya jambo lolote bila ya kupata idhini ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
Cha kushangaza na cha kusikitisha juzi nilikuwa naangalia Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Waziri Mkuu ametamka wazi wazi kwamba fedha zile, ingawa mambo ya Rada, mambo ya Mawasiliano ni mambo ya Muungano, lakini fedha zile hazikutolewa na Wizara ya Ulinzi. Fedha zile zimetolewa na Wizara ya Miundombinu ambayo sio Wizara ya Muungano, Zanzibar hatuwezi kupata fedha zile. Nilisikitika, ingawa Mhe. Omar Yussuf Mzee anazungumza sasa hivi. Hebu na alifanyie kazi, awasiliane na Mhe. Mgimwa kama ile kauli aliyomwambia ya fedha za Rada tutazipata lakini Waziri Mkuu anasema hatuwezi tukazipata kwa sababu zimetoka katika Wizara ya Miundo Mbinu na Miundombinu sio miongoni wa Wizara za Muungano, basi angalau mtusaidie kuweza kujua ukweli. Hili tena naomba sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hebu watusaidie wenzetu mawaziri wa upande wa pili wa muungano.

Kuna picha moja katika gazeti kuna katuni mmoja yeye anasukuma gurudumu yeye yupo chini kuna wenzake wengine wapo juu wanalivuta. Sasa hivi Mheshimiwa tukitaka, tusitake Zanzibar tuna changamoto kubwa katika suala zima la muungano. Sisi tunajitahidi kujenga hoja za kuimarisha muungano. Mambo kama haya ikiwa Waziri wetu wa Zanzibar anasema tunategemea tutapata hichi. Anatokea Waziri wa pili wa Muungano anasema hichi hamkipati. Mimi nadhani hili gurudumu linaonesha kama wengine wanatuachia lituelemee.

Mhe. Naibu Spika, hapa tuna kazi kubwa, tunaomba sana Mawaziri wetu mnapokwenda katika vikao hivi, lakini vile vile yale mazungumzo mnayozungumza basi bora ziwe kauli mnazotupa hapa ziwe za matumaini ya uhakika. Isijekuwa kama ile kauli ya mwaka jana tukaambiwa TRA katika Bajeti yao bilioni 15 tutazipata matokeo yake mwaka huu Mhe. Waziri anatwambia samahani sana fedha zile nasikitika hatukuzipata. Sisi tunasukuma gurudumu la Muungano ili uimarike, lakini wenzetu wanaliachia. Sisi tunataka walivute wao wako juu sisi tupo chini tunasukuma, wakiliachia watatuuwa.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika suala zima la utawala bora. Tunakushukuru sana kwa kushirikiana na Spika kutupatia mafunzo. Ndio maana leo imekuwa kama hadithi ya jogoo kuona mwezi. Sasa hivi kila anayekuja sasa hivi anaanza kuhoji mafungu haya TV, viburudishaji, sijui nini, haya ndiyo yale mafunzo uliyotupa kwa muda wa siku mbili. Tumekwenda ukatufungia shamba, ukatwambia sasa hivi tunakufundisheni namna ya kuchambua bajeti. Haya ndiyo matunda yake. Wenzetu wasije wakashtuka mbona hawa sasa hivi wanaona mbali, tumeoneshwa ndio maana tukawa tunahoji.

Hapa katika suala zima katika mafunzo tuliyoyapata, moja tulichotakiwa tukiangalie katika bajeti na hili pia tuliomba. Serikali yetu, mwakani katika bajeti unapofika ule mwezi wa April basi angalau zile Kamati zinazohusika basi zipewe mtizamo wa Mabajeti ya Serikali yale malengo, kuangalia vile vipaumbele. Tulivyoambiwa kuna mambo kama manne tunatakiwa tuyaangalie tunapopitisha bajeti.

- Tunaangalia MDG *(Millennium Development Goals)*

- Tunaangalia Vision 2020

- Tunaangalia MKUZA

- Tunaangalia sasa hivi tuna MKUZA II katika huo utekelezaji lakini vile vile tunakwenda katika MTF.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia sasa hivi tunaanza kuona ni maeneo mengi ambayo tukiyafanyia kazi vizuri tunaweza tukaokoa fedha nyingi za serikali ambazo zitaweza ku- *cover* hasa katika yale maeneo mengine muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba nizungumze na Mhe. Waziri wa Fedha katika bajeti ya mwakani, katika kuweka hasa ule Utawala Bora. Kuna maeneo kidogo tunahisi hatwendi vizuri. Kuna mchanganyiko kidogo wa matumizi ya fedha *double*, matumizi ya ndani ya Baraza la Wawakilishi na ndani ya serikali. Tulikuwa tunaomba Mhe. Waziri wa Fedha ingawa katika ile sheria tunayosema tumeshaleta Mswada Barazani.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Spika, katoa muongozo tunaufuata na kwa kuwa Waziri wa Fedha nadhani tutakuwa pamoja katika kufanya hiyo *study* basi tuanze kuchanganya zile posho za wale wafanyakazi wanasiasa ambao vile vile ni wa serikali. Sitaki niwataje ni wa aina gani kwa sababu haya ni mambo ya mabunge na serikali. Tuangalie namna gani ile *package* yao kuiweka pamoja, isiwe kule inakwenda hivi na huku inakwenda hivi. Mfano mzuri hata Bunge la Jamuhuri ya Muungano wanafanya. Hilo nalizungumza ndani ya mabano kwa sababu mambo maalumu. Mhe. Waziri katikisa kichwa, kwa hiyo kanifahamu.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, hapa leo nilikuwa nipige buti. Lakini hata nikipiga buti itasaidia nini, nitaumiza kiatu changu bure kinaweza kikachanika, tuna tatizo la Katiba, Mhe. Naibu Spika, tumeshakuletea hoja yetu ya kufanya marekebisho ya Katiba kwa sababu kila tunavyofanya kazi zetu na mafunzo tunayoyapata kuna baadhi ya *arrears* tunakwama kutokana na utata wa Katiba.

Tunaomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria upo, Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma upo, tuangalie namna gani ya kuweza kurekebisha hasa hii sheria yetu ya Utumishi wa Umma kuiachia hizi Tume zikawa zinajitegemea moja kwa moja. Tuna *Separation of Power*, tuna Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Utumishi ya Baraza, lakini vile vile tuna Tume ya Utumishi ya Vikosi au Idara Maalum. Tunaomba sana maeneo haya bado yana mkangayiko mkanganyiko.

Kwa kuwa tumesema kwamba Katiba yetu imesema tutaheshimu utawala bora, lakini vile vile tutaifuata na Katiba ya Zanzibar. Katiba ya Zanzibar inazungumza katika maeneo ya mwanzo nafikiri kifungu cha 5 sina uhakika vizuri, kinazungumza mgawanyo wa madaraka katika mihimili mitatu. Nilikuwa naomba na hili katika marekebisho ya katiba ni vizuri tukampunguzia baadhi ya majukumu Mhe. Rais.
Mfano kwenye Tume ya Utumishi ya Mahakama tunashukuru inakwenda vizuri, kuna ile Tume ya Majaji inamshauri Mhe. Rais. Lakini Baraza la Wawakilishi inatakiwa Tume ya Utumishi ya Baraza imshauri Mhe. Rais katika uteuzi wa Katibu vile vile. Hii ndio katika kuimarisha utawala bora. Katika eneo hili naweza nikaja nikazuia kifungu. Lakini sio katika yale niliyoyazungumza kwamba yanahusu katiba. Naweza nikaja nikazuia kifungu katika suala zima la muhimili ambao haupati nafasi ya kujitetea. Sisi kwa bahati nzuri serikali ndio nyie mnatusikiliza na mnatujibu. Sisi tunakwambieni nyinyi lakini wenzetu Mahakama hapa hawaji. Kwa hivyo ina maana sisi tunachukua jukumu hili la kuwasemea wao muhimili wetu wa tatu.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mahakimu wa Mahakama za mwanzo, Mheshimiwa kuna tatizo. Tatizo mshahara wao kwa kweli unatia aibu. Hili Mheshimiwa tukitaka tusitake, hawa ndio wanaohukumu zile kesi zetu ndogo ndogo. Mishahara yao kwa kweli iko chini sana. Nakumbuka Mhe. Rais katika siku ya Sheria duniani nafikiri alilitolea kauli. Kwa kuwa Mheshimiwa umetenga fungu kwa ajili ya kurekebisha mambo ambayo hawa watu waliokuwa hawajapata fursa ya kuangaliwa mishahara yao. Naomba Mahakimu wa Mwanzo. Hili nitakuja kuzuia kifungu kwa ajili ya kuja kupata maelezo ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika suala zima la hivi vibali vya ajira za muda walioomba. Mimi nadhani sheria tuliyoipitisha, kuna taasisi maalum ambazo ni *professional* ambazo ni adimu kupatikana. Hizi nyengine Mheshimiwa kwa kweli watu wengi wapo sasa hivi, vijana wetu wengi wapo waliomaliza chuo wanaweza wakashika nafasi hizo. Lakini ili kujiridhisha kwa kweli tunakwenda katika utawala bora hebu tuletee yale maombi ya wale walioomba ajira ya mikataba ili tuthibitishe je, wale walioomba na zile nafasi walizoomba ni kweli *profession* ambazo ni adimu ili tuweze kujiridhisha.

Jengine nataka nikupongeze sana Mhe. Waziri kwamba msikivu. Katika kikao kilichopita tulizungumzia tunataka uwe na *data base* ya kuangalia wafanyakazi wetu. Lakini vile vile mahitaji, Mheshimiwa umetuletea *data* nzuri hapa lakini naomba mwaka huu umetoa ajira nafikiri karibu elfu mbili na kitu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda, utamalizia kesho.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunashukuru kwa michango tuliyoanza asubuhi na hivi jioni, lakini bado tunao wachangiaji wengi. Tunaomba kesho tukijaaliwa tuje mapema tuweze kumaliza michago hii. Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao hadi kesho siku ya Alkhamis, tarehe 05/07/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 05/07/2012 saa 3:00 asubuhi)